# *NYIMBO ZA MUNGU*

**NM**

**Saisie par Frère Dieudonné MW**

# *NYIMBO ZA MUNGU*

| | |
|---|---|
| **C.V.** | **Chants de Victoire** |
| **C.H.** | **Choice Hymns** |
| **H.W.** | **Hymns of worship** |
| **I.H.** | **Inspiring Hymns** |
| **R.S.** | **Rédemption Songs** |
| **S.S.S.** | **Sacred Songs and Solos** |
| **H.T.P.** | **Hymns of Truth and Praise** |

**G-4/4** **KUSIFU 1**

1. Musifu Mungu kwa baraka
   Musifu Mungu, watu wote,
   Musifu Mungu, malaika,
   Musifu Baba, Mwana, Roho.

Cfr/ RS 951 CH543 HW282

**G-3/4** **KUSIFU 2**

1. Heshima na sifa kwake Baba mbinguni,
   Aliyetupenda zamani na sasa.

   *Haleluya, usifiwe ! Haleluya, Amina !*
   *Haleluya, usifiwe ! Haleluya, Amina !*

2. Heshima na sifa kwake Yesu Mwokozi,
   Alitukufia kwa 'jili ya zambi.

3. Heshima na sifa kwake Roho ya nuru,
   Anashuhudia Mwokozi na damu.

Cfr/ RS 36 CH31 IH366

**Ab-6/8** **KUSIFU 3**

1. Sifu ! Sifu ! Yesu Mwokozi wa watu !

Imba kutangaza mapenda yake !
Malaika vile, Mulete heshima ;
Jina lake kweli ni takatifu !
Bwana Yesu anatulinda sana,
Kama mushungaji anatubeba.

*Sifu ! Sifu ! Yesu Mwokozi wa watu !*
*Sifu ! Sifu ! Imba ukubwa wake*.

2. Sifu ! Sifu ! Yesu Mwokozi wa watu !
Kwa makosa alitukufilia ;
Kristo, Mwamba, matumaini ya roho
Alitukomboa na damu yake.
Imba sifa kwake aliyeteswa
Kwa kutuonyesha mapendo yake.

3. Sifu ! Sifu ! Yesu Mwokozi ... watu !
Kule mbingu wanamwimbia sifu ;
Yesu Kristo, mwenye kushinda daima,
Ni Mufalme, Nabii, Kuhani wetu.
Atakuja kwa kutawala hapa,
Yesu mwenye enzi na utukufu.

Cfr/ RS 312 CH324 IH223 SSS208

## F-4/4 KUSIFU 4

1. Tunaimba sasa nyimbo kwake Yesu,

Nyimbo za furaha, nyimbo za wokovu ;
Yesu Mukombozi, Mwana wake Mungu,
Ni Mwokozi wetu, na tunamwabudu.

*Kazi zake zote zinatengenea ;*
*Kule kwake mbingu atatupokea.*

2. Watu wa zamani walimuchukia,
Walimushitaki, na walimupiga ;
Ju-u ya kalvari walimutundika,
Yesu alikufa kwa kutuokoa.

3. Ndani ya kaburi alilala kimya,
Hakubaki pale, alifufuliwa ;
Alikwenda Ju-u kwake, Mungu Baba,
Atarudi tena kwa kutukamata.

4. Kwa maisha yetu hapa kwa dunia,
Yesu anachunga, anatuombea,
Kwa wakati wote anatusaidia,
Tumusifu sana, tumufurahie !

Cfr/ RS 418 CV224 IH485 SSS652

**Eb-4/4** **KUSIFU 5**

1. Mungu Mutakatifu, Mungu mwenyezi,
Tunakuimbia nyimbo, tunakuabudu ;
Baba, Mwana, Roho, wote ni mumoja,

Mutakatifu, ndiye wewe tu.

2. Mungu Mutakatifu, tunakusifu,
Jeshi la mbinguni wanatoa taji zao ;
Malaika wote wanakwabudu,
Mwanzo na mwisho, ndiwe wewe tu,

3. Mungu Mutakatifu, unafunikwa,
Macho ya wenye makosa yasikutazame ;
Wewe peke yako ni Mutakatifu,
Mukamilifu, ndiwe wewe tu.

4. Mungu Mutakatifu, Mungu mwenyezi,
Kazi ya mikono yako inakutukuza ;
Wewe mwenye nguvu, Mungu wa mapendo,
Mwenye rehema, ndiwe wewe tu.

Cfr/ RS 25 CH17 IH20 SSS22

**G-3/4** **KUSIFU 6**

1. Kuja, Mufalme wetu, tunakusifu sasa, tuna-abudu ;
Ee, utukufu kwako, wewe ni mushindaji,
Ututawale sisi, Mungu mwenyezi !

2. Kuja, Mwokozi Yesu, ili utubariki, tunakuomba ;
Utusaidie sisi utushindishe vile,
Tuwe watakatifu, tukupendeze.

3. Roho Mutakatifu, jaza mioyo yetu, utuongoze ;
Ututawale wote tusikuasi kamwe,
Una uwezo mwingi, roho wa Mungu.

4. Mungu Muju-u wa wote, tatu katika Moja, tunakusifu ;
Tuta-abudu kule kukutukuza vile,
Tutakapokuona kwako mbinguni.

Cfr/ CH21

**G-4/4** **KUSIFU 7**

1. Tusifu Jina lake Yesu, sisi watu wake ;
: : na taji tumuvike yeye Bwana na Mufalme : :

2. Wachaguliwa wake sisi, tuliokolewa
: : kwa njia ya ne-ema yake, Bwana na Mufalme : :

3. Kwa kila lugha na kabila katika dunia
: : wazidi kutukuza Yesu Bwana na Mufalme : :

4. Na mbele yake sisi sote tuanguke chini,
: : tuimbe sifa kwake Yesu Bwana na Mufalme : :

Cfr/ RS 1 CH2 CV17 SSS203

**G-4/4** **KUSIFU 8**

1. Mutazame utukufu wa Mwokozi wetu Yesu ;
Alibeba taabu kubwa, naye alishinda kufa.
Tia taji, Tia taji !
Yeye mushindaji kweli ! Yeye mushindaji kweli !

2. Mumuvike Kristo taji, nyara zake ndizo nyingi ;
Mwenye nguvu na mamlaka, sifa kwake kule mbingu.
Tia taji, Tia taji !
Kwa Mwokozi na Mufalme ! Kwa Mwokozi na Mufalme !

3. Wenye zambi kwa zihaka walimuvalisha taji ;
Watu wake kwa mapendo wanamutukuza sana.
Tia taji, Tia taji !
Sifa yake mutangaze ! Sifa yake mutangaze !

4. Shangwe kubwa kumwimbia nyimbo za kumutukuza ;
Yesu kwa pahali pake, utukufu uwe wake.
Tia taji, Tia taji !
Kristo, Bwana na Mufalme ! Kristo, Bwana na Mufalme !

Cfr/ HW84

**Ab-3/2** **KUSIFU 9**

1. Furaha kubwa kutangaza sifa ya Mwokozi,
Na utukufu wa Mufalme, ndiye Mungu wangu.

2. Ee Bwana wangu na Mufalme, usaidie sasa
Pahali pote nitangaze sifa yako kubwa.

3. Ee Yesu, Jina tamu sana kupunguza woga,
Ni dawa kwa wenye makosa kuponyesha roho.

4. Watumwa wa makosa Yesu anawafungua ;
Na damu yake inafaa kwa kuniosha mimi.

5. Wanaokombolewa wote, muheshimu Bwana,
Na mutangaze pa'li pote Yesu ni Mwokozi.

Cfr/ CH8 IH222

**Eb-3/4** **KUSIFU 10**

1. Nitaimba na kusifu Yesu Kristo Mukombozi ;
Aliacha utukufu, alikufa kwa kalvari.

*Nitaimba na kusifu Yesu Kristo Mukombozi ;*
*Imba na watakatifu wenye kukutana kwake*.

2. Nilikuwa mupotevu, Yesu alinitafuta ;
Ali-ita na mapendo, alinirudisha kwake.

3. Hata mimi ni zaifu, Yesu aliniokoa ;
Yeye kiongozi wangu anachunga kila siku.

4. Atachunga hata mwisho, atanipeleka kwake ;
Pale nitamutukuza kwa uzuri wake wote

Cfr/ IH103 CH23 SSS875

**Bb-4/4** **KUSIFU 11**

1. Ninafikili, Mungu Baba wangu,
Viumbe vyote ulivyoviumba
Vinaonyesha nguvu yako nyingi
Pahali pote pa dunia hi-i.

*: : Ninakusifu Mungu na Mwokozi,*
*Wewe mukubwa, wewe mukubwa : :*

2. Ninatazama miti na mauwa,
Ninasikia ndege za peponi,
Vilima na bahari kubwa vile
Zinaonyesha nguvu yako Mungu.

3. Ninafikili, Mungu ulituma
Mutoto wako kufa kwa kalvari,
Na damu yake inatoa zambi ;
Ninashangaa kuona pendo lile !

4. Yesu Mwokozi atarudi tena
Kunipeleka kwako, Mungu wangu ;
Nitafurahi, nitakushukuru,
Kukutukuza kwa ukubwa wako.

Cfr/ HTP 1

## Eb-3/4 KUSIFU 12

1. Tunataka kupa kwako sifa na heshima zetu,
   Yesu ndiwe kimbilio wetu sisi wenye zambi.

   *Tunakusifu wewe sasa na kwa milele,*
   *Tunaheshimu Jina lako zuri ;*
   *Tunakusifu wewe sasa na milele,*
   *Kwa pendo lako kubwa kwetu.*

2. Ulilipa ukombozi, na uzima unatupa ;
   Ndani yako ni wokovu na taraja na salama.

3. Tutaimba na furaha na watakatifu wote,
   « Wewe tu unastahili kupokea sifa yetu. »

Cfr/ CV18

## Eb-4/4 KUSIFU 13

1. Musingi wa kanisa ni Kristo, Bwana Yesu,
   Aliliumba vile kwa utukufu wake ;
   Na alilitafuta kutoka kwake mbingu,
   Na alilinunua na damu yake Safi.

2. Kutoka makabila kanisa liko moja,
   Na Bwana ni mumoja, ni Bwana wa kanisa.
   Wokovu ni mumoja kwa watu wa dunia,

Taraja vile moja, taraja ya mbinguni.

3. Katika taabu nyingi, mateso duniani,
Kanisa linangoja salama ya milele ;
Litakapowashinda adui na shetani,
Litapumzika mbingu pamoja na Mwokozi.

Cfr/ RS50 CH25 IH225 SSS228

**G-3/4** **KUSIFU 14**

1. Sifa kwa Bwana, mwenyezi, Mufalme, na Mwumba ;
Ee, nafsi yangu, usifu Mwokozi daima.
Wasikiaji, mukaribie Mwokozi,

2. Sifa kwa Bwana anayetawala na haki,
Mwenye kulinda na mwenye upole na pendo ;
Amekujibu mara kwa mara maombi,
Kukubariki zaidi.

3. Sifa kwa Bwana aliyeku-umba na 'kili ;
Na ananyosha mukono kwa kukuongoza ;
Saa ya huzuni yeye anakufariji,
Ukifichama kwa Bwana.

4. Sifa kwa Bwana, nisifu na moyo wa Shangwe ;
Mbele ya Mungu tufike kuleta asante ;
Acha sauti za watu wake wapenzi
Kumutukuza milele.

Cfr/ IH224

## Ab-4/4 KUSIFU 15

1. Ninashanga-a kabisa kwa pendo la Bwana Yesu,
Sababu alinipenda, na mimi ni mwenye uchafu.

*Ajabu tu, ajabu tu, wimbo wangu kwa milele ;*
*Ajabu tu, ajabu tu, pendo la Mwokozi kwami.*

2. Kwami Mwokozi shambani alinyenyekea Mungu ;
Na jasho kama matone ya damu ilianguka.

3. Na malaika wa Mungu walikarikia Yesu
Kumufariji kwa taabu aliyoipata kwami.

4. Aliyabeba makosa niliyoyafanya yote,
Na alikufa kwa muti kwa kunilipia deni.

5. Nitakapofika kwake, milele nitamusifu
Kwa pendo lake Mwokozi aliyenikufilia.

Cfr/ CH92 IH85

## Eb-4/4 KUSIFU 16

1. Niliposikia Yesu aki-ita nimwamini,
Nilijibu, « Bwana Yesu, ninataka kuwa wako. »

*Nitasifu Bwana Yesu, alikufa kwa makosa ;*
*Tutukuze Jina lake, damu yake inatusafisha.*

2. Njia ya Mungu ni diki, majaribu yanazidi ;
Nita-acha zambi zote, nitafuata Yesu pekee.

3. Heri Jina lake Yesu, alinipokea mimi,
Alinisamehe zambi na kuosha moyo wangu.

4. Utukufu kwake Baba, utukufu kwake Mwana,
Utukufu kwake roho, wao watakatifu ni mumoja.

Cfr/ IH24

**Eb-4/4** **KUSIFU 17**

1. Vika Mwokozi taji, kondo-o na Mufalme,
Majeshi yote ya mbinguni wanasifu sana !
Ee nafsi yangu, sifu aliyekukufia,
Mufalme wako, Bwana kwa milele na milele.

2. Vika Mwokozi taji, ni Bwana wa mapendo,
Vidonda vyake utazame kwa mikono yake.
Ni neema kubwa sana kwa watu wa makosa,
Ee tunashangilia sana, tunamutukuza.

3. Vika Mwokozi taji, ni Bwana wa uzima,
Aliyetoka kaburini, aliyefufuka.

Tunamwimbia sifa kwake aliyekufa
Kutuletea ukombozi, yuko hai milele.

4. Vika Mwokozi taji, ni Bwana wa mbinguni,
Aliyetuma Roho kwetu toka Baba Mungu.
Tutoe sifa kwako uliyetukufia ;
Ee Bwana wetu, utukuzwe sasa na milele.

Cfr/ CH10 IH212 HW46

**Ab-4/4** **KUSIFU 18**

1. Tusifu Mungu wa mbinguni, mwenye utukufu,
Aliyetuma Mwana wake kwa kutuokoa.

*: : Heri Jina lake, heri Jina lake,*
*Heri Jina la Yesu Bwana : :*

2. Ni ju-u ya majina yote, linakuzwa sana ;
Na malaika wanaabudu mwenye nguvu yote.

3. Mwokozi na Rafiki wetu alitukomboa ;
Shauri la wokovu wetu Mungu alitoa.

4. Ni Mwana wa Mufalme na Mukubwa wa salama ;
Atatawala kwa milele, Bwana na Mushinda.

Cfr/ CH4 IH5

**G-4/4** **KUSIFU 19**

1. Napenda kuimbia Bwana sifa, nimekombolewa !
Ni wimbo ju-u ya Mwokozi wangu, nimekombolewa !

*Tangu nilikombolewa,*
*Tangu nilikombolewa ninasifu Jina lake !*
*Tangu nilikombolewa ninasifu Jina la Mwokozi !*

2. Ninafurahi sana kwa Mwokozi, nimekombolewa !
Nataka sana kumutumikia, nimekombolewa !

3. Najua kweli mimi mwana Wake, nimekombolewa !
Nitamutegemea sikuzote, nimekombolewa !

4. Na nitaka-a kwa milele kwake, nimekombolewa !
Kumutukuza, kumusifu yeye, nimekombolewa !

Cfr/ RS379 IH279 CH76

**F-4/4** **KUSIFU 20**

1. Ee siku ya pumziko na siku ya furaha,
Na siku kasahau mateso ya dunia ;
Ni siku yake Bwana, Mwenyezi wa mbinguni,
Ni siku takatifu kusifu Mungu wetu.

2. Kwa siku hii zamani ilitokea nuru,

Na siku hii Mwokozi alifufuka vile ;
Hii siku vile Roho wa Mungu alifika,
Na hivi mara tatu ni siku kubwa sana.

3. Na leo duniani katika inchi zote
Waamini wanaitwa kusifu Mungu wao ;
Tunakusanywa vile kwa Jina lake Bwana,
Na kuabudu Mungu na kusikia Neno.

4. Chakula tunapata kwa Roho zetu leo,
Na vile raha tamu kutoka Mungu Baba.
Heshima iwe sana kwa Baba na kwa Mwana,
Na Roho 'takatifu ; watatu ni mumoja.

Cfr/ IH13

**G-3/4** **KUSIFU 21**

1. Hata juma hili, Bwana, umechunga watu wako ;
Hivi leo tuko hapa kuingia nyumba yako.
:: Kuja, Bwana, kubariki, kwani tunakungojea ::

2. Sasa tunaomba, Mungu, usamehe zambi zetu,
Na uoshe roho zetu tuwe safi mbele yako.
:: tupumzike ndani yako toka mambo ya dunia ::

3. Tunakuja kukusifu, kweli wewe ni karibu ;
Tunataka kutazama utukufu wako, Bwana,
:: Hivi tuna hamu sana kuingia kwako mbingu ::

4. Tuma Neno lako, Mungu, kufundisha watu leo,
Wapotevu wa-amini na kuacha zambi zao.
:: Hivi tukutane, Bwana, hata utakaporudi ::

Cfr/ IH14

**Bb-4/4** **KUSIFU 22**

1. Ee Bwana, tunasifu mapendo yako sana
Tunashanga-a kweli, tunapokutazama ;
Kwa sisi ulikuja kwa kutukufilia,
Tupate usamehe, tufike kwako mbingu.

2. Taraja yetu iko kufika kwako, Bwana,
Na kutazama uso waliou-umiza ;
Faraja ya mioyo na sifa ya midomo
Katika majaribu, furaha na salama.

3. Mwokozi wetu Yesu, pokea shukurani.
Uliyevumilia makosa, haya vile ;
Na sasa unangoja kutufikisha kwako ;
Unastahili kweli kupata utukufu.

Cfr/ HW107

**Eb-6/4** **KUSIFU 23**

1. Damu ya Kristo imeniokoa,
Na nimezaliwa mwenye roho mupya ;
Ee sifa kwa Baba na sifa kwa Mwana,
Damu ya Kristo imeniokoa !

*Sifa ! Sifa ! Mwokozi amenisamehe makosa !*
*Sifa ! Sifa ! Kwani damu ya Kristo imeniokoa !*

2. Damu ya Kristo imeniokoa,
Furaha mbinguni kwa kazi ya Bwana !
Mutoto wa Baba, na vile muriti,
Damu ya Kristo imeniokoa.

3. Damu ya Kristo imeniokoa,
Na Baba alinisamehe makosa ;
Ee bei ya damani ni kufa kwa Bwana ;
Damu ya Kristo imeniokoa !

4. Damu ya Kristo imeniokoa,
Utatu wa Mungu wapate heshima ;
Ee sifa kwa Baba na Mwana na Roho,
Damu ya Kristo imeniokoa !

Cfr/ CH151

**D-4/4** **KUSIFU 24**

1. Mwokozi alitukufia, Mwokozi mukubwa !
Kwa damu tumeokolewa, Mwokozi mukubwa !

*Ee Mwokozi mukubwa ni Yesu, ni Yesu ;*
*Ee Mwokozi mukubwa ni Yesu Mupendwa.*

2. Na sifu Yesu kwa wokovu, Mwokozi mukubwa !
Na upatano naye Mungu, Mwokozi mukubwa !

3. Amesafisha moyo wangu, Mwokozi mukubwa !
Na sasa ananitawala, Mwokozi mukubwa !

4. Anatembea nami sasa, Mwokozi mukubwa !
Ananichunga na salama, Mwokozi mukubwa !

Cfr/ RS 103 CH46 IH116 SSS119

**Ab-3/4** **KUSIFU 25**

1. Tunasifu Bwana Yesu kwa furaha na kwa nguvu ;
Tukijua deni yetu, tujitoe kwake.

2. Tunavikwa na silaha kupigana na Shetani ;
Kwa imani tunaweza kumushinda kweli.

3. Tumutegeme-e sana, yeye tu ni mwaminifu ;
Kweli kitu hakiwezi kututenga naye.

4. Bwana, utuchunge kwako kwa imani na mapendo
Hata siku ya kuona utukufu wako.

5. Tutakuwa pale kwako, tutapata sura yako,
Vitu tusivyoona bado tutavipokea.

Cfr/ CH21 HW285 SSS505

**C-3/4** **KUSIFU 26**

1. Yesu, Mwanzo wa uzima, tunaishi kwako, Bwana ;
Ulishinda Diabolo, haya, woga, vile kufa.
Ulipita kwa mateso kwa kuturudisha kwako ;
*:: Mashukuru elfu elfu yawe kwako kwa milele ::*

2. Bwana Yesu, ulipata fimbo na kuzarauliwa ;
Wewe Bwana wa wabwana, walikuvalisha miiba ;
Wewe ulituokoa kwa vifungo vya makosa ;
*:: Mashukuru elfu elfu kwako, Bwana na Mwokozi ::*

3. Walitia haya nyingi ju-u yako, Ee Mwokozi ;
Ulitubebea yote kwa kuleta ukombozi.
Kwa uchungu wako, Bwana, tunaweza kuokoka ;
*:: Mashukuru elfu elfu kwako, Bwana na Mwokozi ::*

4. Sifa ya mioyo yetu tunakupa, Bwana Yesu ;
Kwa mateso na mauti uliyopokea yote.
Ulidumu kwa huzuni kwa kutupatia raha ;
*:: kwa milele tutaimba mashukuru kwako, Bwana ::*

Cfr/ HW74

**Ab-6/4** **KUSIFU 27**

1. Ninaheshimu Yesu Kristo kwa uzuri wake ;
   Mwenye kuva-a taji njema kwa kiti cha ufalme,
   Kwa kiti cha ufalme.

2. Na hatuwezi kumufananisha na mwingine ;
   Anawapita na uzuri watakatifu wote,
   Watakatifu wote.

3. Aliniokoa nikizama ndani ya makosa,
   Na alinikomboa mimi kwa musalaba wake,
   Kwa musalaba wake.

4. Uzima na furaha yote ananipa bule,
   Na ananishindisha sana kwa zambi na kaburi,
   Kwa zambi na kaburi.

5. Sababu ananionyesha hivi pendo lake,
   Maisha yangu yote pia nitayatoa kwake,
   Nitayatoa kwake.

Cfr/ CH320 IH369

**Bb-3/4** **KUSIFU 28**

1. Tunakushukuru, Mungu, kwa Mwokozi wetu Yesu,
   Na kwa kila neno jema tunalopokea kwako,
   Kwa mashamba na mavuno, jua, mvua, na chakula ;

Tunakushukuru sana kwa salama toka mbingu.

2. Tunakushukuru vile kwa ruhusa ya kuomba,
Na asante kwa uwezo wa kushinda majaribu,
Kwa ubaya, kwa uzuri, kwa faraja yako tamu,
Na kwa neema bora kwetu, kwa mapendo yako, Mungu.

3. Tunakushukuru sana kwa baraka zako zote,
Na kwa nyumba zetu vile, na jama-a, na rafiki,
Kwa huzuni, kwa furaha, kwa salama nawe, Mungu ;
Tunakushukuru sasa kwa taraja ya milele.

Cfr/ IH119

**Eb-3/4** **KUSIFU 29**

1. Ee Mungu Baba, ninakutukuza,
Uaminifu wako ni mukubwa,
Huruma zako hazitapunguka,
Hutageuka hata kwa milele.

*Ee wewe Mungu wangu, ni mwaminifu kweli,*
*Siku kwa siku unanibariki ;*
*Vyote ninavyo uliniletea,*
*Uaminifu mukubwa wa Mungu !*

2. Jua na mvua na mwezi na nyota,
Bonde, milima, mashamba na mito,
Yote inashuhudia pamoja

Uaminifu wa Mungu Mwenyenzi.

3. Ulisamehe uovu na zambi,
Na ulinipa salama rohoni ;
Wewe mwenyewe unaniongoza,
Shangwe ya kweli unaniletea.

4. Mimi zaifu, unanipa nguvu ;
Moyoni mwangu taraja ni tamu ;
Siku kwa siku baraka ni nyingi.
Elfu na elfu unanimwangia.

Cfr/ CH277 IH403

**Ab-3/4** **KUSIFU 30**

1. Abudu Mufalme, mwenye utukufu,
Kwa nyimbo tangaza mapendo wa Mungu ;
Ni mwumba, Mwokozi, Rafiki, Mulinzi ;
Tusifu uzuri wa Mungu Mwenyezi.

2. Mwenye nguvu nyingi, mwenye neema vile,
Mwenye kufunikwa kwa macho ya watu.
Ni Mungu Muju-u, ni Mungu wa nuru ;
Inama kusifu na kumushukuru.

3. Mapendo ya Mungu makubwa kabisa !
Hatuna maneno kwa kuyaeleza ;
Pahali po pote tunayatambua,

Na yanazijaza dunia na mbingu.

4. Na vile viumbe tunavyoviona
Vinashuhudia ukubwa wa Bwana ;
Musingi wa inchi ni tangu zamani,
Unashimamishwa imara milele.

Cfr/ RS 73 IH407 SSS13

**G-4/4** **KUSIFU 31**

1. Tumukaribie Mungu kumusifu na asante ;
Amebarikia shamba, na chakula tumepata ;
Mungu wetu anajua mahitaji yetu yote ;
Hivi tumwimbie Bwana wimbo wetu wa mavuno.

2. Ulimwengu wetu huu ndio shamba lake Mungu ;
Mbegu njema na magugu yanamea kandokando ;
Kwanza jani, kisha suke, na nafaka inaota ;
Utuchunge, Mungu Baba, sisi ni nafaka yako.

3. Bwana Yesu atakuja, atavuna shamba lake ;
Siku ya mavuno yake ataiokota ngano ;
Naye atateketeza kila kitu cha uovu ;
Ngano njema ataweka na kuchunga kwa milele.

4. Hata hivi kuja, Bwana, kwa kuvuna shamba lako ;
Ukusanye watu wako, huru toka zambi zao ;
Kule mbingu watu safi wataona uso wako ;

Kuja tu na malaika kwa mavuno ndiyo mwisho.

Cfr/ IH15 SSS1055

**Ab-3/4** **KUSIFU 32**

1. Kwa Mungu Muju-u uwe utukufu,
Sababu ya yote aliyoyafanya ;
Alitutumia Mwokozi muziri,
Ndiye Mwana wake kwa 'jili ya zambi.

*Tutukuze, tutukuze Jina la Mungu wetu !*
*Tutukuze, tutukuze na tumufurahie !*
*Ee kuja kwa Baba, kwa Yesu Mwokozi,*
*Na umutukuze, Mukubwa zaidi !*

2. Ametukomboa, ametununua
Kwa njia ya damu iliyo damani ;
Mwenye zambi nyingi anayeamini,
Anasamehewa kwa siku yenyewe.

3. Kwa Mungu Muju-u uwe utukufu ;
Tumufurahie kwa Jina la Yesu ;
Furaha kuliko tutakuwa nayo
Wakati tutakapomwona na macho.

Cfr/ CV6 CH29 IH227 SSS23

**F-6/8** **KU ABUDU 33**

1. Yesu, unitazamishe musalaba wako,
Nisikusahau wewe na mauti yako.

*Musalaba wako, Bwana, ni taraja yangu*
*Hata nitakapokwenda kupumzika kwako.*

2. Nilitetemeka pale, mimi mwenye zambi ;
Kwa mapendo na rehema ulinipokea.

3. Yesu, unilinde huko, unifahamishe ;
Jinsi ulivyochukua zambi zangu zote.

4. Nitangoja na taraja na imani vile
Hata nitakapokwenda kwako kwa milele.

Cfr/ RS 390 IH62 SSS134

**F-9/8** **KU ABUDU 34**

1. Tazama Yesu ni kondo-o kwa musalaba wa kalvari ;
Kwa sisi alimwanga damu kwa musalaba wa kalvari.
Sauti yake usikie, « Eloi, lama sabaktani ! »
Tazama Yesu akikufa kwa musalaba wa kalwari.

2. Tazama damu inavuja kwa musalaba wa kalvari ;
Kutoka mbavu na mikono kwa musalaba wa kalvari.
Halafu giza kubwa sana lilitokea kwa dunia,

Mwokozi alikufa pale kwa musalaba wa kalvari.

3. Na sasa kazi imekwisha kwa musalaba wa kalvari ;
Alizishinda zambi zote kwa musalaba wa kalvari.
Na sasa njia kwake Mungu ni wazi kwa wenye imani,
Kwa maana Yesu alikufa kwa musalaba wa kalvari.

4. Alifufuka, alikwenda kwa Baba yake kule mbingu ;
Na anaketi kwa kuume ya Baba yake kule mbingu.
Tunainama kumwabudu, heshima kwako, Ee, Kondo-o !
Yesu, pokea sifa zetu, wewe Mwokozi kule mbingu.

**Eb-4/4** **KU ABUDU 35**

1. Bwana, Mufalme wa uzima, walikuvika taji ;
Nisisahau miiba ile uliyova-a kwami.

*Nisisahau Get'semane, nisisahau musalaba,*
*Nisisahau pendo lako na taabu kwa Kalvari.*

2. Uniongoze kwa kaburi lililo wazi sasa,
Pahali ulipofufuka na ulishinda kufa.

3. Kama Maria na zawadi ninainama kwako,
Kukuonyesha pendo langu ; uipoke-e, Bwana.

4. Niwe tayari kukufuata na musalaba wangu,
Ili nijue ushirika wa taabu ya kalvari.

Cfr/ CH315 IH396

## Bb-6/8 KU ABUDU 36

1. Yesu Mwokozi wetu mwema, yeye muzuri wa kupita ;
   Mungu mukamilifu ndiye Yesu Mwokozi wa kalvari.

   *Mwokozi wa kalvari, namupa roho yangu ;*
   *Alinikufilia, mwenye kubarikiwa !*

2. Ali-ikunywa kopo tele ya matukano taabu vile ;
   Alilipia zambi zote, Yesu Mwokozi wa kalvari.

3. Mwenye makosa anaweza sasa kupata usamehe ;
   Alimimia damu yake, Yesu Mwokozi wa kalvari.

4. Anafariji roho yangu, siku nyingine nitamwona ;
   Nitatukuza na shuk'rani Yesu Mwokozi wa kalvari.

5. Tutakutana kule mbingu kwa kulisifu pendo lako ;
   Tutafanana nawe pale, Yesu Mwokozi wa kalvari.

Cfr/ RS 202 CH60

## C-4/4 KU ABUDU 37

1. Pendo lilikusukuma, Yesu, kutukufilia ;
   Ulitubebea taabu, haya kwa makosa yetu.

Kisha ulifufuliwa, ulishinda kufa kweli ;
Na watakatifu wote watashinda kwa milele.

2. Sasa umekwenda mbingu, taabu zako zimekwisha ;
Makusudi yake Baba uliyatimiza pia.
Sisi ni kanisa lako, unatuombea sana,
Na kututengenezea pa'li petu kule kwako.

3. Sasa sisi wana wako, kwa sababu yake Roho,
Tunalia, Aba, Baba, bila haya, bila woga.
Deni yetu ya mapendo kwako iko kubwa sana,
Tumekutambua wazi, wewe Bwana wa salama.

4. Ni furaha kukusifu, unayetukuzwa ju-u,
Unatuonyesha wazi roho yako ya mapendo.
Ee pokea kuabudu kwa mioyo yetu yote,
Kwani ulimwanga damu ili sisi tuokoke.

Cfr/ CH239 HW119 SSS443

## Ab-3/4 KU ABUDU 38

1. Ee salama ya milele inatoka Baba Mungu ;
Ni salama ya kujua Yesu ni Mwokozi wangu.

2. Kwangu ni salama sasa kwa sababu yake Yesu ;
Alimwanga damu yake kuondoa zambi zangu.

3. Alikufu kuonyesha ana haki na mapendo,

Na kuleta wenye zambi njia kuingia mbingu.

4. Tunakuabudu, Kristo, wewe Mwana wake Mungu,
Na tunakusifi, Bwana, umeshinda zambi zote !

Cfr/ HW117 CH341

**Bb-4/4** **KU ABUDU 39**

1. Ee nini, Mungu wetu, ilikuvuta wewe
Kwa 'jili ya makosa kutoa Mwana wako ?
Mapendo tu yalikuvuta kwa kutoa Mwana wako,
Kwa kutoa Mwana wako.

2. Ee nini, Bwana Yesu, ilikuleta hapa
Kumwanga damu yako, kupata maumivu ?
Mapendo tu yalikuleta kwa kumwanga damu yako.
Kwa kumwanga damu yako.

3. Ee nini, Mungu wetu, ulimutuma Roho
Ajaze roho zetu na pendo na salama ?
Mapendo tu yalitumia watu wako Roho yako,
Watu wako Roho yako.

4. O tutakupa nini kwa neema yako kubwa ?
Tuzidi kwa milele kusifu Jina lako !
Na sasa tunakuabudu kwa mapendo yako, Mungu,
Kwa mapendo yako, Mungu.

Cfr/ HW132

## Eb-4/4 KU ABUDU 40

1. Ni tamu sana Jina la Mwokozi Yesu Bwana,
Linafariji kwa huzuni, na kutoa woga.

2. Linaponyesha roho inayoumia sana,
Ni mana kwa kulisha roho, na kuleta raha.

3. Ni Mwamba wetu tunaosimama ju-u yake,
Na ngabo na pahali pa maficho vilevile.

4. Mwokozi, Muchungaji, na Rafiki na Kohani,
Lakini sifa za kufa-a utazipata mbingu.

5. Kutoka sasa tutapasha pendo lako kubwa ;
Kwa Jina lako kufa na kaburi tutashinda.

Cfr/ SSS112 RS 322 CH281 HW65

## D-3/4 KU ABUDU 41

1. Yesu, Yesu, Yesu, Jina tamu sana,
Linawasha roho na kuleta raha.

2. Yesu, Yesu, Yesu, anatoa zambi ;
Yesu, Jina zuri linatufariji.

3. Yesu, Yesu, Yesu, nguvu analeta,
Vile uhodari kwa kushinda vita.

4. Yesu, Yesu, Yesu, Jina la kushinda
Majaribu yote hapa kwa dunia.

5. Yesu, Yesu, Yesu, ni furaha kwetu
Kwa maisha yote, vile kule mbingu.

Cfr/ CH311 IH246

**Ab-3/2** **KU ABUDU 42**

1. Mwokozi wetu na Mupenzi, uliyetupenda,
Ulijitoa kwa ajili yetu wenye zambi.

2. Tunakupenda sana kwani ulipenda kwanza;
Mbinguni uliacha yote kwa kufika hapa.

3. Na ulika-a pale ju-u sawa na Mungu Baba ;
Ulijinyenyekeza sana kututumikia.

4. Ulikubali kukamata sura yetu, Yesu ;
Nawe ulifanyika mwili, wewe ndiwe Mungu.

5. Kwa hivi tutaonekana kama wewe, Yesu ;
Na tutakuwa wenye haki mbele yako ju-u.

6. Hakose kwa rafiki yetu sisi tutakufa,

Lakini ulikufa kwa wenye kukuchukia.

7. Tunakumbuka pendo lako kubwa sana kwetu,
Linalopita na zaidi pendo letu, Yesu.

Cfr/ SSS327 CH258

**F-6/4** **KU ABUDU 43**

1. Kwa kilima cha Kalvari, akiteswa – yeye nani ?
Kichwa chake na migu-u na mikono ni michungu,
Mbele alikuwa ju-u na furaha kule mbingu,
Mwana wake Mungu, ndiye
kule kwa Kalvari – pekee.

2. Kwa kilima cha kalvari, akifungwa – yeye nani ?
Watu wakimuzihaki, wakisema : « Shuka chini ! »
Yeye alifika hapa na mapendo na baraka,
Mwana wake mutu, ndiye kule kwa kalvari – pekee.

3. Kwa kilima cha kalvari, akikufa – yeye nani ?
Kwa ajili ya makosa yetu – si makosa yake.
Alilipa bei ya zambi, ni sadaka ya ahadi,
Ni kondo-o wetu, ndiye kule kwa kalvari – pekee.

4. Kule mbingu ni Mufalme, Mushindaji – yeye nani ?
Alikufa kwa dunia, bali juu anatukuzwa.
Ee tunainama kwake, anayestahili kweli,
Bwana wa wabwana ndiye, na Mufalme wa wafalme !

Cfr/ SSS227 CH309 HW163

## C-4/4 KU ABUDU 44

1.« Mutu wa masikitiko », Jina gani kwa Mwokozi,
Aliyetukufilia ! Haleluya, Bwana Yesu !

2.Sisi watu wa uchafu, yeye Mungu mwenye haki,
Alitutafuta sisi ; Haleluya, Bwana Yesu !

3.Aliacha Baba yake, akakuja duniani,
Akapata taabu nyingi ; Haleluya, Bwana Yesu !

4.Watu walimuzihaki, wakamupatisha haya,
Wakamuhukumu bule ; Haleluya, Bwana Yesu !

5.Yesu alisulubishwa, akalia : « Imekwisha, »
Alilipa zambi zote ; Haleluya, Bwana Yesu !

6.Atarudi kama Bwana na Mufalme wa wafalme,
Tutaimba kwa furaha, Haleluya, Bwana Yesu !

Cfr/ SSS102 RS 89 CH130 IH302

## Ab-3/4 KU ABUDU 45

1.Kukufikili wewe, Yesu, iko kutamu kwangu ;
Zaidi kukuona wewe, na kupumzika kwako.

2. Hakuna Jina tamu sana kuliko lako, Yesu ;
Inatushinda kufahamu uzuri wako wote.

3. Taraja kwa wenye kutubu na wenye kuanguka,
Unawahurumia wote wanaokutafuta.

4. Inatushinda kueleza mapendo yako, Bwana ;
Na ni wapenzi wako tu wanaoyafahamu.

5. Wewe furaha yetu pekee na taji yetu vile,
Na utukufu wetu, Bwana, sasa na kwa milele.

Cfr/ SSS60 RS 511 CH327 IH33

**Bb-3/4** **KU ABUDU 46**

1. Pendo lako, Bwana Yesu, linapita kila pendo ;
Ni furaha ya mbinguni, ni furaha yetu huko.
Yesu, wewe mwenye neema, vile mwenye pendo kubwa,
Utukaribie sasa, uingie roho zetu.

2. Yesu, sasa utujaze roho zetu na mapendo ;
Tunapata ndani yako yote tunayohitaji.
Uondoshe zambi zote tusizitamani tena ;
Tukikuamini kweli, tunapata kuwa huru.

3. Tunaomba utujaze na uzima wako, Bwana ;
Sisi ni hekalu lako, na huwezi kutuacha.
Tuna hamu ya kupata kukutumikia hapa,

Kukusifu sikuzote kama jeshi la mbinguni.

4. Umalize kazi yako, utukamilishe sisi ;
Tukikutazama sana, tufanane nawe Bwana,
Toka utukufu hata utukufu wake Mungu,
Hata tunafika mbingu mbele yako kuabudu.

Cfr/ SSS242 RS 67 CH12 IH83

## C-3/4 KU ABUDU 47

1. Najua Jina moja zuri kuliko kila Jina huko,
Kuniletea raha tamu, ni Jina hili, Yesu.

*Yesu Jina ziri sana ! Yesu, sikuzote sawa !*
*Yesu, tumwabudu sana na kumwimbia sifa.*

2. Napenda Jina hili jema, linanivuta kwake Mungu,
Kwa saa ya taabu na huzuni linafariji sana.

3. Siwezi mimi kueleza uzuri wake Jina hili
Lakini nitaimba sifa kwa Jina lake Yesu.

Cfr/ RS 4 CH361 IH9 CV8

## Eb-3/4 KU ABUDU 48

1. Inatushinda kufahamu mapendo yake Mungu kwetu,

Mapendo haya yanapita mapendo yetu sisi watu.
Alimutuma Bwana Yesu kutoka kwake mbinguni
Kututafuta, wenye zambi, tupate kusamehewa.

*Inatushinda kufahamu mapendo haha makubwa,*
*Lakini tunajua kweli yatabakia daima.*

2. Hata miaka inapita, vizazi vinakombolana,
Na hata watu wa dunia wanakata-a kuamini,
Mapendo ya Mungu ni sawa, makubwa sana na nguvu,
Tayari kuokoa wote wanaotubu makosa.

3. Ee Mungu mwenye pendo kubwa,
Unifundishe kukupenda,
Nipende vile watu wote na pendo unaonipenda.
Nataka sana, Bwana Yesu, mapendo yako makubwa
Yanisukume kukufuata, kukupendeza daima.

Cfr/ HTP39

**Bb-4/4** **KU ABUDU 49**

1. Ee Baba, nitakuwa kama Yesu,
Baraka ile alinipatia !
Ni mushangao na ajabu pia,
Kwa sura yake atanigeuza.

2. Ee Bwana Yesu, nani kama wewe
Alinipenda hata nitazame

Milele utukufu wako, Kristo,
Mimi zawabu ya mateso yako ?

3. Mapendo yako hayakustarehe
Mbele ya kubariki wana wako ;
Yanashiriki vitu vyote nasi,
Hata uriti wako, Bwana Yesu,

4. Wapenzi wako wote kwa milele
Kwa utukufu watakusanyika,
Na kwa furaha watakuzunguka,
Kukuabudu na kukutukuza.

Cfr/ SSS297 IH363 HW195

**Ab-3/4** **KU ABUDU 50**

1. Napenda kusikia Jina la Bwana Yesu Kristo,
Ni kama wimbo tamu sana kuliko kila Jina.

2. Linaonyesha pendo lake aliyenikufia,
Na damu yake ya damani iliyonikomboa.

3. Linanifurahisha roho, machozi yanakwisha,
Na linaniambia kwamba : « Usiogope kamwe. »

4. Pamoja na waamini wote, wenye kuokolewa,
Nitamwimbia Yesu sifa mbinguni kwa milele.

Cfr/ SSS663 RS 485 CH357 CV5

## G-6/8 KU ABUDU 51

1. Jina la pendo kubwa, Yesu Mwokozi,
Linalopita yote Yesu Mwokozi ;
Sisi hatuna kitu kukupendeza, Mungu.
Sharti utupe yote, Yesu Mwokozi.

2. Ulifanyika mwili, Yesu Mwokozi,
Na ulitoa damu, Yesu Mwokozi
Ulilishuhudia pendo lililo kubwa
Kuliko pendo lote, Yesu Mwokozi.

3. Na kwako tuna haki, Yesu Mwokozi,
Makimbilio letu, Yesu Mwokozi ;
Hatuna woga mwingi wa taabu na huzuni,
Kwako tunafichama, Yesu Mwokozi.

4. Utarudia tena, Yesu Mwokozi,
Kwa kutimiza raha, Yesu Mwokozi ;
Bwana, tutakuona, halafu tutakuwa
Sawa nawe milele, Yesu Mwokozi.

Cfr/ SSS581 CH300

## G-6/8 KU ABUDU 52

1. Ee Bwana, ulivumilia hukuma, mauti kwa mimi,
Kwami ulipata huzuni, mateso na miiba Kalvari ;
Na uli-ibeba azabu niweze kupata uhuru ;
Milele nitakushukuru,
Mwokozi na Bwana Mupendwa.

2. Ulivumilia laumu, zarau na vile zihaka,
Mapigo na haya, mateso, na mate ya wenye makosa ;
Kulipa makosa kwa mimi, ulisulibishwa, Ee Bwana ;
Milele nitakushukuru,
Mwokozi na Bwana Mupendwa.

3. Ee Bwana nitakushukuru kwa yote uliyoyabeba,
Mauti na giza na taabu, niweze kupata uzima,
Na vile nishinde milele nawe kule kwa utukufu ;
Milele nitakushukuru,
Mwokozi na Bwana Mupendwa.

Cfr/ HW128

**Eb-4/4** **KU ABUDU 53**

1. Tunapenda sas hii tamu kukumbuka musalaba
Wa Mwokozi wetu Yesu, sisi watu wa makosa.

2. Ustarehe tunapata kwa zabihu yetu Yesu,
Alitukomboa sisi, alilipa deni yetu.

3. Hapa mbingu ni karibu tunapotazama Yesu,

Kwani alitusamehe, Yeye mwaminifu.

4. Na imani tunafika mbele ya Mwokozi Yesu ;
Bwana nasi ni mumoja na hatutatengwa naye.

5. Twende kwake kwa akili, tufahamu nia yake,
Tujifunze sikuzote neema na rehema zake.

Cfr/ SSS316 RS 566 HW179

**Ab-4/4** **KU ABUDU 54**

1. Kwako pekee, Bwana, ni salama tamu.
Unajua taabu ya mioyo yetu ;
Ulitoka mbingu kwa kutuokoa,
Uliteswa sana kwa wenye makosa.
Si rafiki hapa, Bwana, kama wewe,
Kwa wenye huzuni hatuna mwingine.

2. Watu wa huzuni waje kwake Kristo,
Atatoa taabu, zambi, na mizigo ;
Yesu anaita : « Muje kwangu sasa, »
Kuna ustarehe tamu kwa mioyo.
Si rafiki hapa, Bwana, kama wewe,
Kwa wenye mizigo hatuna mwingine.

3. Hata mali yote ya dunia huko
Haileti raha kwa mioyo yetu ;
Wewe, Bwana Yesu, unatuletea
Kufurai sana, raha na salama.

Si rafiki hapa, Bwana, kama wewe,
Kwa roho ya kiu hatuna mwingine.

Cfr/ CH189

**F-4/4** **KU ABUDU 55**

1. Ninapo-ona Mwokozi wa watu
Kwa musalaba wa haya na taabu,
Ninahesabu faida yo yote
Kuwa hasara kwa 'jili yake.

2. Nisijisifu kwa kitu kingine,
Ila kwa kufa kwa Kristo Mwokozi ;
Vyote nilivyovipenda zamani,
Ninavitoa kwa Bwana yake.

3. Ona machapa kwa mbavu ya Kristo,
Na kwa mikono na vile migu-u ;
Yanaonyesha mapendo ya Mungu
Aliyokuwa nayo kwa watu.

4. Na kama ningalipata dunia,
Ndoko kabisa – zawadi kwa Bwana ;
Kwa pendo hili nitamutolea
Roho, maisha, na vitu vyote.

Cfr/ IH423 RS 573 CH385

## G-4/4 KU ABUDU 56

1. Mufalme wa utukufu, tunakuabudu sasa,
Na tunainama kwako, unapita wote pia !
Tunakutukuza wewe, njia zako nzuri zote

2. Mufalme wa utukufu, Bwana ya viumbe vyote,
Ulikataliwa hapa hata na taifa lako ;
Sasa tunakuheshimu wewe, mwenye utukufu.

3. Bwana wa uzima wetu, ulibeba taabu zetu,
Mupenzi wa Baba yako, Ee uliumia sana ;
Tunakukumbuka wewe, na kusifu Jina lako.

4. Kristo, utavikwa taji na mavazi ya kifalme,
Na tunakushuhudia kwamba wewe ni Mufalme ;
Ee tunakunyenyekea, Kristo, Bwana kwa milele.

Cfr/ CH317 RS 835 HW92

## F-3/2 KU ABUDU 57

1. Ninatimia ndani yako na ninapata haki kwako ;
Mauti yako, Bwana Yesu, ililipia deni yangu.

*Ninatakaswa nawe, Bwana, na ninahesabiwa haki,*
*Kwa damu ulinisamehe, na utanitukuza vile.*

2. Ninatimia ndani yako, makosa hayatatawala
Katika moyo wangu tena, uwezo wako umeshinda.

3. Umetimiza mahitaji ya roho yangu, Bwana Yesu ;
Ee wewe unafaa kabisa, sitahitaji kitu tena.

4. Wachaguliwa siku moja watakutana kwako, Bwana,
Na nitakuwa pale vile, nikitimia ndani yako.

Cfr/ CH265 HW129

**F-4/4** **KU ABUDU 58**

1. Ee Kristo, kwako roho yangu inakuta raha ;
Salama niliyotafuta nimepata sasa.

*Ee Kristo, wewe unafa-a kupumzisha roho ;*
*Salama, shangwe, na mapendo ninapata kwako.*

2. Nilitafuta raha pekee, sikukutafuta ;
Nilijaribu, pendo lako lilinikamata.

3. Nilijaribu upendezi wote wa dunia,
Lakini sikupata ustarehe na furaha.

4. Kipofu mimi, sikuona macho yako, Bwana,
Lakini sasa wema wako wazi ninaona.

Cfr/ SSS853 RS 301 CH140

**Eb-4/4** **KU ABUDU 59**

1. Nafsi yangu, angalia Yesu Mukombozi wako ;
Yeye ni kwa utukufu, mbali na makosa yote.

2. Anaketi kule mbingu, haki yake inanga-a ;
Anaionyesha damu, bei ya ukombozi wetu.

3. Alibeba zambi zote kwa kilima cha Kalvari,
Na hukumu imepita, Ee furaha kubwa sana !

4. Sasa Mungu anataka sisi tuwe kwake mbingu ;
Anatutengenezea vitu vyote taratibu.

5. Neno hili, « kwa milele », ni baraka ya kuzidi,
Wala kitu hakiwezi kututenga na Mwokozi.

6. Tumusifu Bwana wetu, sisi ni watoto wake ;
Tutaimba kwa milele, na tutafurahi kwake.

Cfr/ HW120

**Eb-4/4** **KU ABUDU 60**

1. Rehema ya kuhani wetu tunaikumbuka,
Na moyo wako unajaa na pendo kubwa sana.

2. Anafahamu majaribu, uzaifu wetu,
Sababu alijaribiwa kama sisi watu.

3. Makosa hayakuchafua Mukombozi wetu ;
Kondoo mutakatifu, yeye ni sadaka yetu.

4. Wakati alipotembea hapa kwa dunia,
Machozi mengi alitoa – anajua yetu.

5. Tukaribie kiti cha ne-ema bila woga,
Tupate neema kusaidia saa ya mahitaji.

Cfr/ HW147 ao 329

**D-9/8** **KU ABUDU 61**

1. Kwa kondo-o tunapumzika,
Kwa mapendo ya mushangao ;
Zambi zetu alisamehe, damu yake ilizitoa.

2. Sasa roho zetu za woga zinajazwa na raha tamu ;
Mungu Baba alipendezwa
Na sadaka ya Yesu Mwana.

3. Sasa woga hauko tena kwani damu ya Bwana Yesu
Mara moja iliondoa zambi zote kwa roho yangu.

4. Ninajazwa na raha tamu na ningali kwa ulimwengu ;
Kisha ngambo kwa utukufu nitakuta raha yenyewe.

Cfr/ HW115

**C-4/4** **KU ABUDU 62**

1. Ee Mungu ndiye nguvu yetu, raha, na taraja,
   Anachungaga watu wake sasa na milele.

2. Na hata mbele ya milima Mungu alikuwa ;
   Uwezo wake uliumba vyote duniani.

3. Miaka elfu ni kwa Mungu kama siku moja ;
   Milele Mungu yuko sawa, Jana, leo, kesho ;

4. Ee Mungu, Musaidizi wetu, tumaini vile,
   Utuongoze hata mwisho wa safari yetu.

Cfr/ SSS513 CH331

**F-4/4** **KU ABUDU 63**

1. Ee Bwana Yesu, Mwumba wa dunia,
   Mwana wa Mungu na mutu vile,
   Ninakupenda, ninakusifu,
   Wewe furaha yangu pia.

2. Shamba na mwitu, yote ni mizuri,
   Lakini unaipita mbali ;

Wewe ni mwema, mutakatifu,
Unayenipa shangwe kubwa.

3. Jua na mwezi inanga-a sana,
Pamoja na nyota za mbingu ;
Uzuri wako na utukufu
Unatushinda kufahamu.

Cfr/ IH78 CHS305 CV149

## G-3/4 MEZA YA BWANA 64

1. Kama ulivyoagiza, Bwana, ninafika meza yako
Kwa kukumbuka kufa kwako
Kwa mimi mwenye zambi.

2. Mwili wako uliovunjika ni mukate wa uzima,
Na damu iliyomwangika, agano jipya kwami.

3. Nikiona musalaba wako kwa kilima cha Kalvari,
Nakukumbuka na sadaka uliyonitolea.

4. Ninakukumbuka na matesa uliyoyabeba kwami ;
Ningali na maisha yangu nitakusifu wewe.

5. Hata saa midomo yangu hii itakapofungwa kimya,
Nitatangaza kufa kwako, na utanikumbuka.

Cfr/ IH91 HW333

## G-4/4 MEZA YA BWANA 65

1. Kwa mukate na kwa mvinyo, arabuni yake Roho,
Kwa maneno ya mapendo, tunakusifu, Bwana.

2. Mvinyo na mukate vile ni mufano wa mauti
Ya Mwokozi wetu mwema ; tunakusifu, Bwana.

3. Kwa maneno ya kitabu ya kuonyesha Yesu,
Na kutukokota kwake, tunakusifu, Bwana.

4. Kwa habari za mbinguni na kwa ufufuko wetu,
Na kukaa karibu nawe, tunakusifu, Bwana.

5. Huu mukate ni mufano wa Mwokozi akikufa,
Hakushindwa na mauti ; tunakusifu, Bwana.

6. Na kikombe ni mufano wa kutukumbusha damu
Uliyoimwanga yote, tunakusifu, Bwana.

7. Na kwa siku ya furaha utakaporudi kwetu
Kwa kupata utukufu, tunakusifu, Bwana.

Cfr/ HW153

## F-3/4 MEZA YA BWANA 66

1. Tunazunguka meza na Yesu katikati,
Kwa Kristo wote ni mumoja, hata sisi wengi.

2. Kwa zambi zetu Yesu alitukufilia,
Na tulikufa ndani Yake na tulifufuka.

3. Mukate na kikombe tunakamata sasa ;
Tunapumzika kwa kifua cha Mwokozi Bwana.

4. Tutatawala naye Mufalme Yesu Kristo ;
Tutafurahi kwa karamu, ndoa ya Kondoo.

Cfr/ HW191

**Eb-4/4** **UBATIZO 67**

1. Tunazikwa kwa kaburi la Mwokozi Yesu Bwana ;
Mungu anatuhesabu kuwa wafu kwa makosa.

2. Kufa na hukumu vile haziwezi kutugusa ;
Bwana alibeba yote, nguvu yao amemaliza.

3. Yesu alifufuliwa toka wafu, yeye kwanza ;
Nasi tumeumbwa tena, sisi ni wahuru sasa.

4. Ubatizo tunapata, sura ya mauti yake ;
Nasi tunafufuka naye, ndani yake tunakaa.

5. Tunangoja ukombozi wa mi-ili yetu vile ;
Atatugeuza pia kufanana naye Yesu.

6. Bwana, sasa tunataka kushiriki haya yako ;
Mungu atatupokea, kwani tuko ndani yako.

Cfr/ CH526

**F-3/4** **UBATIZO 68**

1. Uliagiza, Yesu Bwana, na ninazikwa kwa mufano,
Hivi ninatangaza wazi mimi ni mutu wako sasa.

2. Ninakutii kwa neno hili, ninakunyenyekea hivi,
Kwani nataka kukufuata hata katika ubatizo.

3. Huu ni mufano wa kaburi ulipozikwa ndani yake ;
Niki-ingia, natambua bei kubwa ya wokovu wangu.

4. Ninapotoka, ni mufano wa ufufuko wako, Bwana,
Na nitaishi mutu mupya, mimi si tena wa dunia.

5. Nijihesabu kuwa mutu kwa zambi zilizoku-ua,
Mufu kwa mambo ya dunia
Yasiyokupendeza, Bwana.

6. Ninapokutazama, Bwana, na utukufu wako wote,
Ninahesabu haya bule ninayobeba kwake hapa.

Cfr/ CH527 HW341

**C-3/4** **ROHO MUTAKATIFU 69**

1. Tangaza neno hili dunia isikie
Mwokozi ametuma musa-idizi kwetu ;
Wakristo pa'li pote wafarijiwe naye.
Musa-idizi yuko !

*Musa-idizi yuko, Musa-idizi yuko,*
*Ni Roho yake Mungu aliyetumwa kwetu ;*
*Ahadi yake nzuri inatimia kweli*
*Musa-idizi yuko !*

2. Kumbuka Roho huyu aliyetumwa kwetu
Anatukuza Yesu katika roho zetu ;
Na anawaongoza wenye kupenda Bwana,
Musa-idizi yuko !

3. Anatufunulia habari za maneno
Yatakayokua kwa mwisho wa dunia ;
Anayasema yote anayoyasikia,
Musa-idizi yuko

4. Na nina Roho huyu katika moyo wangu,
Ananifahamisha maneno yake Yesu ;
Ninashanga-a sana kwa neema yake Bwana,
Musa-idizi yuko !

Cfr/ SSS198 RS 536 IH152

## Eb-4/4 ROHO MUTAKATIFU 70

1. Mwokozi aliahidia wanafunzi wake
Kutuma Musaidizi kwao toka mbingu.

2. Kwa hivi Roho alikuja, naye anapanga
Katika roho ya mwenye unyenyekevu.

3. Katika kweli yote ana'ngoza wa-amini,
Maneno yake anayosikia kwake.

4. Anatukuza Yesu, naye anatutangaza
Habari za maneno yatakayokuja.

5. Matunda yake Roho ni mapendo na furaha,
Salama, neema, wema, na uaminifu.

6. Ee utujaze Roho yako, Mungu, tunaomba,
Apange kwetu kubakia sikuzote.

Cfr/ SSS191 RS 539

## Eb-6/8 BIBLIA 71

1. Maneno ya Mungu ni ta-a na nuru kwa njia yangu,
Kwa kunisafisha kwa zambi na kuniongoza kwake.

*Nimeficha Maneno ya Mungu*
*Moyoni nisimukose-e,*
*Nisimukose-e, nisimukose-e,*
*Maneno ya Mungu moyoni.*

2. Milele maneno ya Mungu yanasimamishwa juu ;
Yanatufundisha kujua Mwokozi ni mwaminifu.

3. Mapema, saa sita, usiku, nisifu Mwokozi wangu,
Sababu maneno matamu yananipatisha nguvu.

4. Biblia inatuambia Mwokozi ni Yesu Kristo ;
Anawaletea wokovu wanaopotea mbali

Cfr/ IH158

**Ab-4/4** **BIBLIA 72**

1. Biblia inasimama sana kama mwamba wa imara ;
Katika Biblia tunapata Neno la Mungu wa milele.

*Biblia inasimama sana, haitapunguka hata milele,*
*Na nitasimama kwa ngambo yote ju-u ya Biblia.*

2. Biblia inasimama sawa na mulima ju-u sana,
Na watu hawataweza kweli kuishinda na nguvu yao.

3. Biblia inasimama sana, kwa milele itashinda ;

Sababu Mungu aliandika ndani yake sheria zake.

4. Biblia inasimama kwani ni Kitabu chake Mungu ;
Nita-amini na nitadumu kuitii kwa maisha yangu.

Cfr/ CH465

**F-3/4** **BIBLIA 73**

1. Neno takatifu sana ni Biblia yake Mungu,
Nikisoma ndani yake inanifundisha sana.

2. Inanikemea vile ninapotembea mbali ;
Inanionyesha nji, na mapendo ya Mwokozi.

3. Inanifariji mimi ninaposumbuka sana ;
Niki-iamini kweli nitashinda hata kufa.

4. Inaniambia wingi wa furaha ya mbinguni ;
Ninapenda neno hili, ni hazina ya damani.

Cfr/ IH460

**G-3/4** **HABARI NJEMA 74**

1. Ni neema ya kunishangaza iliyoniokoa ;
Nilipotea, lakini Yesu alinivuta kwake.

2. Hukumu ya Mwamuzi Mungu niliogopa sana ;
Lakina sasa, kwa neema yake, sitaogopa tena.

3. Katika majaribu mengi nimesimama nguvu ;
Kwa neema yake alinichunga, hataniacha kamwe.

4. Tutashukuru Mungu wetu milele na milele
Kwa neema kubwa tuliyo-ona katika Mwana wake.

Cfr/ CH40 IH385

**Db-9/4** **HABARI NJEMA 75**

1. Mungu aliposifiwa mbinguni,
Zambi ilipoijaza dunia,
Yesu alitoka muji wa Baba
Awe Mwokozi kwa wenye makosa.

*Alinipenda, kunikufia,*
*Na alizikwa katika kaburi ;*
*Alifufuka na kuniokoa ;*
*Atarudia – Ee siku ya shangwe !*

2. Watu walimupeleka Kalvari,
Kwa misumari walimutoboa ;
Walimuzihaki na walizarau
Mwenye kubeba makosa ya watu.

3. Kufa hakuweza kumuzuiza

Mwana wa Mungu katika kaburi ;
Alifufuka kwa siku ya tatu,
Yeye Mushinda na Bwana ya yote !

4. Atarudia katika mawingu
Kwa kukamata wenye kumwamini ;
Tutafurahi kuona Mwokozi
Na tutaishi naye kwa milele.

Cfr/ IH137 CH143

**G-4/4** **HABARI NJEMA 76**

1. Nina neno toka Bwana, Haleluya !
Na neno hili nitakupa ;
Ma-andiko ya Kitabu, Haleluya !
Yanasema : « Utazame Yesu. »

*Utazame Yesu, ndugu, utazame Yesu sasa ;*
*Ma-andiko ya Kitabu, Haleluya !*
*Yanasema : « Utazame Yesu. »*

2. Nina neno la mapendo, Haleluya !
Ni neno, Ee rafiki, kwawe ;
Na ni neno toka ju-u, Haleluya !
Yesu Kristo alisema kweli.

3. Na uzima utapata, Haleluya !
Uzima wa milele, ndugu ;

Utazame Yesu sasa, Haleluya !
Yesu pekee atakuokoa.

4. Ninaweza kuhubiri, Haleluya !
Habari ya wokovu wangu,
Kuamini Jina lake, Haleluya !
Nimepata kwake tu uzima.

Cfr/ SSS411 RS 98IH231

**F-6/8** **HABARI NJEMA 77**

1. Dunia 'nalala kwa giza la zambi,
Nuru ni Yesu pekee ;
Mwenye utukufu anatuongoza,
Nuru ni Yesu pekee.

*Kuja kwa Nuru, anakuita,*
*Nimeipata kwa roho yangu ;*
*Mimi kipofu, sasa naona*
*Nuru ni Yesu pekee.*

2. Hatutatembea kwa giza kabisa,
Nuru ni Yesu pekee ;
Sababu tunafuata Yesu Mwokozi,
Nuru ni Yesu pekee.

3. Kwa wenye makosa, wenye kupotea,
Nuru ni Yesu pekee ;

Kwendeni kuoshwa na damu ya Yesu,
Nuru ni Yesu pekee.

4. Hawana hitaji la jua mbinguni,
Nuru ya mbingu Yesu ;
Kondo-o wa Mungu ni nuru ya muji,
Nuru ya mbingu Yesu.

Cfr/ SSS417 RS 157 IH335 CH167

**Eb-4/4** **HABARI NJEMA 78**

1. Mwokozi wangu alinimwangia damu yake ;
Kwa mwenye zambi, mwenye haki alitoa mwili.

*Kule kwa musalaba wa Yesu Mwokozi*
*Niliacha zambi zangu kabisa ;*
*Nilimupokea na nimeokoka,*
*Na sasa furaha inazidi.*

2. Makosa yangu yalifunga Yesu kwa Kalvari ;
Huruma na mapendo yake ni makubwa kweli.

3. Na giza lilificha Yesu pale kwa Kalvari :
Ajabu kubwa, Mwumba wangu alikufa kwami !

4. Siwezi kulipia deni kwa huzuni yangu,
Lakini nitatoa vyote kwa Mwokozi wangu.

Cfr/ IH55 CH33

**Ab-4/4** **HABARI NJEMA 79**

1. Moyo uligeuzwa na vile maisha, saa Yesu alipoingia ;
Nikapata uwezo na nuru moyoni, saa Yesu alipoingia.

*Saa Yesu alipoingia, saa Yesu alipoingia,*
*Haleluya kwa Yesu Mwokozi pekee,*
*Aliniokoa kabisa !*

2. Niliacha makosa na njia ya zambi, saa Yesu alipoingia ;
Naye alisamehe na alisafisha, saa Yesu alipoingia.

3. Nilipata salama iliyo ya mbingu, saa Yesu alipoingia ;
Woga uliniacha na shaka njiani, saa Yesu alipoingia.

4. Nilipata taraja ya kwenda mbinguni,
Saa Yesu alipoingia ;
Na furaha ilijaza roho kabisa, saa Yesu alipoingia.

Cfr/ IH280

**G-3/2** **HABARI NJEMA 80**

1. Ee siku ya kuokolewa ni kweli siku ya furaha ;
Kwa neema na mapendo kwangu,
Aliondoa zambi zangu.

*Siku kubwa ya furaha, mimi ni mutu wake sasa,*
*Ndiye anayeniongoza*
*Kumwangalia na kumwomba.*
*Siku kubwa ya furaha, mimi ni mutu wake sasa,*

2. Sitapotea tena kamwe, ananiita mwana wake.
Alinivuta kwa mapendo, nifuate mwito wake pekee.

3. Na tumekwisha kupatana ;
Mimi ni wake, yeye wangu.
Ninamushuhudia Yesu ; nitamutii, nitamufuata.

4. Furaha yake ninapata, ananijaza raha sasa.
Hakuna kitu wala mutu anayeweza kunitenga.
Cfr/ SSS866 RS 622 IH98 CV123

**Ab-4/4** **HABARI NJEMA 81**

1. Nilipofika kwa musalaba,
Nikanyanyua sauti yangu :
« Yesu Mwokozi, unirehemu ! » Akaniokoa.
Yesu asifiwe, Yesu asifiwe !
Alisikia kilio changu, Yesu asifiwe !

2. Nilipofika kwa Bwana Yesu,
Nikamusihi Mwokozi wangu :
« Unitakase, unisafishe ! » Akanisikia.
Yesu asifiwe, Yesu asifiwe !

Alisikia maombi yangu, Yesu asifiwe !

3. Ona kisima cha musalaba,
   Leo kingali cha nguvu sawa
   Kukuokoa na kusafisha, Yesu asifiwe !
   Yesu asifiwe, Yesu asifiwe !
   Kukuokoa na kusafisha, Yesu asifiwe !

4. Kuja kuoshwa katika maji
   Yaliyo damu ya Yesu Kristo ;
   Umusadiki, utatimizwa, Yesu asifiwe !
   Yesu asifiwe, Yesu asifiwe !
   Umusadiki, utatimizwa, Yesu asifiwe !

Cfr/ RS 192 IH376 CH55

**G-6/8** **HABARI NJEMA 82**

1. Yesu kwa muji wa Betelehemu
   Alizaliwa katika ta-abu ;
   Ninashangaa sababu Mwokozi alitafuta mimi.
   Alitafuta mimi, alitafuta mimi,
   Ninashangaa sababu Mwokozi alitafuta mimi.

2. Yesu Mwokozi, zamani Kalvari
   Deni ya zambi alinilipia ;
   Kunileteа uhuru wa kweli alinikufilia.
   Alinikufilia, alinikufilia,
   Kunileteа uhuru wa kweli alinikufilia.

3. Yesu Mwokozi alinikumbuka
Nami ningali tu mbali na Baba,
Na siku zote alinitafuta, akini-ita mimi.
Akini-ita mimi, akini-ita mimi,
Na siku zote alinitafuta, akini-ita mimi.

4. Yesu Mwokozi aliniahidi
Atarudia kutoka mbinguni,
Na nitamwona katika mawingu, atanitwa-a kwake.
Atanitwa-a kwake, atanitwa-a kwake,
Na nitamwona katika mawingu, atanitwa-a kwake.

Cfr/ SSS40 RS 115 IH110

**Bb-6/8** **HABARI NJEMA 83**

1. Nilizama kwa makosa, katika maji ya zambi ;
Roho yangu iliona kufa na giza tele ;
Mungu alinisikia nilipomulilia,
Akanipandisha na kuniokoa.

*:: Nimeokoka, nimeokoka,*
*Kwa Yesu Mukombozi nimeokoka ::*

2. Sasa Yesu amekuwa Makimbilio yangu ;
Pendo lake kubwa sana liko moyoni mwangu ;
Neema yake ya kuzidi inanijaza roho ;
Niwe mwaminifu kwake siku zote.

3. Nawe mwenye sikitiko, kuna matumaini ;
Yesu anakufahamu na atakusaidia ;
Atakupandisha toka tope la kuteleza ;
Upoke-e neema yake kwa wokovu.

Cfr/ IH84 CH95

**Eb-3/4** **HABARI NJEMA 84**

1. Bwana Yesu amesema : « Ee wewe ni zaifu ;
Angalia na kuomba kwa kupata nguvu kwangu. »

*Yesu alikufa kwa ajili yangu,*
*Aliziondosha zambi, furaha kubwa kwangu !*

2. Pendo la Mwokozi wangu limeyeyusha moyo ;
Ametoa zambi zangu na kiburi na uchoyo.

3. Sina kitu mukononi cha kunifaidia ;
Ni zaifu, muhitaji, Yesu, ninakulilia.

4. Mungu akinisaidia, nitamaliza mwendo ;
« Yesu alikufa kwami », nitaimba pale ngambo.

5. Siku moja nitafika mbinguni kwako, Bwana ;
Tutaimba sisi sote, tutakushukuru sana.

Cfr/ SSS855 RS 198 IH104 CH104

**C-4/4** **HABARI NJEMA 85**

1. Waisraeli kule kwa Misri walipaka-a miimo na damu,
Na malaika hakuingia
Kwa kuharibu mwana wa kwanza.

*Mungu akiona damu, damu yake Yesu Kristo,*
*Kweli kufa kutapita, kutapita kabisa kwa sisi.*

2. Kule Farao hakukubali kuwafungua watu wa Mungu ;
Hakuamini na hakuti-i, na alipata taabu kuzidi.

3. Mwenye makosa, kuja kwa Yesu, aliahidi kukuokoa ;
Atafunika zambi na damu, tena hukumu hutaipata.

4. Neema, rehema, pendo la Bwana,
Ni aminifu, kweli na kubwa ;
Makimbilio utayapata, damu inapitisha hukumu.

Cfr/ IH120 CH48

**G-3/4** **HABARI NJEMA 86**

1. Neema ya Bwana ni kubwa sana,
Kubwa kuliko zambi za watu,
Kule Kalvari tunaiona,
Pa’li pa kufa kwa Bwana Yesu.

*Neema yake inasamehe makosa yetu,*
*Neema yake kubwa kuliko uovu wetu.*

2. Tuko katika hatari kubwa,
Tutapotea tusipotubu ;
Neema ya Bwana inaonyesha
Yesu Mwokozi ni kimbilio.

3. Ndugu, huwezi kuficha zambi,
Mungu mbinguni anaziona !
Ee unataka kusukuliwa ?
Damu ya Yesu itakuosha.

4. Neema ya Bwana ni kubwa sana,
Iko tayari kwawe, Mupenzi ;
Kiri makosa, amini Yesu.
Atasamehe kwa neema yake.

Cfr/ IH416 CH119

**C-4/4** **HABARI NJEMA 87**

1. Yote ninayo niliyapokea
Kwa wema wake unaoenea ;
Mimi si kitu, namutegemea ;
Nimeokolewa kwa ne-ema.

*Niliyekuwa nimetoroka,*

*Kwa pendo lake nimeokoka !*
*Yesu ni mwema na mwenye rehema.*
*Nimeokolewa kwa ne-ema !*

2. Nilitembea zamani kwa zambi
Katika njia ya kufa, lakini
Yesu alinitafuta polini ;
Nimeokolewa kwa ne-ema.

3. Nimetakaswa na Yesu Mwokozi,
Si kwa matendo na si kwa machozi,
Ila kwa damu nina ukombozi ;
Nimeokolewa kwa ne-ema.

4. Raha ya mbingu imeni-ingia,
Kwa shangwe kubwa namufurahia.
Kwa kuwa Yesu 'nanirehemia ;
Nimeokolewa kwa ne-ema.

Cfr/ RS 605 CH132

**D-3/4** **HABARI NJEMA 88**

1. Ne-ema, neno tamu kwa masikio yangu,
Ni wimbo wa mbinguni ju-u, dunia isikie.

*Nimeokolewa na ne-ema pekee ;*
*Yesu Kristo alikufa kwami na watu wote.*

2. Kwa neema Jina langu lina-andikwa mbingu,
Na neema ilinipeleka karibu naye Yesu

3. Kwa neema njia yako ni wazi mbele yangu ;
Ninapokea kwa ne-ema ninayoyahitaji.

4. Kwa neema ninaweza kuomba Mungu Baba ;
Ni neema inayonichunga mupaka saa ya kufa.

5. Uache neema yako kuniendesha mbele,
Unipe neema kujitoa kwawe, Mwokozi wangu.

Cfr/ SSS8 IH108 CH83

**C-6/8** **HABARI NJEMA 89**

1. Pendo la Mungu ni kubwa, pasha habari hizi ;
Pendo la Mungu ni kubwa, mwanzo wa nyimbo zote ;
Na malaika mbinguni walihubiri dunia ;
Mutu wa zambi, sikia, pendo la Mungu ni kubwa !

*Pendo kubwa, pendo kubwa,*
*Pendo kubwa, pendo la Mungu ni kubwa !*

2. Pendo la Mungu ni kubwa kwako uliye mbali ;
Pendo la Mungu ni kubwa, yeye anakuita.
Toka kilima Kalvari, tangu ku-umba dunia,
Limeonyeshwa hakika, pendo la Mungu ni kubwa !

3. Pendo la Mungu ni kubwa, kutuletea raha ;
Pendo la Mungu ni kubwa, tutafurahi sana.
Tutakutana mbinguni na waliotangulia,
Na tutaimba pamoja : « Pendo la Mungu ni kubwa. »

Cfr/ IH69 CH69

## G-6/8 HABARI NJEMA 90

1. Imba Neno la Mungu tena, Neno lenye uzima ;
‘Nionyeshe uzuri wake, Neno lenye uzima.
Linaleta uzima, linaleta imani.

*Neno la kweli, Neno la ‘jabu,*
*Neno la Mungu na uzima ;*
*Neno la kweli, Neno la ‘jabu,*
*Neno lenye uzima.*

2. Kristo mwenye mapendo yote anakuita sasa ;
Mwenye zambi, sikia Yesu, anakuita sasa
Analeta uzima kwa kufika mbinguni.

3. Uhubiri Habari Njema, Neno lenye uzima.
Linaleta salama kubwa, Neno lenye uzima.
Yesu ni Mukombozi kuokoa milele.

Cfr/ SSS357 IH163 CH156

**Eb-4/4** **HABARI NJEMA 91**

1. Yesu aliniokoa toka zambi,
Ni Mwokozi muzuri kwa mimi ;
Yesu alinifungua toka woga,
Ni Mwokozi muzuri kwa mimi.

*Yesu Mwokozi muzuri kwa mimi,*
*Ni Mwokozi muzuri kwa mimi ;*
*Toka zambi zangu aliniokoa,*
*Ni Mwokozi muzuri kwa mimi.*

2. Ni Rafiki mwenye neema na mapendo,
Ni Mwokozi muzuri kwa mimi ;
Mahitaji yote ninapata kwake,
Ni Mwokozi muzuri kwa mimi.

3. Yeye ni karibu kwa kunifariji,
Ni Mwokozi muzuri kwa mimi ;
Ananisamehe zambi zangu zote,
Ni Mwokozi muzuri kwa mimi.

4. Pendo langu kwaye linaongezeka,
Ni Mwokozi muzuri kwa mimi ;
Neema yake tamu inaniongoza,
Ni Mwokozi muzuri kwa mimi.

Cfr/ IH259

**Ab-6/4** **HABARI NJEMA 92**

1. Dunia ya zambi haileti furaha
Kama Neno la Mungu kwa mimi,
Sawa Yesu Mwokozi alivyobeba zambi,
Na damu inazifunika.

*Damu inazifunika ubaya na zambi zangu,*
*Hukumu na taabu Yesu alizibeba,*
*Na damu inazifunika.*

2. Mapigo ya Yesu na mi-iba mikali
Yote yanaonyesha mapendo ;
Nikiona Kalvari nina haya kwa zambi,
Na damu inazifunika.

3. Nilimutazama kule kwa musalaba
Na ajabu kwa neema ya Mungu ;
Nilipiga magoti zambi zangu kukiri,
Na damu inazifunika.

4. Ninamushukuru kwani alinunua
Roho yangu na bei ya damani ;
Na furaha na nyimbo ninamusifu sana
Kwa damu inayofunika.

Cfr/ IH96 CH59

**Db-4/4** **HABARI NJEMA 93**

1. Rafiki, muyasikilize sasa mafundisho yetu
   Yanayoweza kusaidia na kuwaokoa watu.

   *Nani anaokoa watu ?*
   *(Mwana wa Mungu kwa Kalvari)*
   *Kwa njia gani ? (Kutukufia)*
   *Na yuko wapi ? (Amini)*
   *Mbinguni anatuombea.*

2. Hakuna malaika ju-u aliyeliweza hili ;
   Mwenye kuteswa kwa Kalvari
   Alikuwa Mungu Mwana.

3. Ni Neno la kutushangaza na kuwasha roho zetu ;
   Yesu, kuhani letu, sasa anatuombea juu.

4. Utapokea Yesu sasa, na utamunyenyekea ?
   Ataijaza roho yako na uwezo na furaha.

Cfr/ RS881 CH131

**Eb-6/8** **HABARI NJEMA 94**

1. Mwokozi Yesu alikwenda kule kwa Kalvari,
   Alitukufilia pale kwa kutuokoa.

   *Mapendo gani ya Mwokozi ! Tumupende sana,*
   *Na tuamini damu yake, tumutumikie.*

2. Inatushinda kufahamu aliyoyabeba,
Lakini tunajua alitukufilia sisi.

3. Kwa kusamehe zambi zetu Yesu alifufa,
Kwa damu tuokoke na tufike kwake mbingu.

4. Mwingine hakufaa kutulipia deni yetu ;
Mwokozi pekee aliweza kufungua mbingu.

Cfr/ SSS1134 IH458 CH179

## G-6/8 HABARI NJEMA 95

1. Kwa pendo lake kubwa Mwokozi alikuja,
Na alinitafuta katika poli mbali ;
Na malaika wali-imba na furaha ju-u yangu.

*Alinitafuta, akaniokoa,*
*Akaniondosha kwa mabaya.*
*Akanirudisha kwake Mungu.*

2. Kwa zizi lake zuri alinibeba tena,
Na aliniambia, « Wewe ni wangu sasa. »
Sauti yake ya mapendo ilinifariji sana.

3. Ninakumbuka jinsi alivyotoa damu,
Ninakumbuka vile mi-iba na mateso,
Mwokozi alibeba yote kwa sababu ya mapendo.

4. Ninakufua, Yesu, katika nuru yako ;
Ninakumbuka sana baraka yako nyingi ;
Milele nitaendelea kukusifu kwa furaha.

Cfr/ SSS59 RS141 IH446 CH101

## Ab-3/4 HABARI NJEMA 96

1. Umesoma habari za musalaba wa Mwokozi Yesu ?
Damu yake ilimwangika pale kukulipia deni.

*Alikukufia musalabani, hivi umekombolewa ;*
*Mapendo yake ya mushangao,*
*Mapendo makubwa gani !*

2. Umesoma ya kwamba walimuvika taji ya mi-iba ?
Aliwaombea : « Uwasamehe, kwani hawafahamu. »

3. Umesoma ya kama aliokoa mwizi mwenye toba,
Aliyemusihi musalabani : « Bwana, unikumbuke » ?

4. Umesoma ya kwamba Mwokozi alilia, « Imekwisha » ?
Umesema : « Bwana, asante kwako uliyenikufia » ?

Cfr/ RS694 IH67 CH71

## Eb-3/4 HABARI NJEMA 97

1. Bwana Yesu alikuja kutafuta wapotevu ;
Kwa rehema yake Mungu tunapata kuokoka.

*Tunaimba kwa furaha, kwani tumekombolewa,*
*Sifa kubwa kwake Yesu, kwani alituokoa.*

2. Bwana Yesu alikuja kwa ajili yetu yote ;
Tunapata kuponyeshwa kwa mapigo yake kule.

3. Tulifungwa na Shetani, tulikuwa wafu kweli ;
Mukombozi alikuja, sasa tunafunguliwa.

4. Wala mali, wala kazi, haziwezi kuokoa ;
Yesu pekee anaweza kusamehe zambi zetu.

5. Wewe ndugu, usingoje, kuja sasa kwake Yesu ;
Atakuokoa leo, utaimba na furaha.

6. Siku moja Bwana Yesu atarudi duniani ;
Atatupeleka kwake kwa mungini wa mbinguni.

Cfr/ IH405

## Ab-6/8 HABARI NJEMA 98

1. Nimekombolewa kabisa, nitaitangaza daima ;
Nimekombolewa na Yesu, na mimi ni wake milele.

*Nimekombolewa na damu ya Yesu Mwokozi ;*

*Nimekombolewa, na mimi ni wake milele.*

2. Kwa Yesu furaha ni nyingi, kuliko furaha nyingine ;
Najua yeye ni karibu na tunabakia pamoja.

3. Ninamufikili saa zote, Mwokozi muzuri wa watu ;
Mapendo makubwa ni yake,
Kwa hivi naimba na nguvu.

4. Najua nitamutazama Mufalme Mupenzi mbinguni,
Anayenichunga na pendo, kunipa furaha moyoni.

Cfr/ IH276 CH149

**C-4/4** **HABARI NJEMA 99**

1. Siku nyingi nilifanya zambi,
Sikujua neno la Mwokozi,
Sikujua taabu yake kwami kwa Kalvari.

*Bwana Yesu alinirehemu,*
*Zambi zangu alizisamehe,*
*Nilipata kuwa huru kweli kwa Kalvari.*

2. Niliposikia Neno lake,
Moyo wangu ukalia sana,
Nikakiri zambi zangu zote kwa Kalvari.

3. Sasa Yesu ni Mufalme wangu,

Atanitawala kwa milele ;
Roho yangu inaimba sifa kwa Kalvari.

4. Ee mapendo gani ya Mwokozi !
Na rehema yake kubwa kwetu !
Tulipatanishwa naye Mungu kwa Kalvari.

Cfr/ IH172 CH207

**Eb-4/4** **HABARI NJEMA 100**

1. Pasha habari za Yesu, uziandike moyoni ;
Uni-imbie zaburi za kumusifu Mwokozi,
Sifa iliyotangazwa na malaika zamani :
« Mungu akuzwe mbinguni, iwe amani duniani. »

*Pasha habari za Yesu, uziandike moyoni*
*Uni-imbie zaburi za kumusifu Mwokozi.*

2. Pasha habari za Yesu, jinsi alivyoyashinda
Taabu, jaribu, na teso, umasikini na bezo ;
Zambi, hukumu ya Mungu akachukua mwenyewe ;
Kila wakati tayari kwa kusaidia wahitaji.

3. Pasha habari za Yesu za musalaba na kufa
Ona kaburi mwambani alipotoka Mwokozi.
Pendo la Yesu ni kubwa aliyekufa Golgota,
Akafufuka hakika, namushukuru siku zote.

Cfr/ RS456 IH113 CH162

## G-3/4 HABARI NJEMA 101

1. Ni ahadi ya Mungu kuleta wokovu
   Na wenye kuamini Mwokozi ni Yesu.

   *:: Haleluya ! Imekwisha, ninaamini kabisa*
   *Na nimeokoka kwa damu ya Yesu ::*

2. Hata njia ni yenye hatari na mbaya
   Ninajua Yesu Kristo atanichunga.

3. Ndugu zangu wapenzi ni wengi mbinguni,
   Wanachungwa na Yesu na wanamwimbia.

4. Hata saa tuimbe pamoja nao vile,
   Na kusifu Mwokozi, Mupenzi milele.

Cfr/ SSS841 RS274 IH433 CH187

## Eb-6/8 HABARI NJEMA 102

1. Munganga amekuja hapa, ndiye Bwana Yesu ;
   Anaponyesha roho zetu kwa ugonjwa wote.

   *Jina lake linapita kila Jina duniani ;*
   *Jina kubwa, Jina jema, Yesu, Bwana Yesu.*

2. Anasamehe zambi zetu kama tukitubu ;
Anatukaribisha kwake kwa rehema kubwa.

3. Wakati wa masikitiko, anatufariji ;
Akitukaribia sana, woga unatoka.

4. Watoto wanapenda sana Jina lake Yesu ;
Linawalinda kwa ubaya wakijaribiwa.

5. Katika vita na mabaya linatupa nguvu ;
Shetani analikimbia Jina lake Yesu.

6. Mbinguni kwa furaha kubwa tutaona Yesu,
Tutasahau taabu yote, tutamushukuru.

Cfr/ SSS89 RS291 CV60

**Eb-4/4** **HABARI NJEMA 103**

1. Siwezi mimi kufahamu sana
Neema yake Mungu kwangu ;
Zamani nilikuwa mukosaji, sasa amenisamehe.

*Ninajua Mwokozi wangu anayeweza kulinda sana*
*Uriti kwami mbinguni hata siku yake Bwana.*

2. Siwezi mimi kufahamu sana namna alivyonivuta ;
Niliamini Neno lake kweli, ninaona raha tele.

3. Siwezi mimi kufahamu kazi Roho anayoifanya,
Anayeweza kufundisha mutu kuamini Yesu Kristo.

4. Sijui mimi siku zangu tena kutembea duniani ;
Na labda nitaona taabu na mateso na huzuni nyingi.

5. Sijui mimi kama siku moja nitaona kufa huko ;
Ao kwa haraka nitabadilika Bwana atakapokuja.

Cfr/ SSS857 CV233 IH264 CH85

**D-6/8** **HABARI NJEMA 104**

1. Zamani muke mwenye ugonjwa katika makutano
Ali-igusa nguo ya Yesu naye aliponyeshwa.

*Na wewe vile amini, na utaokolewa ;*
*Uzima mupya utapata kwa Yesu Mukombozi.*

2. Ee alikuja na woga mwingi karibu naye Bwana ;
Alifahamu aliponyeshwa na nguvu yake kubwa.

3. Yesu alisamehe makosa ya mwanamuke yule,
Salama tamu ili-ingia rohoni mwake pale.

Cfr/ SSS55 RS140

**Ab-6/8** **HABARI NJEMA 105**

1. Pendo la mushangao hili kuniokoa,
Mutu mubaya, mwenye zambi, bila taraja ;
Giza lilifunga vile, Ee siku kubwa,
Nilipopata kuokoka. Pendo la Mungu !

*Pendo la Mungu liliniokoa,*
*Pendo la Mungu lilinisafisha ;*
*Pendo la Mungu lilitoa Yesu,*
*Pendo la Mungu, sifu Jina lake !*

2. Pendo liliongoza Yesu kwa musalaba
Hata kwa watu wa makosa, Ee pendo kubwa !
Vile kwa pendo ninaweza kuomba Mungu,
Nimeokoka, Haleluya ! Pendo la Mungu !

3. Pendo lilifungua mbingu kwa wenye zambi ;
Kule milele Mukombozi atatawala.
Toka kwa giza nilingia pa'li pa nuru ;
Yesu pekee alisaidia. ! Pendo la Mungu !

Cfr/ CH205

**Eb-9/4** **HABARI NJEMA 106**

1. Sisi ni huru toka torati,
Damu ya Kristo ni ukombozi ;
Tulipofungwa chini ya laana,

Kristo alitufanya huru.

*Huru kabisa, ndugu, sikia !*
*Huru kabisa, ndugu, amini !*
*Kwa neema Kristo musalabani*
*Alitufanya huru kweli.*

2. Sasa azabu haitakuwa
Kwa wenye kumwamini Mwokozi ;
Tuna wokovu mutimilifu,
Kwani tuna-amini Yesu.

3. Sisi ni sasa wana wa Mungu,
Kwa neema yake anatuchunga ;
Tumepokea kwake uzima
Na tumepita toka kufa.

Cfr/ CV88 RS186 IH112

**Eb-3/4** **HABARI NJEMA 107**

1. Sina akili nyingi kufahamu Neno lake Mungu,
Najua hili moja tu : Yesu ni Mwokozi wangu.

2. Najua alikufa kwa Kalvari kwa makosa yangu ;
Ninahitaji Yesu tu kuwa Mukombozi wangu.

3. Siwezi mimi vile kufahamu pendo lake kubwa.
Na linanishangaza tu, pendo la Mwokozi wangu.

4. Na sasa anaishi kwa pahali pa mbinguni juu ;
Yeye Mufalme wangu tu, ndiye Mukombozi wangu.

Cfr/ SSS849 RS395 IH154

**D-4/4** **HABARI NJEMA 108**

1. Zahabu na feza haziniokoi,
Na mali haiwezi kutoa makosa ;
Lakini kwa damu ya Yesu Mwokozi
Nimenunuliwa nipate uhuru.

*Nakombolewa pasipo mali,*
*Na kwa neema nimeokoka :*
*Ni bei gali, kwa damu yake*
*Alilipa deni yangu.*

2. Zahabu na feza hazina uwezo
Kwa kunipatia usafi rohoni ;
Mwokozi alinikomboa kwa damu,
Nipate wokovu, nitoke kwa zambi.

3. Zahabu na feza haziufungui
Mulango wa kukaribia Mwenyezi,
Lakini kwa damu nimeifikia
Ne-ema ya Mungu aliye Mukuu.

4. Zahabu na feza hazinifichi

Nyumbani mwa Mungu niliyemubisha ;
Lakini nimekombolewa kwa damu,
Kwa hivi nitachukuliwa mbinguni.

Cfr/ RS321 CH124

**C-4/4** **HABARI NJEMA 109**

1. Watu wa makosa wana zambi nyingi,
Zambi zinaleta kufa kwa milele ;
Watahukumiwa na Mwamuzi Mungu,
Kisha watapata taabu na mateso.

*Mwana wake Mungu anaita leo :*
*Kiri zambi zako zote mbele yake ;*
*Uamini sasa na kufuata Bwana.*
*Atakusamehe zambi zako zote.*

2. Mwenye kukata-a Bwana Yesu Kristo
Anamukata-a Mungu vilevile ;
Kwa milele moto utamutaabisha
Kwani anabisha ma-agizo yake.

3. Pa'li pa Shetani ni pabaya sana.
Moto unawaka pale kwa milele ;
Mungu atatupa Diabolo kule
Na wenye kubisha Neno lake Mungu.

4. Tutaona Yesu kule kwake mbingu,

Ni pahali pa furaha kubwa sana ;
Yesu Mukombozi, Bwana wa wabwana,
Anashinda kule akituombea.

Cfr/ SSS757 RS463 IH386

## D-4/4 HABARI NJEMA 110

1. Damu yako yenye baraka inayotuosha makosa,
Ilitoka musalabani, Bwana Yesu, ulipokufa.
Ee ninastahili hukumu, na siwezi mimi kujiosha ;
Unioshe katika damu, nipate usafi kabisa.

*Safi, safi kweli ! Safi, safi kweli !*
*Unioshe katika damu, nipate usafi kabisa*

2. Yesu ulivikwa mi-iba, kutundikwa ju-u ya muti,
Ulivumilia mateso, maumivu na majeraha ;
Damu yako ilimwangika, ni kisima nisafishwe nacho ;
Unioshe katika damu, nipate usafi kabisa.

3. Baba, kweli nina makosa, moyo wangu wa uzaifu,
Mimi mwenye zambi rohoni nitaona wapi Mwokozi ?
Yesu, kwako musalabani ninakuja kuamini sasa ;
Unioshe katika damu, nipate usafi kabisa.

4. Bwana, nimefika karibu, unilinde kwako milele,
Ufungue kamba ya zambi, na ujaze moyo wenyewe !
Na karibu na musalaba nibakie hata kufa kwangu ;

Unioshe katika damu, nipate usafi kabisa.

Cfr/ SSS113 CV120 IH97 CH39

**Eb-3/4** **HABARI NJEMA 111**

1. Naona sasa damu ya Kondo-o yake Mungu,
   Ilimwangika kwa Kalvari kwa ajili yangu.

   *Naona damu ya Mwokozi, nasafishwa ndani yake ;*
   *Kwa damu ninasifu Mungu, damu ya damani kweli.*

2. Kwa nia na zamiri safi ninakwenda mbingu,
   Sababu ninavikwa sasa haki yake Yesu.

3. Ajabu kubwa, nimeonja heri ya mbinguni !
   Kwa damu yake Yesu aliosha moyo wangu.

Cfr/ RS144 IH189

**Bb-4/4** **HABARI NJEMA 112**

1. Unakubali kuacha makosa ?
   Kwa damu ya Yesu kuna uwezo ;
   Na unataka kushinda Shetani
   Kwa damu ya Yesu Mwokozi ?

   *:: Kuna nguvu ya ajabu kubwa,*

*Ndiyo damu ya Mwokozi ::*

2. Unakubali kuvunja tamaa ?
Kwa damu ya Yesu kuna uwezo ;
Kuja upate usafi wa moyo
Kwa damu ya Yesu Mwokozi ?

3. Unakubali kuoshwa moyoni ?
Kwa damu ya Yesu kuna uwezo ;
Vitaondoshwa vipaku vya zambi
Kwa damu ya Yesu Mwokozi ?

4. Unakubali kutenda vizuri ?
Kwa damu ya Yesu kuna uwezo ;
Na unataka kufika mbinguni
Kwa damu ya Yesu Mwokozi ?

Cfr/ SSS145 CV135 IH425 CH209

## G-4/4 HABARI NJEMA 113

1. Nini itanisafisha ? damu ya Mwokozi Yesu ;
Kuondosha zambi zangu ? Damu ya Mwokozi Yesu.

*Ee damu ya Mwokozi ina uwezo wote*
*Kutusafisha sisi tunaoamini Yesu.*

2. Nini itaniokoa ? damu ya Mwokozi Yesu ;
Nini itanisamehe ? Damu ya Mwokozi Yesu.

3. Nini itanikomboa ? damu ya Mwokozi Yesu ;
Na kulipa deni yangu ? Damu ya Mwokozi Yesu.

4. Kuna njia moja pekee, damu ya Mwokozi Yesu,
Ninaweza kuamini damu ya Mwokozi Yesu.

5. Ile ni taraja yangu, damu ya Mwokozi Yesu ;
Na salama yangu yote, damu ya Mwokozi Yesu.

Cfr/ SSS874 RS99 CV109 CH203

**Eb-4/4** **HABARI NJEMA 114**

1. Kweli maji hayaweji kusafisha roho,
Hayawezi kuondosha zambi, hata moja.

*Damu ya Mwokozi Yesu ina nguvu nyingi*
*Kusafisha roho zetu toka zambi zote.*

2. Yesu alikuja kufa kwa ajili yetu,
Akamwanga damu yake kwa katuokoa.

3. Damu yake ni tayari kutuchunga safi,
Tupendeze Bwana yetu aliyetupenda.

4. Kila mara tunaanguka Yesu ni karibu
Kutusimamisha tena kwa uwezo wake.

5. Tuamini damu yake kutupa uwezo
Kwa kushinda majaribu ya mudanganyifu.

Cfr/ CV166

**C-4/4** **HABARI NJEMA 115**

1. Kisima chenye damu safi kutoka musalaba
Kina uwezo kuondosha vipaku vya makosa,
Vipaku vya makosa, vipaku vya makosa,
Kina uwezo kuondosha vipaku vya makosa.

2. Musalabani munyangani alimwamini Yesu,
Na alipata usamehe, nitaupata vile ;
Nitaupata vile, nitaupata vile,
Na alipata usamehe, nitaupata vile.

3. Mwokozi wangu, damu yako daima ina nguvu
Ya kuokoa wenye zambi wa makabila yote ;
Wa makabila yote, wa makabila yote,
Ya kuokoa wenye zambi wa makabila yote.

4. Kisima kile cha ajabu ni tumaini langu ;
Ninakusifu wewe sasa na hata kufa kwangu ;
Na hata kufa kwangu, na hata kufa kwangu,
Ninakusifu wewe sasa na hata kufa kwangu.

Cfr/ SSS129 RS137 IH115

**Eb-4/4** **HABARI NJEMA 116**

1. Hata ninalia na machozi kama muto,
   Haitaondosha woga, haitasafisha zambi,
   Ninalia bule.

   *Yesu alinikufia, aliteshwa kwa Kalvari,*
   *Yesu ananingojea, ataniokoa.*

2. Hata ninafanya kazi nyingi njema sana,
   Sitapata roho mpya, vile sitasamehewa,
   Kazi yangu bule.

3. Kama nikingoja bila kuamini Yesu,
   Bila kumukaribia ; nitakufa kwa milele,
   Ninangoja bule.

4. Sasa ninaamini Yesu alinikufia,
   Alifanya kazi yote, Bwana Yesu peke yake
   Ataniokoa.

Cfr/ SSS337 CH193

**F-4/4** **HABARI NJEMA 117**

1. Mimi mwenye makosa nilikombolewa,
   Mwokozi alipojitoa ;
   Zambi zangu na zako alizichukua,

Kwa damu aliniokoa.

*Zambi zangu zilimutundika Mwokozi*
*Alipojitoa Kalvari ;*
*Alizarauliwa na kukataliwa*
*Atupatanishe na Mungu.*

2. Yesu mwenye upole na mwenye mapendo
Ananitakasa rohoni ;
Nimepata uhuru kwa Yesu Mwokozi,
Alikufa musalabani.

3. Namwambata Mwokozi, sitaki kumwacha,
Kwa kuwa alinikufia ;
Nakusifu, Ee Yesu, unayenipenda,
Daima nakushangilia.

Cfr/ RS737 CH174

**Bb-3/4** **HABARI NJEMA 118**

1. Mwamba uliopasuka, ndani yako nijifiche ;
Damu iliyomwangika toka mbavu zako, Bwana.
Iwe dawa kuponyesha roho yangu toka zambi.

2. Kazi za mikono yangu haziwezi kukomboa ;
Hata ningelia sana na kutenda kazi nyingi,
Singeweza kuokoka, wewe pekee ni Mwokozi.

3. Ndani yangu sinakitu, ninashika musalaba ;
Mimi bule, univike ; sina nguvu, usaidie ;
Nimuchafu, unioshe ; nisipate kupotea.

4. Kwa maisha yangu yote hata nitakata roho,
Hata siku ya kuitwa mbele ya Mufalme wangu.
Mwamba uliopasuka, nijifiche ndani yako.

Cfr/ SSS237 RS164 IH315 CH148

## G-3/4 HABARI NJEMA 119

1. Tumepata neno zuri : Yesu aliniokoa !
Tulipashe kwa dunia : Yesu aliniokoa !
Linapaswa kusikiwa na wakubwa na watoto,
Ni habari za furaha : Yesu aliniokoa !

2. Tuna hamu ya kuimba : Yesu aliniokoa !
Ni uzima kwa waovu : Yesu aliniokoa !
Kweli alitufungua, alivunja munyororo,
Sisi mali yake sasa : Yesu aliniokoa !

3. Neno kubwa la makubwa : Yesu aliniokoa !
Linashinda na zaidi : Yesu aliniokoa !
Sema niki-ishi hai, hata nitakapokufa,
Ninataka kusikia : Yesu aliniokoa !

4. Tutangaze neno hili : Yesu aliniokoa !
Kila mutu asikie : Yesu aliniokoa !

Inchi zote zifurahi, watu wote wa-amini,
Na waimbe na kusifu : Yesu aliniokoa !

Cfr/ SSS1079 RS200 IH469 CH195

## Eb-4/4 HABARI NJEMA 120

1. Mungu ni pahali pote, hutamukimbia yeye ;
Anakutazama sana, naye hatalala kamwe.

*Giza, nuru, sikuzote Mungu anakutazama ;*
*Hata unafanya nini, Mungu anaona yote.*

2. Neno gani unasema, Mungu analisikia ;
Hata mafikili yote anayatambua wazi.

3. Yesu atakapokuja, atawahukumu wote
Kwa kadiri ya matendo yanayoandikwa kwake.

4. Unajua deni yako ? utalipa kitu gani ?
Uamini Bwana Yesu, naye atakusamehe.

Cfr/ Tabernacle 4-15

## Bb-4/4 HABARI NJEMA 121

1. Piga makengele ya furaha leo
Kwa sababu mutu ametubu !

Mwana mupotevu amerudi sasa,
Baba amemusamehe yote.

*Nyimbo za furaha za mbinguni,*
*Nyimbo za furaha za waamini !*
*Tunasifu Mungu kwa sababu sasa*
*Mutu huyu anaamini Yesu.*

2. Piga makengele, ni furaha nyingi,
Mukosaji amefunguliwa !
Yesu alivunja minyororo yake,
Alimupa roho ya kimwana.

3. Piga makengele, hizi ni habari
Za kupasha mbali na karibu !
Mutu amepata kuwa mutu mupya,
Zambi zake zimeondolewa !

Cfr/ SSS650 RS285 IH300

**Ab-4/4** **KUITA WATU 122**

1. Umekuja kwake Yesu kusafishwa ?
Umeoshwa kwa damu ya Kristo ?
Unategemea neema yake sasa ?
Umeoshwa kwa damu ya Kristo ?

*Umeoshwa, Umeoshwa,*
*Umeoshwa kwa damu ya Kristo ?*

*Roho yako imepata kuwa safi ?*
*Umeoshwa kwa damu ya Kristo ?*

2. Sikuzote unafuata njia yake ?
Umeoshwa kwa damu ya Kristo ?
Umepata raha na salama kwake ?
Umeoshwa kwa damu ya Kristo ?

3. Wewe ni tayari kwa kuona Yesu ?
Umeoshwa kwa damu ya Kristo ?
Naye atakupeleka kwake mbingu ?
Umeoshwa kwa damu ya Kristo ?

4. Ndugu yangu, ninaku-uliza sasa :
Umeoshwa kwa damu ya Kristo ?
Usikawe tena, kuja kuamini,
Utaoshwa kwa damu ya Kristo ?

Cfr/ SSS378 RS171 IH95 CH68

**G-4/4** **KUITA WATU 123**

1. Utazame Mwokozi aliyekufa kwawe
Ili wewe upate uzima ;
Utazame kwa pendo atakusa-idia,
Usidumu zambini daima.

*Ona, ona Yesu !*
*Utazame Mwokozi aliyekufa kwawe*

*Ili wewe upate uzima.*

2. Bwana Yesu alisulibishwa kwa Kalvari
Ili sisi tupate wokovu ;
Na alitukomboa kwa damu yake safi,
Kwake yeye tupate uzima.

3. Ee rafiki, Mwokozi anakuita leo,
Anataka ufike upesi ;
Unakawa kwa nini, ufike bila woga,
Uondoke katika hatari.

4. Fika sasa, pokea uzima wa milele,
Bwana Yesu alituletea ;
Na kuishi mbinguni ni tumaini letu,
Umwamini na hutapotea.

Cfr/ SSS123 RS169 CV82 CH251

## **Eb-4/4** **KUITA WATU 124**

1. Kuja kwa Yesu na usikawe,
Anaonyesha njia ya mbingu ;
Umusikie, anakusihi : « Mutu wa zambi, kuja ! »

*Kuja sasa kwake Bwana Yesu,*
*Atakuokoa toka zambi ;*
*Amini Yesu moyoni mwako, upate usamehe.*

2. Kuja, mutoto, anakuita, anakupenda, atakuchunga ;
Umuchague kwa Bwana yako, wewe mutoto, kuja.

3. Atapokea watu wo wote, sasa anakuongojea wewe ;
Tubu upate kusamehewa, kuja na zambi zako.

4. Sasa ni siku kuokolewa, kuja upesi kwa musalaba ;
Mwenye masikitiko na zambi, kuja kwa Yesu sasa.

Cfr/ SSS1165 RS123 CH438

**Ab-6/8** **KUITA WATU 125**

1. Yesu Mwokozi anaita watu, mimi na wewe na wote ;
Anakungoja kukukaribisha, wewe uliye zambini.

*Urudi, urudi, sasa urudi kwa Yesu !*
*Anakuita na anakungoja ; leo urudi kwa Yesu !*

2. Unakata-a Mwokozi kwa nini ? anakungoja ufike ;
Kuna nafasi karibu na Yesu, njia ni wazi kwa wote.

3. Kumbuka saa zinapita upesi, hazitarudi kabisa !
Kuja kwa Yesu upate amani, leo ungali muzima.

4. Ona mapendo makubwa ya Yesu,
Yanaenea kwa wote ;
Na kwa ne-ema anatukumbuka,
Wewe na mimi na wote.

Cfr/ RS95 IH201 CH243

## Eb-6/4 KUITA WATU 126

1. Na hali yangu ninakuja pasipo neno ila moja :
   Ulimimia damu yako, ninakuja kwako, Bwana.

2. Na hali yangu sitangoja kujisafisha kosa moja ;
   Kwa damu utaniokoa, ninakuja kwako, Bwana.

3. Na hali yangu kwa matata, mashaka, woga na azabu,
   Nipate raha kwako, Mungu, ninakuja kwako, Bwana.

4. Na hali yangu masikini, kipofu, bule, na zaifu,
   Nipate mali ya milele, ninakuja kwako, Bwana.

5. Na hali yangu ninaamini ahadi zako zote kweli ;
   Nipate usamehe wako, ninakuja kwako, Bwana.

Cfr/ SSS473 CV124 IH198 CH226

## C-4/4 KUITA WATU 127

1. Usikie Bwana Yesu anayekuita leo ;
   Aliteswa, alikufa kwa ajili yako wewe.

*Usikie Bwana Yesu, anapiga hodi kwako ;*
*Umufungulie moyo, umukaribishe sasa.*

2. Sikuzote ulicheza, kupendeza mwili wako ;
Ulimusahau Yesu aliyekukufilia.

3. Unasema : « nitakuja kusikia Neno lake » ;
Ee rafiki, ukumbuke unaweza kufa leo.

4. Yesu anaita sasa kwa ne-ema na mapendo ;
Leo siku ya wokovu, umufungulie moyo.

Cfr/ SSS443 CV54 IH420 CH239

**D-4/4** **KUITA WATU 128**

1. Mwenye kusikia, kuja kwake Yesu,
Yeye ni Mwokozi wa wenye makosa ;
Acha zambi zako, umwamini yeye.
Kila mwenye zambi aje.

*Kila mwenye zambi aje kwa Mwokozi,*
*Mutangaze neno hili kila pa'li ;*
*Baba ya mapendo anaita leo :*
*Kila mwenye zambi aje.*

2. Mwenye kusikia, kuja, usikawe,
Leo lango la wokovu liko wazi ;
Yesu ndiye njia, kweli, na uzima,

Kila mwenye zambi aje.

3. Mwenye kusikia na kufika kwake,
Atamupokea, ni ahadi yake ;
Atachunga vile, hata kwa milele,
Kila mwenye zambi aje.

Cfr/ SSS389 CV111 IH206 CH204

## G-6/8 KUITA WATU 129

1. « Hakose kesho nita-amini,
Nitapokea Yesu Mwokozi. »
Mungu anakuita, usikawie tena,
Leo ni siku nzuri kuokolewa.

2. Hakose kesho saa itapita ;
Kwa nini unazarau Bwana ?
Kwa neema yake kubwa Mungu atapokea ;
Saa haijapita bado, kuja kwa Yesu.

3. Hakose kesho saa ya hukumu
Itakupata mbele ya Mungu ;
Umusikie sasa, anakupenda sana,
Fikili neno hili, usipote-e !

Cfr/ SSS452 CV89 IH187 CH211

## G-3/4 KUITA WATU 130

1. Usikie Yesu Kristo, yeye anakuita,
   Sikia na kujibu, sasa kuja kwa Bwana.

2. Anaweza kuokoa mwenye kumusadiki,
   Na atakuokoa kama ukimwamini.

3. Anapenda kusamehe watu wanaotubu,
   Na atakusamehe – kuja sasa kwa Yesu.

4. Ukimbie sasa kwake, na atakupokea,
   Kimbia kwa Mwokozi na atakupokea.

5. Omba Yesu, omba Yesu, na atakusikia,
   Uombe Yesu sasa, na atakusikia.

6. Anapenda watu wote, Yesu anakupenda,
   Milele na milele Yesu atakupenda.

7. Haleluya, Haleluya, Haleluya, Amina !
   Tuimbe Haleluya, Haleluya, Amina !

Cfr/ RS105

## G-4/4 KUITA WATU 131

1. Ee kuja, mutu wa makosa, kuja kwa rehema ;
   Mwokozi atakupokea kama ukikuja.

*Umwamini, umwamini, umwamini Yesu,*
*Naye atakuokoa, umwamini Yesu.*

2. Mwokozi alimwanga damu yake kwa Kalvari,
Na damu ile inaweza kusafisha safi.

3. Ee Yesu tu ni njia kuingia kule mbingu ;
Amini sasa kwa kupata usamehe kwake.

4. Ungana nasi watu wake, njia iko wazi ;
Na tutakuwa kwa milele na furaha nyingi.

Cfr/ SSS392 RS196 IH188 CH217

**Ab-6/8** **KUITA WATU 132**

1. Hatua moja inakutenga na Mwokozi ;
Unangojea nini ? Ufike kwake leo !

*Hatua moja, hatua moja ; kuja, anangoja ;*
*Kuja kutubu zambi, atasamehe zote !*
*Usikatae tena wokovu wake Mungu !*

2. Hatua moja mbele, anakungoja sasa ;
Amini Neno lake, na utasamehewa.

3. Hatua moja mbele, uzima utaona ;
Siku si nyingi huko, unangojea nini ?

4. Hatua moja mbele, kwa nini unakawa ?
Omba : Ee Bwana Yesu, unipoke-e sasa !

Cfr/ SSS448 RS273 IH160 CH236

**f-4/4** **KUITA WATU 133**

1. Utafurahi kuwa na uhuru ? umutazame Yesu ;
Kukuokoa alikukufia, umutazame Yesu.

*Umutazame Yesu, umutazame Yesu,*
*Yesu pekee atakuokoa, kuja na kumwamini.*

2. Kama Shetani akikujaribu, umutazame Yesu ;
Nguvu kushinda atakupatia ; umutazame Yesu.

3. Njia ni ndefu, unachoka sana ? umutazame Yesu ;
Atafariji na mapendo yake ; umutazame Yesu.

4. Usiogope siku za huzuni ; umutazame Yesu ;
Hata kwa siku za furaha nyingi ; umutazame Yesu.

Cfr/ IH73 CH89

**G-4/4** **KUITA WATU 134**

1. Kama ukitaka kuwa mutu wake Yesu,
Kama ukitaka kumufuata yeye,

Kama ukitaka asaidie sikuzote,
Umufungulie moyo.

*Ataondoa zambi zako zote,*
*Na utaipokea nguvu yake ;*
*Ukiokoka utaona kwamba*
*Ni vema kumufuata Yesu kweli.*

2. Kama ukitaka kuwa mutu mwenye heri,
Na kushinda zambi kwa uwezo wake,
Kama ukitaka utulivu na faraja,
Umufungulie moyo.

3. Kama ukitaka kumutumikia Yesu
Na kufuata njia yake duniani,
Kama ukitaka kuingia kule mbingu,
Umufungulie moyo.

Cfr/ RS574 IH346

**F-3/4** **KUITA WATU 135**

1. Mateso yanakusumbusha, na unatembea kwa giza ?
Geuka, tazama Mwokozi, uzima na nuru pokea.

*Utazame Mwokozi, fikili uzuri wa Bwana ;*
*Mambo ya dunia yatapunguka*
*Mbele ya utukufu wa Yesu.*

2. Mwokozi alitukufilia, tuishi pamoja na yeye ;

Na tusijitoe kwa zambi, kwa Yesu tushinde kabisa.

3. Ahadi za Mungu ni kweli ; amini na utaokolea ;
Halafu uende po pote, hubiri habari za Bwana.

Cfr/ IH379

**G-4/4** **KUITA WATU 136**

1. Nina Mwokozi anayeniombea,
Rafiki kuliko wengine wo wote ;
Na sasa mbinguni ananitunza sana,
Laiti upate Mwokozi mwenyewe !

*Ninakuombea, ninakuombea,*
*Ninakuombea, upate kuamini !*

2. Nina taraja kutoka Baba wangu,
Ya kama atanipokea mbinguni ;
Na sasa ninamungojea kuni-ita,
Laiti upate taraja yenyewe !

3. Nina mavazi yanayoningojea,
Mavazi meupe ndiyo utukufu ;
Na nitayapata mbinguni kwake Mungu,
Laiti upate mavazi yenyewe !

4. Nina salama inayopita yote,
Si kama dunia inayoitoa ;

Inatoka Yesu kwa pendo lake kubwa,
Laiti upate salama yenyewe !

Cfr/ SSS350 CV100 IH195 CH220

## Bb-6/8 MWENENDO WA WAAMINI 137

1. Tamu sana ni maneno ya habari njema,
Jana, leo, na milele Yesu yuko sawa ;
Hata sasa anapenda watu wa makosa,
Kufariji wenye taabu, sifu Jina lake !

*Jana, leo, na milele Yesu yuko sawa,*
*Vyote vinapogeuka, Yesu yuko sawa.*
*Sifu Jina lake ! Sifu Jina lake !*
*Vyote vinapogeuka, Yesu yuko sawa.*

2. Mwenye kusamehe Petro atatusamehe ;
Atatoa shaka zote kama kwa Tomasi ;
Mwanafunzi alilala kifuani mwake ;
Anaita watu sasa kupumzika kwake.

3. Alinyamazisha maji kule kwa bahari,
Hivyo anaweza kuondoa woga vile ;
Akaomba na huzuni kwa Getesemane ;
Anaweza kufahamu taabu zetu zote

4. Kama alivyotembea na wafuasi wake,
Na kuwafariji kwa safari ya Emau,

Vivyo hivyo anapenda kutembea nasi
Yeye Mufariji mwema leo na milele

Cfr/ RS385 IH441 CH329

## D-6/8 MWENENDO WA WAAMINI 138

1. Heri kabisa, Yesu ni wangu !
Ni Muchungaji, na mimi ni wake ;
Nimezaliwa mara ya pili,
Ninasafishwa kwa damu yake.

*::Yesu ni wimbo wa roho yangu,*
*Nitakusifu hata milele ::*

2. Kule mbinguni kuna furaha
Juu ya mwenye kutubu makosa ;
Nilisikia Neno la Mungu,
Nilijitoa kwa Bwana Yesu.

3. Ninashukuru Yesu Mwokozi,
Na roho yangu inashangilia ;
Mimi si kitu mbele ya Mungu,
Kwa neema yake ananipenda.

4. Ninastarehe sasa kwa Yesu,
Nina salama kutoka kwa Mungu
Ninangojea Yesu afike
Kunipeleka kwake mbinguni.

Cfr/ SSS873 RS417 IH311 CH41

## Ab-4/4 MWENENDO WA WAAMINI 139

1. Moyo wangu una wimbo leo, Yesu ananiambia :
« Siku zote nitakuongoza, Ee usiogope tena. »

*Yesu, Yesu, Yesu, Jina tamu sana ;*
*Linajaza roho na furaha na salama.*

*2.* Mbele nilitaka kuharibu roho yangu na makosa ;
Yesu aliingia kuokoa, sasa nimesamehewa.

*3.* Hata ana'ngoza kwa mateso, taabu ya kuzidi sana,
Yesu ni Mushinda sikuzote, naye anajua njia.

*4.* Yesu ni karibu kurudia kutukaribisha kwake,
Kutawala naye kwa milele
Kwa mungini wake mbingu.

Cfr/ CH183 IH309

## F-4/4 MWENENDO WA WAAMINI 140

1. Ee nitakimbia kwa Mwamba wa nguvu
Kutoka huzuni, mateso, na taabu ;
Nachoka na zambi, nataka tu Mungu ;
Ee nitafichama kwa Mwamba wa nguvu.

*Nitafichama kwako, Mwokozi ;*
*Ee Mwamba wa nguvu, unifiche kwako.*

2. Kwa sa aye salama na vile kwa taabu,
Na saa majaribu yanaponitesa,
Nina kimbilio katika zoruba,
Ee nitafichama kwa Mwamba wa nguvu.

3. Adui ya roho anapozunguka,
Naweza kusema habari kwa Yesu,
Atanisikia na kunifariji,
Ee nitafichama kwa Mwamba wa nguvu.

Cfr/ SSS519 IH421 CH345

**Bb-4/4** **MWENENDO WA WAAMINI 141**

1. Usimame kwa ahadi zake Kristo,
Sasa na milele umusifu sana ;
Leta utukufu wote kwake Mungu,
Usimame kwa ahadi zake.

*Usimame, leo usimame kwa ahadi zake ;*
*Usimame, simama kwa ahadi zake Mungu*

2. Usimame kwa ahadi za milele,
Hata majaribu yanatesa sana ;
Utapata nguvu kwa Maneno yake,

Usimame kwa ahadi zake.

3. Usimame kwa ahadi zake Bwana,
Kwani unafungwa kwa milele kwake,
Roho atakushindisha sikuzote,
Usimame kwa ahadi zake.

4. Usimame kwa ahadi, hutaanguka,
Ukisikiza Roho aki-ita :
Upumzike ndani ya Mwokozi wako,
Usimame kwa ahadi zake.

Cfr/ SSS877 RS13 IH328 CH28

**Bb-6/8** **MWENENDO WA WAAMINI 142**

1. Usiogope mateso yako, Mungu anakulinda ;
Bali tazama mapenzi yake, Mungu anakulinda.

*Mungu anakulinda siku kwa siku njiani mwake ;*
*Anakulinda daima, Mungu anakulinda.*

2. Una muzigo muzito sana ? Mungu anakulinda ;
Na kwa hatari ya njia yako, Mungu anakulinda.

3. Anakumbuka hitaji lako, Mungu anakulinda
Utashiriki uzuri wake, Mungu anakulinda.

4. Katika njia ya taabu nyingi, Mungu anakulinda ;

Hata ukifazaika sana, Mungu anakulinda.

Cfr/ IH428 CH262

## D-3/4 MWENENDO WA WAAMINI 143

1. Ee Yehova, Mungu wangu, uni'ngoze duniani ;
Mimi ni zaifu sana, una nguvu ya kutosha.
Kweli wewe ni mukate wa uzima,
Nitashiba, Yesu, kwako tu daima.

2. Kama ulivyo-ongoza watu wako wa zamani,
Acha nguzo ndiyo moto kuniangazia njia.
Mushindaji, uwe ngabo yangu nguvu ;
Nisishindwe na adui zangu, Mungu.

3. Nikifika kwa kivuko cha kupita kule kwako,
Uondoshe woga wote, nifikishwe kwa salama.
Nitatoa sifa nyingi kwako, Mungu ;
Nitaimba nyimbo za kukushukuru.

Cfr/ CV203 IH27

## Db-6/8 MWENENDO WA WAAMINI 144

1. Huzuni yangu ni kitu kweli
Machoni mwa Bwana Yesu ?
Saa ya masumbuko na
Majaribu yeye ananihurumia ?

*Kabisa ! Anaona yote na ananihurumia ;*
*Taabu yangu yote nilete kwake,*
*Hataniacha kamwe.*

2. Mwokozi yuko karibu kweli ninapo-ogopa sana ?
Na nikitembea katika giza,
Bwana ni karibu kuchunga ?

3. Wakati ninapopima sana nishinde saa ya jaribu,
Na nina-anguka, huzuni kubwa !
Atapenda kunisamehe ?

4. Wakati wa kufa kwa wapenzi,
Kuachwa na ndugu zangu,
Na upekee ukinishika nguvu,
Bwana atakuwa karibu ?

Cfr/ RS401 IH321

## Ab-4/4 MWENENDO WA WAAMINI 145

1. Jina lake Yesu Kristo tunapenda kusikia ;
Ni furaha na taraja saa tunapolikumbuka.

*Jina kubwa, Jina zuri, ni taraja ya dunia ;*
*Jina kubwa, Jina zuri, ni furaha ya mbinguni.*

2. Jina lake Yesu Kristo ni mulinzi kama ngabo,

Vile kimbilio letu, tukijaribiwa sana.

3. Jina lake Yesu Kristo, ni furaha yetu kubwa,
Saa tunapoimba sifa kwa Mupenzi wetu Yesu.

4. Tutaona Yesu Kristo, tutaanguka mbele yake,
Kwa sababu yeye Bwana na Mufalme wa wafalme.

Cfr/ SSS91 RS465 CV37 CH367

## G-3/4 MWENENDO WA WAAMINI 146

1. Yesu ni Rafiki yangu, anyenipenda sana ;
Sawasawa sikuzote, jana, leo, na milele.

*Haleluya, Yesu Kristo ni Mwokozi na Rafiki,*
*Muchungaji na Mufariji, Mwaminifu kwa milele.*

2. Yesu ni Mushinda wangu, anayenificha kwake,
Nikijaribiwa sana, yeye ni uwezo wangu.

3. Yesu Mufariji wangu katikati ya huzuni,
Saa ninapolia kwake, ananisikia mbio.

4. Yesu Mwokozi wangu,
Muchungaji wangu mwema ;
Ananionyesha njia, na sitapotea kamwe.

5. Yesu, ninapata kwako yote ninayohitaji ;

Kwani ulininunua, mini wako, wewe wangu.

Cfr/ HW62 Tabernacle 4-93

## Ab-3/4 MWENENDO WA WAAMINI 147

1. Baba wangu Mufalme, ndiye Mungu Mwenyezi,
Kweli anannipenda kabisa ;
Ana nyumba tayari kwami kule mbinguni,
Mali yake nitaishiriki.

*Baba wangu Mufalme ananipenda sana,*
*Naye ananilinda daima ;*
*Kwa wakati mwingine Yesu atani-ita*
*Kwa kuka-a nyumbani na yeye*.

2. Baba wangu Mufalme ni mwenye neema nyingi,
Ananihurumia hakika ;
Kwa maneno yo yote na pahali po pote
Ninaweza kumutegemea.

3. Baba wangu Mufalme ananiahidia
Kwamba atani-ita mbinguni ;
Pale nitatazama uso wake milele,
Nami nitasahau huzuni.

Cfr/ IH274

## G-9/8 MWENENDO WA WAAMINI 148

1. Pahali pote ninapokwenda,
   Ama kwa jua, ama kwa giza,
   Yesu Mwokozi aliahidi hatanipungukia daima.

*Nuru ya mbingu, nuru ya mbingu,*
*Ninatembea sasa kwa nuru ;*
*Haleluya ! Ninamusifu na shangwe kubwa,*
*Yesu ni wangu.*

2. *Wakati taabu inapokuja, Yesu hawezi kunisahau ;*
   *Aliahidi neno la kweli, atanichunga hata milele.*

3. Ninamusifu kwa nuru yake inayoniongoza kwa njia ;
   Nikitembea kando ya Yesu, sitapotea hata kidogo.

4. Katika njia kwenda mbinguni
   Niendele-e ndani ya nuru,
   Ninamwimbia nyimbo za sifa
   Kumushukuru kwa pendo lake.

Cfr/ IH291

## G-4/4 MWENENDO WA WAAMINI 149

1. Hakuna rafiki kama Yesu, Yesu tu, Yesu tu !
   Wapi mwingine kutuokoa ? Yesu tu, Yesu tu !

*Anajua mateso yetu, anapenda kutusaidia ;*
*Hakuna rafiki kama Yesu, Yesu tu, Yesu tu !*

2. Yeye pekee ni mutakatifu, Yesu tu, Yesu tu !
Na vile yeye munyenyekevu, Yesu tu, Yesu tu !

3. Nani karibu pahali pote ? Yesu tu, Yesu tu !
Nani anayetupenda wote ? Yesu tu, Yesu tu !

4. Alijitoa kwa zambi zetu, Yesu tu, Yesu tu !
Na tutakuwa naye mbinguni, Yesu tu, Yesu tu !

Cfr/ SSS904 RS110 IH435 CH182

**Bb-4/4** **MWENENDO WA WAAMINI 150**

1. Muchungaji Yesu, mwenye pendo kubwa,
Sisi wa-amini ni kondo-o zake ;
Tukihuzunika, Yesu anajua,
Anakaribia kwa kutusaidia.

2. Na Shetani hapa anatutafuta,
Sawasawa simba anatungojea ;
Tukumbuke Yesu ndiye Musaidia,
Kama aki-ita tutamusikia.

3. Tutabarikiwa mioyoni mwetu,
Kama tukifuata nyuma yake Bwana ;
Hatutaogopa tukimitazama

Akikwenda mbele ya kondo-o zake.

4. Muchungaji mwema, Yesu Mukombozi,
Alituokoa sisi watu bule ;
Damu yake safi alitumwangia,
Kutupatanisha naye Mungu Baba.

Cfr/ SSS1153 RS667 CH455

## Bb-6/8 MWENENDO WA WAAMINI 151

1. Kwami muchungaji ni Bwana Yesu,
Sitapungukiwa kitu ;
Kwa maana ananitembeza katika lisho bichi.

*Ee, nira yake laini kabisa, ananifunga na mapendo,*
*Kuniongoza katika njia, muchana na usiku.*

2. Na anarudisha nafsi hakika, ananiongoza vile
Katika njia yenye haki kwa Jina lake safi.

3. Hata nikipita kati ya bonde la kufa na giza lake,
Sitaogopa neno baya kwa maana wewe yuko.

Cfr/ RS467 CH313

## G-6/8 MWENENDO WA WAAMINI 152

1. Niwe karibu nawe, Ee Mungu wangu,
Hata katika taabu niwe karibu ;
Huu wimbo wangu, Bwana : Niwe karibu nawe,
Niwe karibu nawe, Ee Mungu wangu !

2. Ninasafiri hapa, sitakawia ;
Giza ni duniani, raha haiko ;
Hata ni hivi, Bwana, niwe karibu nawe,
Niwe karibu nawe, Ee Mungu wangu !

3. Hata mateso mengi yananipata,
Nitakumbuka hili, unarehema,
Na yatanikokota niwe karibu nawe,
Niwe karibu nawe, Ee Mungu wangu !

4. Saa nitakapokwenda kwako mbinguni,
Nitasahau taabu ya duniani ;
Ungali wimbo wangu niwe karibu nawe,
Niwe karibu nawe, Ee Mungu wangu !

Cfr/ SSS581 RS569 IH148

## G-4/4 MWENENDO WA WAAMINI 153

1. Najua Rafiki mwema, anatunza sana kila siku,
Anaweza kuponyesha ku-umia kwa mutima ;
Jina lake ni Yesu Kristo.

*Najua Rafiki mwema, naye anaja-a neema,*

*Nikiomba na kulia yeye ananisikia,*
*Ndiye Yesu, na si mwingine.*

2. Nimepata Rafiki mwema kufariji na kunipa raha,
Namutegemea yeye, sina woga wa adui ;
Na Rafiki ni Yesu Kristo.

3. Nikifika mutoni pale, unaitwa « kufa » na « kaburi »,
Sitafazaika kamwe, Yesu atakuwa nami ;
Ni Rafiki mukubwa sana.

4. Pwani nzuri ya kule ju-u,
Nitafika kwa ne-ema kubwa ;
Nitaimba na kinubi, nitasifu Yesu sana
Kwa mapendo na urafiki.

Cfr/ SSS1191 RS88 CV228

## F-3/4 MWENENDO WA WAAMINI 154

1. Ninataka Bwana Yesu awe nami sikuzote ;
Pendo lake litakuwa sawa miaka yote.

*Ee ukubwa wa mapendo yake Yesu, Bwana wangu ;*
*Ameniokoa kweli, atanipeleka kwake.*

2. Ninataka Bwana Yesu kwa wakati wa mateso ;
Anajua kufariji na kufuraisha moyo.

3. Ninataka Bwana Yesu kumutegemea sana,
Kuongozwa naye vile kwa safari yangu hapa.

4. Ninataka Bwana Yesu, kumupenda, kumufuata,
Hata nitakapo-ona uso wake kule mbingu.

Cfr/ RS369 IH344 CH160

**G-4/4** **MWENENDO WA WAAMINI 155**

1. Nani anayeninyanyua ? ni Yesu Kristo ;
Na anayenipigania ? Ni Yesu Kristo.
O Yesu ninakuamini, wewe tu utanishibisha,
Kwami silala ya kushinda ni Yesu Kristo.

2. Mwenye kunifikisha mbingu ni Yesu Kristo ;
Mwenye kunipa shangwe kubwa ni Yesu Kristo.
Na hata katika mateso na masumbuko, majaribu,
Kwami taraja na furaha ni Yesu Kristo.

3. Nani aliyeniokoa ? Ni Yesu Kristo ;
Nani anayefa-a kwangu ? Ni Yesu Kristo.
Bado kidogo nitakwenda kule
Kwa nyumba yake Baba.
Na nitaishi kwa milele na Yesu Kristo

Cfr/ CV195

## G-4/4 MWENENDO WA WAAMINI 156

1.Musingi wa nguvu ni Yesu Mwokozi,
Tuweke imani kwa neno la Mungu ;
Alituahidi kutupa wokovu,
::Tuliokimbia karibu na Bwana ::

2.« Usiwe na woga, usifazaike,
Nitakusaidia kwa saa ya mateso,
Kukusimamisha na kukupa nguvu ;
::Mukono wa neema utakushindisha ::

3.« Katika mateso na saa ya jaribu,,
Ne-ema ya Mungu inafa-a kwawe ;
Ukali wa moto hautaku-uma,
:: Nataka kutoa uchafu wa roho ::

4.« Mwenye kupumzika na kuniamini,
Siwezi, siwezi kumwacha daima ;
Na hata Shetani atamujaribu,
:: Siwezi, siwezi kumwacha daima »

Cfr/ SSS526 IH326 CH14

## Ab-4/4 MWENENDO WA WAAMINI 157

1.Nina ushirika na furaha kubwa,
Nikitegemea Yesu Bwana ;
Ninapata heri na salama vile,

Nikitegemea Yesu Bwana.

*Raha, raha, raha kwa Yesu na salama ;*
*Raha, raha, nikitegemea Yesu Bwana.*

2. Raha ya ajabu ni rohoni mwangu,
Nikitegemea Yesu Bwana ;
Nuru inangaza njia ya maisha,
Nikitegemea Yesu Bwana

3. Woga na huzuni zinatoka kwangu,
Nikitegemea Yesu Bwana ;
Ninafarijiwa sikuzote naye,
Nikitegemea Yesu Bwana.

Cfr/ RS377 IH323 CH361

## Ab-6/8 MWENENDO WA WAAMINI 158

1. Usiache zambi kushinda rohoni,
Yesu anataka kukupa uwezo
Kushinda Shetani na hila ya zambi ;
Imani kwa Yesu itakushindisha.

*Omba Yesu kwa nguvu ya kushinda Shetani ;*
*Anapenda kuchunga na atakushindisha..*

2. Acha urafiki na watu wabaya,
Na usitukane Jina lake Mungu ;

Uwe na imani, na neema na kweli ;
Imani kwa Yesu itakushindisha.

3. Mungu ataleta taji ya uzima
Kwa mwenye kushinda adui Shetani ;
Tazama Mwokozi, ndiye mwenye nguvu ;
Imani kwa Yesu itakushindisha.

Cfr/ SSS698 IH457

## F-6/4 MWENENDO WA WAAMINI 159

1. Yesu unayenipenda, leo nijifiche kwako ;
Zambi kama mvua kubwa zimetaka kunishinda.
Ee Mwokozi, unifiche, unitwae niwe kwako,
Niokoke kwa mabaya na nisiwe mbali nawe.

2. Wewe tu ni kimbilio, hapa ni matata mengi ;
Ninakuhitaji sana, Ee usiniache pekee.
Mimi ninakuamini, wewe Musaidizi wangu ;
Chini ya mabawa yako ninachungwa na salama.

3. Yote ninayoitaji ninapata kwako, Bwana ;
Roho inapolegea, unisimamishe tena.
Wewe mwenye haki pia, mimi mwenye zambi kubwa ;
Wewe pekee unaweza kusafisha moyo kweli.

4. Neema nyingi iko kwako kufunika zambi zangu ;
Unitwae, unichunge, unilinde hata mwisho.

Hivi nikukaribie, unishike kwa mikono :
Nikujue wewe pekee, hapa chini, kule ju-u.

Cfr/ SSS227 IH442 CH309

## C-6/8 MWENENDO WA WAAMINI 160

1. Ee mara ngapi tunasumbuka na roho inalegea,
Tunazungushwa na giza kubwa, tunaogopa sana ?
Sauti tamu ya Bwana Yesu tunasikia kusema :
« Mutoto wangu ninakupenda, sitakuacha daima. »

*:: kwa kila wakati, kwa kila pahali,*
*Aliahidi kuchunga, hataniacha daima ::*

2. Mupenzi, umesahau mbio sauti hii ya mapendo
Ya Bwana Yesu aliyetoa uzima wake kwawe ?
« Mutoto unayechoka sana, kumbuka sitakuacha ;
Niliahidi nitakuchunga na kuwa nawe daima. »

3. Halafu, ndugu, ufarijiwe katika kila matata,
Mwokozi wako anakupenda, hatakuacha kamwe ;
Unyoshe kwake mukono wako, utamukuta karibu,
Faraja tamu kumusikia : « Sitakuacha daima. »

Cfr/ CH285

## G-4/4 MWENENDO WA WAAMINI 161

1. Kati’ mikono yake Yesu ananilinda,
Katika pendo kubwa ninapumzika sana.
Ninasikia sasa sauti yake Bwana,
Na inanikumbusha mbingu na raha yake.

*Kati’ mikono yake Yesu ananilinda Kati’*
*Katika pendo kubwa ninapumzika sana.*

2. Kati’ mikono yake nitapumzika kimya,
Yesu atanilinda, yeye uwezo wangu.
Sasa hakuna shaka, wala sioni woga ;
Saa ya kupata taabu, Yesu anafariji.

3. Yesu Mwokozi wangu aliyenikomboa
Atanificha kwake, katika Mwamba nguvu.
Kwa siku ya matata na majaribu tele,
Ninangojea Yesu, atarudia kwami.

Cfr/ SSS57 RS653 CV244 CH535

## F-3/4 MWENENDO WA WAAMINI 162

1. Tukikwenda kamoja kushikana na Mungu,
Tunapata amani na raha ;
Tukifanya daima yanayomupendeza,
Ni karibu kwa kutusaidia.

*Raha, furaha, tunapata kwa Bwana,*

*Tukidumu katika kuamini, kutii.*

2. Kama pepo, tufani zikivuma kabisa,
Zinakoma kwa neno la Yesu ;
Tukiona jaribu na ku'goza adui,
Tutashinda kwa nguvu ya Yesu.

3. Hatuwezi kujua pendo tamu la Mungu
Na furaha ya kweli moyoni,
Kama hatujatoa vitu vyote kwa Bwana
Na kutii ma-agizo ya Mungu.

4. Tuna raha ya Mungu kwa shindano lo lote,
Tukitii na tukimusadiki ;
Jua lake la pendo linawa-angazia
Wa-amini na wenye kutii.

Cfr/ SSS642 RS459 IH402 CH391

## Eb-4/4 MWENENDO WA WAAMINI 163

1. Yesu, Muchungaji wetu mwema, utuchunge siku zote,
Utulishe sisi kundi lako na chakula cha milele.
:: Bwana Yesu, Bwana Yesu, sisi wako, utuchunge ::

2. Tuna taabu na mateso mengi, sisi ni zaifu sana ;
Tunajaribiwa na Shetani, utulinde kwa mapendo.
:: Bwana Yesu, Bwana Yesu, usikie tukiomba ::

3. Ulisema utatupokea hata sisi wenye zambi ;
Una neema na rehema nyingi, utuhurumie sisi.
:: Bwana Yesu, Bwana Yesu, tunakutafuta sana ::

4. Yesu, uwe nasi hata mwisho, tusiache njia yako ;
Tukufuate kwa mapenzi yako, hivi tutakupendeza.
:: Bwana Yesu, Bwana Yesu, utukaribishe kwako ::

Cfr/ SSS1164 IH38 CH353

## Ab-3/4 MWENENDO WA WAAMINI 164

1. Njia yote naongozwa kwa mukono wa Mwokozi ;
Ninaona wema wake, sina shaka wala woga,
Nina raha ya mbinguni, na salama tamu sana,
:: Na katika mambo yote ananitendea mema ::

2. Njia yote naongozwa, ninategemea Yesu ;
Analinda jaribuni, ananipatisha nguvu.
Nikiona kiu hapa, nikichoka kwa safari,
:: Ninapata maji mengi toka Mwamba wa milele ::

3. Njia yote naongozwa kwa mapendo yake bora ;
Ananituliza sana na ahadi yake nzuri.
Nitafika kwake mbingu kufurahi kwa milele,
:: Nitaimba neno hili, Yesu aliniongoza ::

Cfr/ SSS522 IH22 CH260

## G-4/4 MWENENDO WA WAAMINI 165

1. Unachoka kwa matata na masikitiko ?
   Yesu anaita : « Kuja kupumzika. »

2. Nitamutambua wazi kwa alama gani ?
   Ona mbavu na mikono na miguu.

3. Taji nzuri ya Mufalme inapamba kichwa ?
   Ndiyo, utaona taji ya mi-iba.

4. Kama nikifuata Yesu, atanipa nini ?
   Utulivu na salama na furaha.

5. Nikiomba anitwae, atanifukuza ?
   Sivyo, atalinda sana kwa milele.

6. Nikifuata, nikishinda, nitapata mema ?
   Wengi wanashuhudia : « ndiyo, ndiyo. »

Cfr/ SSS401 RS152 IH17 CV209

## F-3/4 MWENENDO WA WAAMINI 166

1. Jua la roho ni wewe, Mwokozi,
   Giza haliko pahali ulipo ;
   Wingu la zambi lisifiche
   Uso wa Bwana machoni mwangu.

2. Hata kwa saa ya kulala usiku
Sitaogopa, wewe ni karibu.
Nitapumzika kwa salama
Kwani unanifunza daima.

3. Saa ya muchana unanishindisha,
Nita-anguka usiponichunga,
Uache nuru ya mbinguni
Kunionyesha njia ya haki.

4. Uwe karibu nami saa ya kufa,
Uniongoze kwa bonde la giza
Unifikishe kwako juu,
Nione uso wako mbinguni.

Cfr/ SSS302 RS947 IH19 CV1

**Ab-4/4** **MWENENDO WA WAAMINI 167**

1. Watu wanakuzarau, woga ni moyoni ?
Huta-achwa peke yako – Yesu hageuki.

*Yesu hageuki, Yesu hageuki,*
*Vitu vyote vinapita, Yesu yuko sawa.*

2. Hata taabu inakuja, majaribu mengi,
Ukumbuke Yesu yuko, yeye ni karibu.

3. Kwa mateso na huzuni, anapenda sawa ;
Umutegeme-e yeye, ndiye mwaminifu.

Cfr/ IH496 CH54

**Eb-3/4** **MWENENDO WA WAAMINI 168**

1. Nikipata ulimwengu wote,
Na kukosa Yesu Mukombozi,
Sitakua na furaha kamwe,
Vitu vya dunia hii ni bule !
Nikipata ulimwengu wote,
Na kukosa Yesu Mukombozi,
Nitakuwa na huzuni sana, Yesu pekee anafurahisha.

2. Kama mimi mutajiri kweli,
Na kuheshimiwa na wengine,
Na kukosa kuwa na taraja
Yakufika muji wa mbinguni ;
Nikipata ulimwengu wote,
Na kukosa Yesu Mukombozi,
Yeye aliyenikufilia, nitakwenda wapi saa ya kufa ?

3. Ee maisha yangu bila Yesu
Ni faida gani kwami hapa ?
Tena kwa milele bila yeye,
Taabu na machozi bila mwisho ;
Hata niki-ishi bila Yesu, nina'gopa sana saa ya kufa,
Kukutana na Mwamuzi Mungu,

Kwa milele bila Mukombozi !

4. Ee furaha iko kwake Yesu, anajua kufariji moyo,
Hata nina zambi nyingi sana, yeye atazisamehe zote ;
Nikiishi na Yesu pamoja, na kukosa mali ya dunia,
Nina vitu vyote kwake Yesu,
Yeye Muchungaji wangu mwema !

Cfr/ CH108

## Ab-3/4 MWENENDO WA WAAMINI 169

1. Nina Rafiki mwema naye alinikufia ;
Alinivuta kwake na amenifanya mupya.
Ni mali yake Yesu tu, ninaongozwa naye ;
Na alinikomboa kwa agano la mapendo.

2. Nina Rafiki mwema aliyeondoa zambi ;
Aliniweka huru na kunipa Roho yake ?
Na vitu vyote ninavyo ninavitoa kwake,
Maisha yangu yake tu, kuimba sifa kwake.

3. Nina Rafiki mwema na ana uwezo wote ;
Pamoja naye Yesu ninashinda majaribu.
Atanitwa-a kwake kwa mungini wa furaha,
Nitasterehe kwake kwa milele na milele.

Cfr/ SSS871 IH269 CV22 CH105

## F-3/4 MWENDO WA WAAMINI 170

1. Mapendo yake Mungu yanatu-unganisha,
‘Shirika wa watakatifu, heri ya mbinguni.

2. Kwa kiti cha ne-ema tukaribie Baba
Kwa tumaini, ujasiri, kwa imani moja.

3. Tunashirikiana uchungu na mateso.
Mizigo tunabebeana kwa mapendo mengi.

4. Tuna-achana huko kwa sikitiko sana,
Tutaonana tena kwake na furaha kubwa.

Cfr/ SSS506 RS946 IH35 CH539

## Ab-4/4 MWENENDO WA WAAMINI 171

1. Ni kutamu sana kwangu kumutegemea Yesu,
Kuamini Neno lake na ahadi zake bora.

*Yesu, Yesu, ninaamini, ninajua wema wake ;*
*Yesu, Yesu, ninapenda, ni rafiki ya damani.*

2. Ni kutamu sana kwangu kumutegemea Yesu,
Kuamini damu yake kusafisha zambi zangu.

3. Ndiyo, ni kutamu sana kumutegemea Yesu,
Kwake ninapata raha, na furaha, na salama.

4. Kumutegemea Yesu ni furaha yangu yote ;
Yeye ni Rafiki bora anayetembea nami.

Cfr/ RS426 IH317 CH373

## D-6/8 MWENENDO WA WAAMINI 172

1. Sina woga kwenda na Mwokozi Yesu,
Ataniongoza na kunibariki ;
Bila Yesu sitakuwa na furaha.
Yesu tu anafukuza woga wote.

*Kila pa'li na Mwokozi sitajua woga*
*Kila pa'li na Mwokozi nitakwenda.*

2. Na Mwokozi sitakuwa peke yangu,
Hata nikiashwa na rafiki zangu ;
Hata akiniongoza kwa mateso,
Nitasifu kwani Yesu ni karibu.

3. Kili pa'li Yesu anaponituma
Kutangaza Neno lake la wokovu,
Nitapenda kwenda kama aki-ita,
Ao kubaki hapa kama akitaka.

4. Yesu ni pamoja nami, nitalala
Saa ya giza la usiku bila woga,
Nikijua kwake mbingu nitafika

Na safari hapa itamalizika.

Cfr/ SSS627 RS423 IH23 CH260

## Bb-3/4 MWENENDO WA WAAMINI 173

1. Bwana Yesu, uniongoze kwa bahari ya maisha,
Hata kwa mawimbi mengi, kwa zoruba ya hatari ;
Bwana Yesu, uniongoze, nakutegemea wewe.

2. Bwana Yesu, uniongoze, utulize moyo wangu ;
Neno moja toka kwako lilinyamazisha pepo.
Bwana Yesu, uniongoze, leta utulivu wako.

3. Bwana Yesu, uniongoze, niyashinde majaribu ;
Mengi yananidanganya, mengi yanafunga macho ;
Bwana Yesu, uniongoze, niwe mushindaji kweli.

4. Bwana Yesu, uniongoze, nitakapovuka ngambo ;
Nikiona woga, giza, leta nuru na amani ;
Bwana Yesu, uniongoze, uwe nami hata mwisho.

Cfr/ SSS555 RS330 IH64 CH297

## F-4/4 MWENENDO WA WAAMINI 174

1. Hakika Yesu Mwamba nguvu,
Nitafichama kwake Yesu.
Kwa saa ya taabu na mateso,

Nitafichama kwake Yesu.

*Ee Yesu yeye pekee ni Mwamba nguvu*
*Kwa kunificha, kuniokoa ;*
*Ee Yesu yeye pekee ni Mwamba nguvu*
*Kwa siku ya hukumu kubwa.*

2. Shetani hataniumiza, nitafichama kwake Yesu ;
Siwezi kuogopa tena, nitafichama kwake Yesu.

3. Hatari ikinifikia, nitafichama kwake Yesu ;
Sitaki kutembea mbali, nitafichama kwake Yesu.

4. Usiku na muchana vile, nitafichama kwake Yesu ;
Atasaidia sikuzote, nitafichama kwake Yesu.

Cfr/ SSS539 IH413

**Ab-6/4** **MWENENDO WA WAAMINI 175**

1. Mapendezi ya dunia sitamani tena ;
Nina-acha yote, Yesu, nifanane nawe.

*Nifanane nawe, Yesu, ao nyumbani ao po pote ;*
*Kila siku ya maisha, nifanane nawe.*

2. Ulivunja kila pingu la makosa yangu,
Hata nikutumikie, nifanane nawe.

3. Toka hapa kwenda mbingu kwa safari nzima.
Nitapasha Neno lako, nifanane nawe.

4. Nikukute kule mbingu, Mukombozi wangu.
Nisikie Neno « Vema », nifanane nawe.

Cfr/ IH349

**F-4/4** **MWENENDO WA WAAMINI 176**

1. Ee, taraja yako ni wapi, ndugu,
Kwa kukusaidia saa ya taabu ?
Una kimbilio katika Kristo,
Ao unategemea nani ?

*Tuna taraja ya kweli, ndugu,*
*Saa ya mateso na saa ya taabu,*
*Mwamba wenye nguvu Bwana Yesu*
*Anayetuchunga kwa mambo yote.*

2. Kamba ya mapendo inakufunga,
Wewe na Mwokozi ni pamoja ?
Saa Shetani anapokujaribu,
Yesu anakupatisha nguvu ?

3. Tutafika mbingu kuona Yesu
Na pamoja tutamushukuru
Kwa kuchunga kwake kwa sikuzote
Na kulipa deni yetu yote.

Cfr/ SSS879 RS180 IH332 CH205

**F-4/4** **MWENENDO WA WAAMINI 177**

1. Ninakuta Bwana Yesu Rafiki yangu kweli,
Kwa mapendo anapita sisi sote,
Kwa matata musaidizi, kwa zambi ni Mwokozi,
Mufariji kwa huzuni yeye pekee.
Na anataka sana nilete taabu kwake,
Mateso, masumbuko, ayabebe.

*Anapenda watu wote, alinikufilia,*
*Mwana wake Mungu na Rafiki yangu !*

2. Kwa dunia alibeba huzuni na mateso,
Alikufilia wenye zambi wote ;
Walipiga, walitesa Mupenzi wake Mungu,
Alibeba taabu ya makosa yetu.
Anastahili kweli kupata sifa nyingi,
Nitamukuza Yesu Kristo pekee.

3. Aliniahidi hivi, hataniacha kamwe,
Atachunga watu wake kwa huzuni ;
Hata kitu gani hapa kinaningoja mimi,
Sitakiogopa kwani Yesu yuko.
Halafu kule mbingu karibu na Mwokozi
Furaha itakuwa kwa milele.

Cfr/ RS360 IH285 CH80

**Bb-4/4** **MWENENDO WA WAAMINI 178**

1. Navutwa kwake Yesu na ninamufurahia,
Uzuri wake unapita vyote vya dunia ;
Siwezi ku-upima kweli kwa mawazo yangu,
Uzuri wake unazidi kuwa bora kwangu !

*Siwezi kueleza uzuri wake huko,*
*Lakini nitaufahamu wote kule mbingu*

2. Mapendo ya ajabu kubwa nayasifu sana,
Yakanivuta kwa upole, nije kwake Bwana ;
Yakanitoa mimi katika unyonge wangu,
Mapendo yake yanazidi kuwa bora kwangu !

*Siwezi kueleza mapendo wake huko,*
*Lakini nitayafahamu yote kule mbingu.*

3. Wokovu wake wa ajabu usifiwe sana,
Uliondoa woga, ukanipa utulivu ;
Napenda Yesu aliyechukua zambi zangu,
Wokovu wake unazidi kuwa bora kwangu.

*Siwezi kueleza wokovu wake huko,*
*Lakini nitaufahamu wote kule mbingu.*

Cfr/ RS458 IH281

## Ab-4/4 MWENENDO WA WAAMINI 179

1. Ninataka kumufuata Yesu Mukombozi
Ama kwa rafiki ama kwa wageni vile ;
Kwa pahali pa furaha ama sikitiko,
Nimukaribie Yesu sikuzote.

*Nimufuate, nimukaribie,*
*Sikuzote na po pote nitembe-e naye ;*
*Nimufuate, nimukaribie,*
*Yesu mbele, mimi nyuma hata mwisho.*

2. Ju-u ya milima nitasikiliza Yesu,
Hata mabondeni nitashikamana naye ;
Jua, giza ; afya, ‘gonjwa ; utulivu, vita ;
Kwa maneno yote Yesu ni karibu.

3. Nikiteka maji ao nikilima shamba,
Nikibaki kwa mungini, ama kwa safari ;
Neno hili moja pekee ninataka sana,
Nimukaribie Yesu sikuzote.

Cfr/ SSS529 IH343

## Ab-6/4MWENENDO WA WAAMINI 180

1. Ee ninataka kusikia hu-u ya neema yake Bwana,
Yeye aliyekufa kwami, maana ananipenda sana.

*Habari za Yesu, habari za Yesu,*
*Na za mapendo yake kwami, ninafurahi kusikia.*

*2.* Ee ninataka kutambua vile mapenzi yake Bwana,
Ili nijue kumufuata, kumutukuza sikuzote.

*3.* Ee ninataka kufahamu vile kitabu chake Mungu,
Hata niweze kuongozwa na Yesu kwa maneno yote.

*4.* Ee ninataka kusikia ju-u ya Yesu kule mbingu ;
Yeye mwenyewe atarudi kutupeleka wote kwake.

Cfr/ SSS571 RS432 IH356 CH325

**F-6/8** **MWENENDO WA WAAMINI 181**

1. Uchunge wakati kusema na Bwana ;
Na vile kusoma Neno takatifu ;
Fanya urafiki na wenye imani ;
Na omba baraka kwa neno lo lote.

2. Uchunge wakati, saa inakimbia ;
Ushinde saa zote pamoja na Bwana ;
Ukimutazama, utabadilishwa
Kupata mufano wa Yesu hakika.

3. Uchunge wakati, atakuongoza ;
Umutegeme-e kwa mambo yo yote ;

Katika furaha, katika huzuni,
Umutumaini, atakushindisha.

4. Uchunge wakati, salama moyoni ;
Yesu atawale hata mafikili ;
Atakufundisha na Roho ya kweli ;
Utatayarishwa kufika mbinguni.

Cfr/ SSS688 IH374 CH365

**Ab-3/4** **MWENENDO WA WAAMINI 182**

1. Unitembeze, Bwana wangu,
Katika njia kwenda mbingu ;
Unipatishe vile nguvu niende mbele nawe, Yesu.

*Niende mbele nawe, Yesu,*
*Katika Neno lake Mungu ;*
*Uniwezeshe kila siku niende mbele nawe, Yesu.*

*2.* Shetani ananijaribu, lakini utanipa nguvu ;
Unisaidie, ninaomba, niende mbele nawe, Yesu.

*3.* Maneno ya dunia hapa siyatamani tena, Bwana ;
Kuliko vyote ninataka niende mbele nawe, Yesu.

*4.* Ninakata-a zambi zote, nataka tu nikupendeze ;
Hata kufika kule mbingu niende mbele nawe, Yesu.

Cfr/ RS797 IH345

## Ab-4/4 MWENENDO WA WAAMINI 183

*1.* Roho yangu inaja-a na furaha na salama,
Maana ninajua Yesu ananifanyia mema.

*Yesu, Yesu, nitafuata Mukombozi wa pekee ;*
*Roho yangu inaja-a na mapendo kwa Mwokozi.*

2. Yesu alinitafuta mwenye kusahau Mungu ;
Alimwanga damu yake kuokoa roho yangu.

3. Sitamani zambi tena, haziwezi kunifunga ;
Munyororo wa Shetani Yesu aliufungua.

4. Ninawaombea ndugu katika dunia pia,
Hata Neno la uzima wataweza kusikia.

Cfr/ RS426 IH317 CH373

## Db-4/4 MWENENDO WA WAAMINI 184

1. Ninapenda kumusifu Bwana Yesu,
Ni Rafiki wangu mwaminifu kweli ;
Alinipa moyo mupya na uzima,
Nani ataweza neno kama hili ?

*Ee mapendo yake ni makubwa !*
*Sina Musaidizi kama Yesu ;*
*Yeye tu aliondosha zambi zangu,*
*Ee, ananipenda sana.*

2. Nilikuwa  na makosa mengi sana,
Moyo wangu ulikuwa na huzuni ;
Yesu alinizungusha na mapendo,
Alinionyesha njia ya wokovu.

3. Ee furaha kujuana naye Bwana,
Na maneno yake yote ya mapendo ;
Kisha siku nitakapofika kwake
Macho yangu yataona uso wake.
Cfr/ CH100

**G-3/4** **MWENENDO WA WAAMINI 185**

1. Kiongozi, Mwana wa Mungu,
Ni karibu na mwaminifu ;
Anatuongoza saa zote, sisi wasafiri jangwani,
Tukichoka, tunafurahi tukimusikia Yesu
Akisema : « Kuja, mupenzi, nitakuongoza mbinguni. »

2. Sikuzote yeye Rafiki ni tayari kutusaidia ;
Na hatutabaki na shaka, na hatutakuwa na woga.
Saa zoruba inapovuma, nafsi inapolegea,
Akisema : « Kuja, mupenzi, nitakuongoza mbinguni. »

3. Kazi yetu inapokwisha, tutatazamia pumziko ;
Damu yake Mwana wa Mungu
Ni taraja yetu ya mbingu.
Hatutaogopa mauti, tutachungwa na Mwokozi,
Akisema : « Kuja, mupenzi, nitakuongoza mbinguni. »

Cfr/ SSS194 RS541 IH412

## G-6/4 MWENENDO WA WAAMINI 186

1. Nisadiki Yesu Kristo sikuzote duniani,
Hata na imani ndogo, nisadiki Yesu pekee.

*Nisadiki Yesu pekee, nisadiki sikuzote,*
*Kati ya bahari gani, nisadiki Yesu pekee.*

2. Roho yake anaagaza roho yangu njia zote,
Nikifuata, sitaanguka, nisadiki Yesu pekee.

3. Ninaimba kwa furaha, ninaomba saa ya taabu,
Kati ya habari vile, nisadiki Yesu pekee.

4. Nisadiki hata mwisho wa uzima wangu hapa,
Hata kwenda kwangu mbingu, nisadiki Yesu pekee.

Cfr/ IH333 CH358

## G-4/4 MWENENDO WA WAAMINI 187

1. Kama una mahitaji, huna mali nyingi tena,
Nja-a vile ikifika kwako nyingi,
Ukumbuke Mungu Baba analinda kila saa,
Leta taabu yako yote kwake Yesu.

*Uiache yote kwake,*
*Acha taabu yako yote kwake Yesu ;*
*Ukimusadiki Mungu, atakupatisha nguvu,*
*Acha taabu yako yote kwake.*

2. Wewe ni mugonjwa vile, mwili unauma sana,
Taabu inaleta woga mwingi kwako ?
Yesu anajua yote naye atakusaidia,
Leta taabu yako yote kwake Yesu.

3. Kama wewe ni muzee, unachoka sikuzote,
Ee, usisahau Mungu yuko nawe ;
Yesu ni karibu sasa, na atakuchunga sana,
Leta taabu yako yote kwake Yesu.

Cfr/ CH296

## F-3/4 MWENENDO WA WAAMINI 188

1. Yesu Mwokozi alinikufia,
Naye amenipa uzima mupya ;
Nikitazama Mwokozi daima,
Kila dakika naishi kwa Bwana.

*Kila dakika nachungwa na Yesu,*
*Kila dakika napata uzima ;*
*Nikitazama Mwokozi daima,*
*Kila dakika naishi kwa Bwana.*

2. Kwa majaribu, mateso na taabu,
Yesu Mwokozi ananishindisha,
Na anabeba mizigo ya roho ;
Kila dakika ananisaidia.

3. Saa ya huzuni, machozi, uchungu,
Saa ya hatari, saa ya uzaifu,
Hata Mwokozi ni kule mbinguni,
Kila dakika ananifikili.

4. Hata ugonjwa unanikamata,
Yesu anaweza kuniponyesha ;
Hata katika maneno yo yote,
Kila dakika ananichungaga.

Cfr/ CV218 IH353 CH267

## Eb-2/4 MWENENDO WA WAAMINI 189

1. Ukichukuliwa na mashaka yako,
Na kuona woga kwamba utashindwa,
Uhesabu tu baraka yake Mungu,
Na utashanga-a kwa rehema yake.

*Uhesabu tu baraka zote,*
*Mungu alikubariki nazo !*
*Ukumbuke mambo yote pia,*
*Na utashanga-a kwa rehema yake.*

2. Na ukisumbushwa na huzuni nyingi,
Ukiona musalaba ni muzito,
Uhesabu tu baraka kila siku,
Na kwa moyo wote utasifu Mungu.

3. Usi-itamani mali ya dunia,
Utajiri wako ni Mwenyezi  Mungu ;
Uhesabu tu baraka na kumbuka
Mali haiwezi kufungua mbingu.

4. Na katika mambo yote huko chini
Ukumbuke pendo kubwa la Mwokozi ;
Vile ujumlishe tu baraka zote,
Tena mwisho atakupeleka kwake.

Cfr/ SSS745 RS5 CV208

## Db-4/4 MWENENDO WA WAAMINI 190

1. Wakati salama inapojaza roho,
Na vile wakati wa taabu,
Umenifundisha kusema kwa kweli :
« Najua Mwokozi ni wangu. »

*Ninajua Yesu Bwana,*
*Ninapata salama moyoni.*

2. Wakati Shetani anaponijaribu,
Salama inachunga roho,
Kwa maana Mwokozi ananikumbuka
Na kunipa nguvu kushinda.

3. Hukumu ya zambi sitaogopa tena,
Mwokozi ali-imaliza
Saa alipobeba makosa Kalvari
Na kuyaondosha kabisa.

4. Ninatazamia kurudi kwake Yesu
Afike katika mawingu,
Nione kwa macho ninayemupenda,
Ni-ishi milele na yeye.

Cfr/ SSS901 RS413 IH271 CH386

**G-4/4** **MWENENDO WA WAAMINI 191**

1. Mufalme wa mapendo ndiye Muchungaji wangu ;
Sipungukiwi kitu kwani mimi ni wa Yesu.

2. Anaongoza kando ya vijito vitulivu ;
Ninakulishwa sikuzote kwa malisho yake.

3. Nawe karibu siogopi sasa hata kufa ;
Na gongo lako, fimbo yako zinanifariji.

4. Kwa sokuzote za maisha nitapata wema ;
Nyumbani mwake nitasifu Muchungaji wangu.

Cfr/ RS394 IH424

**Db-3/4** **MWENENDO WA WAAMINI 192**

1. Ee kundi la Mungu, musiyaogope
Maneno yo yote katika dunia ;
Uwezo wa Mungu anawapa ninyi,
Na anawalinda anawapenda.

*Mumusadiki, mumusadiki,*
*Vyote vinawezekana kwa Yesu.*
*Mumusadiki, mumusadiki,*
*Vyote vinawezekana kwa Yesu.*

2. Ee kundi la Mungu, musiyaogope
Maneno mabaya, huzuni, na taabu ;
Mwokozi mwenyewe atawaongoza,
Yeye alikunywa uchungu wa wote.

3. Ee kundi la Mungu, musiyaogope
Maneno ya kesho musiyoyajua ;
Hawezi kuacha mwenye kumwamini
Na atabakia karibu saa zote.

Cfr/ IH327

## D-4/4 MWENENDO WA WAAMINI 193

1. Mwokozi ananiongoza, ni neno la kunifariji !
Pahali pote, sikuzote, mukono wake unaniongoza.

*Mwokozi ananiongoza pahali*
*Pote na mukono wake ;*
*Niwe mufuata wake kweli*
*Na kumutumikia sikuzote.*

2. Pahali pa matata kubwa, pahali pa furaha nyingi,
Si neno kama nikijua mukono wake unaniongoza.

3. Ee Bwana, ninataka sana karibu nawe kubakia ;
Ninafurahi kutambua mukono wake unaniongoza.

4. Na siku kazi yangu hapa nitakapomaliza yote,
Mauti sitaiogopa ; Mwokozi atanifikisha kwake.

Cfr/ SSS542 IH71 CH282

## Ab-3/4 MWENENDO WA WAAMINI 194

1. Mwokozi aliniambia : « Nitasamehe zambi zako ; »
Furaha inazidi sana, furaha kama ya mbinguni.

*Ee haleluya, nimusifu ! Alisamehe zambi zangu !*
*Pahali pote na saa zote nina furaha ya mbinguni.*

2. Zamani sikujua njia kunifikisha kule mbingu ;
Lakini sasa ninajua Mwokozi alinikufia.

3. Katika utajiri mwingi na hata kwa umasikini,
Pahali pote na saa zote nina furaha ya mbinguni.

Cfr/ RS368 CH155

## G-3/4 MWENENDO WA WAAMINI 195

1. Ninasimama kwake Kristo, yeye Mwamba wa imara ;
Sina mwingine kuamini, yeye tu taraja yangu.

*Ninasimama kwake Kristo*
*Mwamba wa imara, sana,*
*Pengine pote ni muchanga.*

2. Saa giza linapomuficha, ninaamini neema yake ;
Na katikati ya zoruba, ninashika Yesu sana.

3. Ananisimamisha sana ju-u ya ahadi zake ;
Na hata vyote vinaanguka, nimutegemee pekee.

4. Wakati atakaporudi, atanipeleka kwake ;
Atanivika haki yake, sitamukosea tena.

Cfr/ SSS902 RS420 IH329 CH121

## G-6/8 MWENENDO WA WAAMINI 196

1. Zamani nili-ishi kwa zambi, nilikosa nuru,
Lakini sasa nimepokea Kristo ndani yangu.

*Kristo ndani yangu, Kristo ndani yangu,*
*Wokovu mukubwa sana, Kristo ndani yangu.*

2. Kwa moyo wangu nimegeuzwa, nimejazwa tele
Na Roho, nuru, uzima, pendo, *Kristo ndani yangu.*

3. Nataka kufanana na Yesu, kuwa sawa naye ;
Nataka wote wajue kweli *Kristo ndani yangu.*

Cfr/ IH512 CH125

## F-4/4 MWENENDO WA WAAMINI 197

1. Nikiona uzaifu na imani ndogo,
Nikijaribiwa sana, Yesu, unilinde.

*Unilinde vema, unilinde vema,*
*Kwa sababu ya mapendo, unilinde vema.*

2. Peke yangu sitaweza kukushikilia ;

Pendo langu ni zaifu, Yesu, unilinde.

3. Mimi mali yako sasa, ulinikomboa,
Ulitoa damu yako, Yesu, unilinde.

4. Huta-acha nipote-e, unalinda sana ;
Kwani ninakuamini, Yesu, unilinde.

Cfr/ CV232 CH201

## Db-4/4 MWENENDO WA WAAMINI 198

1. Ee Mwokozi, unilinde na uniongoze kweli,
Njia ni matata sana, bila wewe nitaanguka.

*Bwana Yesu, uni'ngoze kwa upole,*
*Nikufuate duniani kila siku, kila saa.*

2. Wewe ndiwe kimbilio kwa wakati wa zoruba,
Nawe siogopi kitu, kwako tumaini langu.

3. Kisha siku ya mauti utanifikisha kwako,
Nitazame uso wako, na machozi yatakwisha.

Cfr/ SSS537 RS370 CH354

## Ab-4/4 KAZI YA WAAMINI 199

1. Napenda kutangaza habari za Mwokozi,
Habari za mapendo na utukufu wake ;
Napenda kuzipasha habari hizi tamu,
Inanifundisha kuliko kila neno.

*Napenda kutangaza habari za Mwokozi,*
*Habari za mapendo ya Yesu Bwana yangu.*

2. Napenda kutangaza habari za Mwokozi,
Ni mushangao kwangu, ajabu kubwa kweli ;
Napenda kuzipasha sababu zilikuwa
Baraka kubwa kwami na ziliniokoa.

3. Napenda kutangaza habari za Mwokozi,
Ni kila mara tamu kuliko kwa mutima ;
Napenda kuzipasha ; wengine hata leo
Hawajazisikia, hawajaokolewa.

4. Napenda kutangaza habari za Mwokozi
Kwa watu wenye nja-a, kwa watu wengine kiu ;
Na nitakapofika mbinguni, nitaimba
Habari hizi tena, habari za mapendo.

Cfr/ SSS46 RS606 IH155 CH87

## Bb-4/4 KAZI YA WAAMINI 200

1. Watu wa Mungu, mumalize kazi
Ya kuhubiri Neno la Mwokozi ;

Yeye aliyeumba watu wote
Hatari mutu kupotea kwake.

*Hubiri watu Neno la Yesu,*
*La ukombozi, salama na wokovu.*

2. Tazama watu wanafungwa sana
Katika giza la makosa mengi ;
Na wanangoja kusikia neno
La Yesu mwenye kuwakufilia.

3. Pasha habari watu wasikie
Mungu alionyesha pendo lake
Siku alipotuma Bwana Yesu
Awe Mwokozi kwa wenye makosa.

4. Tuma vijana wako kutumika
Kazi ya Mungu kwa pahali pote ;
Na toa mali kwa kuwasaidia,
Yesu atakurudishia yote.

Cfr/ IH471

## G-4/4 KAZI YA WAAMINI 201

1. Nitaka sana kusikia Neno yako waziwazi,
Na nitakwenda kutafuta wenye kupotea mbali,

2. Uniongoze ili mimi nitafute wapotevu

Na kuwaleta kwako, Bwana, waokoke, wakufuate.

3. Unipatishe nguvu, Bwana, nisimame kwa imara ;
Unifundishe, kisha mimi nitawafundisha wana wako.

4. Ufanye kazi yako nami, pa'li gani, kila siku ;
Nataka kusaidia wenye mahitaji na huzuni.

Cfr/ RS602 IH337

**Bb-4/4 KAZI YA WAAMINI 202**

1. Kutumika kazi kwa Mwokozi Yesu
Kunaniletea shangwe ;
Roho yangu inapata kufurahi kutumika kazi yake.

*Kutumika kazi yake ninaleta vitu vyote ;*
*Ninataka shangwe nyingi kutumika kazi yake.*

2. Kutumika kazi kwa Mwokozi Yesu
Kunaniletea shangwe ;
Nitaimba hata kati ya huzuni, kutumika kazi yake.

3. Kutumika kazi kwa Mwokozi Yesu
Kunaniletea shangwe ;
Kila siku Yesu ananiongoza kutumika kazi yake.

4. Kutumika kazi kwa Mwokozi Yesu
Kunaniletea shangwe ;

Ninaleta vitu vyangu vyote kwake
Kutumika kazi yake.

Cfr/ IH293

## Bb-4/4 KAZI YA WAAMINI 203

1. Simama kwa Mufalme, askari yake Yesu !
Nyanyua na furaha bendera yake safi ;
Tufuate nyuma yake kushinda Diabolo,
Mwenye kutudanganya, mwenye kutuonea.

2. Sikia baragumu, linatuita sasa !
Tuendele-e mbele, kusudi ni kushinda ;
Tusiogope kamwe hatari ya shindano,
Lakini tupigane kwa nguvu yake Mungu.

3. Simama, fanya vita kwa Jina lake Yesu !
Tuvikwe na silaha ya haki kwa kifua ;
Hakika tutashinda na ngabo ya imani,
Kofia ya wokovu, upanga ndio Neno.

4. Shindano letu hapa 'takwisha siku moja,
Tupige vita leo, pumziko ni mbinguni ;
Na kila mushindaji atapokea taji
Na utukufu tele karibu na Mufalme.

Cfr/ SSS680 RS52 IH180 CV204

## D-2/4 KAZI YA WAAMINI 204

1. Ee bendera inatwekwa kututangulia,
Tusione woga tena, twende kwa kushinda.

*Bwana Yesu anakuja, tumutazamie,*
*Kwa uwezo wake Yesu atatushindisha.*

2. Ee Shetani ni karibu, anatutafuta,
Anataka tuanguke, tufe, tupote-e.

3. Tunajua Bwana Yesu ni pamoja nasi ;
Tusimame sawasawa na askari wema.

4. Vita kubwa, vita kali iko mbele yetu ;
Tuwe watu wahodari, twende, tutashinda.

5. Basi, kwa bendera yake tunashikamana ;
Atutie nguvu yake hata kuja kwake.

Cfr/ SSS669 IH168 CV193

## Bb-4/4 KAZI YA WAAMINI 205

1. Chini ya bendera yake Yesu Kristo
Tunakwenda mbele sasa ;
Tunainyanyua watu waione, tuki-imba sifa kwake.

*Twende mbele, twende mbele,*

*Kwa Kristo tuna-acha yote ;*
*Tumuvike taji, tumwimbie chini ya bendera yake.*

2. Musala wake ni bendera yetu,
Tutashinda chini yake ;
Sisi ni askari za Mufalme Yesu, hatutaogopa kamwe.

3. Kwa pahali pote pa dunia hii tutangaze Neno lake ;
Wanye kuamini wataokolewa, watakuwa wana wake.

4. Basi asubui ni karibu sana Yesu atakapokuja
Mushindaji wa adui zake zote, duniani kutawala.

Cfr/ SSS675 IH182 CV196

## Bb-4/4 KAZI YA WAAMINI 206

1. Uwatafute wanaopotea,
Kwa pendo uwaondoe kwa zambi ;
Lia na wenye huzuni rohoni,
Uwapeleke kwa Yesu Mwokozi !

*Uwatafute wanaopotea !*
*Yesu Mwokozi atawaokoa.*

2. Anatafuta waliokimbia,
Anawangoja warudi upesi ;
Uwafundishe kwa pendo na kweli
Ju-u ya neema na haki ya Yesu.

3. Ndani ya roho na katika, siri
Hakose wanatafuta wokovu ;
Uwaongoze kwa Yesu Mwokozi,
Uwaonyeshe mapendo ya Mungu.

4. Uwatafute wanaopotea.
Mungu atakupa pendo na nguvu ;
Uwapeleke kwa Yesu Mwokozi !
Ataokoa wanaoamini.

Cfr/ SSS814 RS435 IH397 CH486

## F-4/4 KAZI YA WAAMINI 207

1. Fanyia Mungu kazi, usiku unakuja,
Utumikie Mungu siku zako zote.
Anza mapema sana, dumu muchana kutwa,
Usiku unakuja, kazi itakwisha.

2. Fanyia Mungu kazi kama ingali jua,
Usipoteze bule siku zako hapa !
Uyatimize yote bila kukosa neno ;
Usiku unakuja, kazi itakwisha.

3. Fanyia Mungu kazi, saa inapita mbio,
Fanya bidi-i sana kutafuta ndugu !
Utumikie Mungu kwa nguvu yako yote ;
Usiku unakuja, kazi itakwisha.

Cfr/ SSS778 RS429 IH410 CH493

**C-4/4 KAZI YA WAAMINI 208**

1. Penda mbegu njema, anza asubui,
Omba Mungu sana kubariki kazi.
Kwa wakati wake utakwenda vile
Na kuvuna mbegu na furaha tele.

*:: Twende kwa mavuno, twende kwa mavuno,*
*Kwa furaha kubwa twende kwa mavuno ::*

*2.* Penda mbegu njema ju-u ya milima,
Na tuendele-e hata mabondeni !
Neno lake Mungu litawafungua
Watu wa makosa kwa furaha kubwa.

*3.* Panda mbegu njema hata kwa machozi,
Ukumbuke Yesu, leo uhubiri !
Bwana wetu Yesu atakuja tena
Na zawabu yetu kwa furaha kubwa.

Cfr/ SSS757 RS463 IH386

**Eb-4/4 KAZI YA WAAMINI 209**

1. Ee askari, twende, vita tuipige,
Macho yetu yawe ju-u ya Mufalme ;

Anatuongoza kwa kupiga vita,
Twende mbele na kufuata nyuma yake Bwana.

*Twende mbele, sisi askari, vita twipige ;*
*Musalaba wake unatangulia.*

2. Kweli tutashinda jeshi la Shetani,
Ee askari, twende mbele na Mufalme ;
Watatetemeka wanaposikia
Nyimbo zetu za kusifu Yesu Kristo Bwana.

3. Kama jeshi kubwa twende naye mbele,
Tunafuata ndugu zetu za zamani ;
Katika Mwokozi tuna roho moja,
Mafundisho na mapendo na taraja sawa.

4. Basi ninyi ndugu, tu-ungane sasa,
Tushirikiane kumusifu Yesu ;
Sifa, utukufu kwake Kristo Bwana,
Wimbo huu tutauimba kwake milele.

Cfr/ SSS706 RS460 IH177 CH343

## F-6/8 KAZI YA WAAMINI 210

1. Askari wahodari, tusimame kwa kushinda ;
Tupige vita kali kwa wakati wa muchana.
Adui wanangoja, ndugu, tusiwaogope ;
Imani ni uwezo wetu kwa kushinda wote.

*Imani kwa Yesu Kristo, imani kwa Yesu Kristo,*
*Imani kwa Yesu Kristo ni uwezo wetu.*

2. Bendera ni mapendo, na upanga Neno lake ;
Tufuate na furaha wa-amini wa zamani ;
Kwa nguvu ya imani yao Shetani alishindwa,
Na ngabo ya imani yao ni ngabo yetu vile.

3. Shetani ni tayari, ana hila nyingi sana ;
Tutupe uzaifu wetu, twende kumushinda ;
Tujifungie kweli na kofia ya wokovu ;
Adui za Mwokozi ni zaifu mbele yetu.

4. Mushinda wa adui atapata vazi zuri,
Na Jina lake Yesu atakiri kule mbingu.
Mapendo yakitusukuma twende kupigana ;
Kwa Jina la Mwokozi tutashinda Diabolo.

Cfr/ SSS682 IH171

## Ab-4/4 KAZI YA WAAMINI 211

1. Toka giza watu wengi wanalia :
« Tuma nuru, tuma nuru ! »
Kuna wapotevu, kuna wenye zambi,
Tuma nuru, tuma nuru !

*Tuma nuru, ya Habari Njema, iangaze pa'li pote ;*

*Tuma nuru, ya Habari Njema, iangaze kwa milele.*

2. Leo Mungu anaita, akisema :
   « Tuma nuru, tuma nuru ! »
   Tujitoe kwake, tutafute watu,
   Tuma nuru, tuma nuru !

3. Na tumwombe Mungu neema itangazwe,
   Tuma nuru, tuma nuru !
   Hata watu wengi wapoke-e Kristo,
   Tuma nuru, tuma nuru !

4. Tusichoke sasa kumutumikia,
   Tuma nuru, tuma nuru !
   Mungu atatupa taji ya uzima,
   Tuma nuru, tuma nuru !

Cfr/ SSS1082 RS628 IH475 CH490

## G-3/2 KAZI YA WAAMINI 212

1. Askari wa Mwokozi mimi na mufuata wake,
   Sitaogopa kutangaza Jina la Mwokozi.

2. Sitaogopa majaribu na kupata taabu
   Katika vita na makosa kwa ajili yake.

3. Nitapigana na adui na uwezo wake ;
   Dunia inamuchukia Yesu Bwana wangu.

4. Ee Bwana, niwe muhodari, niwe mwaminifu,
Nibebe taabu na uchungu kwa ne-ema yako.

Cfr/ IH94

**C-4/4** **KAZI YA WAAMINI 213**

1. Nani ni wa Yesu ? amutumikie !
Atafute watu na kuwahubiri !
Nani anataka kujitoa leo
Kumufuata Yesu katika mateso ?

*Mani ni wa Yesu, nimutumikie !*
*Nitafute watu, kwake warudie !*

2. Kwa mapendo yake tunalazimishwa
Kutafuta wenye zambi na makosa ;
Tunaendelea kuhubiri Neno,
Na kuvuta watu ili waokoke.

3. Yesu alitununua sisi sote
Akimwanga damu yake kwa Kalvari ;
Kwake tumepata raha na uhuru,
Tunataka sasa kuwa waaminifu.

4. Hata vita ikiongezeka huko,
Tuko na bendera ya kushinda kwetu ;
Siku ya pumziko inakaribia,

Itabadilisha vita kuwa shangwe !

Cfr/ RS8 IH186

## D-6/8 KAZI YA WAAMINI 214

1. Nikifika kwake Bwana, yeye Mukombozi wangu,
Na sikumutumikia hata siku moja hapa ?

*Nitakwenda kukutana naye na mikono bule,*
*Bila tunda hata moja ? Itakuwa haya kubwa !*

2. Hata siogopi kufa, kitu ninacho-ogopa
Ni kufika kwake Bwana bila nafsi hata moja.

3. Siku nyingi nimeishi bila kumutumikia ;
Zimepita zote bule, zimepita kwa milele !

4. Ee wapenzi, musimame, mutumike kila siku,
Mutafute wapotevu, muwalete kwa milele !

Cfr/ SSS789 IH138 CH485

## Bb-3/4 KAZI YA WAAMINI 215

1. Pendo la Baba wa mbingu linanga-a sikuzote ;
Anataka tusambaze nuru yake duniani.

*Nuru yetu iangaze mbele ya wenzetu huko ;*
*Ionyeshe kila mutu njia wazi ya mbinguni.*

2. Zambi zimetia giza huko chini duniani ;
Macho ya watu wengine wanatazamia nuru.

3. Ndugu wangu, angalia ta-a yako iwa safi,
Ili mutu asikose kuiona, aokoke !

Cfr/ SSS805 IH251 CH476 CV75

## Ab-4/4 KAZI YA WAAMINI 216

1. Ninasikia Muchungaji anayeita toka jangwa,
Akiwaita wapotevu kama kondo-o bila zizi.

*Uwalete, uwalete, uwalete toka zambi zao ;*
*Uwalete, uwalete, uwalete kwake Yesu.*

2. Nani ‘takwenda kusaidia kuwatafuta wapotevu,
Kuwaletea Muchungaji, awaokoe toka zambi ?

3. Katika jangwa wanalia na kwa vilima na mabonde ;
Bwana anakuita wewe :
« Kwenda kuwafikisha kwangu. »

Cfr/ SSS752 RS109 IH32 CV161

## Ab-3/4 KAZI YA WAAMINI 217

1. Shamba la Mungu ni tayari
   Kuvuna mbegu za kukomea ;
   Wavunaji, mufike mbio kwa kuyavuna mavuno yake.

*Bwana Yesu, tunaomba, uwatume watenda kazi,*
*Waokote miganda yote,*
*Na watapata mavuno mengi.*

2. Uwatume mapema sana, na uwatume saa ya muchana ;
   Hata sa-a ya mangaribi wengine waje kutenda kazi.

3. Ee Mukristo, usichelewe,
   Lakini kwenda mbio kwa kazi !
   Macho yako nyanyua kwani
   Mwokozi Yesu yuko karibu !

Cfr/ SSS1086 IH514 CH483

## C-6/8 KAZI YA WAAMINI 218

1. Safari yangu huko ina habari nyingi,
   Na inapita katika giza na jaribu ;
   Najua kwa hakika, Mwokozi ni karibu,
   Na ninamufuata pahali po pote.

*Pamoja na Yesu njiani sina woga ;*
*Ni kweli furaha na heri rohoni pahali pote ;*

*Nitayashiriki mateso pamoja naye,*
*Na nitamufuata Mwokozi hata mwisho.*

2. Nikitangaza Neno la Mungu duniani
Katika mataifa walio wakaidi,
Nina furaha kubwa moyoni mwangu kwani
Mwokozi ni nami pahali po pote.

3. Na Bwana akitaka nibaki hapa kwangu,
Wengine wakitumwa kwa inchi mbalimbali,
Kusudi langu moja, nidumu kumufuata,
Mungini na vile pahali po pote.

4. Si sharti nifahamu kusudi la Mwokozi,
Ni kazi yangu huko kufuata kiongozi ;
Na hata nikibaki ao hata nikikwenda,
Nitafuata Yesu pahali po pote.
Cfr/ IH29

## F-4/4 KUJITOA KWA MUNGU 219

1. Ee Bwana, niwe mufuata wa kweli,
Nikupendeze kwa kila wakati,
Nikikutii na furaha daima,
Hii tu ni njia kupata baraka.

*Ee Yesu Bwana wangu, ninajitoa kwako,*
*Sababu ulimwanga kwa mimi damu yako ;*
*Mufalme wangu ndiwe, unitawale sasa,*

*Maisha yangu yote yawe kwa heshima yako.*

2. Ee Bwana, ulijitoa kwa mimi,
Na ulilipa bei ya zambi zangu ;
Mapendo haya yananisukuma
Maisha yangu kutoa kwa wewe.

3. Ee Bwana, nikupendeze daima,
Kila wakati nikutumikie ;
Mimi tayari kubeba mateso,
Haya, hasara kwa ajili yako.

4. Kuliko mambo mengine yo yote
Ninakusudi kukufurahisha,
Nikiwaleta waliopotea
Karibu nawe wapate uzima
Cfr/ IH354

**Ab-4/4** **KUJITOA KWA MUNGU 220**

1. Yesu, ninauchukua musalaba wangu kwawe,
Nina-acha vitu vyote nilivyovipenda mbele,
Baba, mama, na watoto, ndugu, nyumba, mali yote ;
Hata hivi ninapata utajiri ndani yako.

2. Watu wengi wanacheka, wananizarau sana,
Wananidanganya vile, wewe tu ni mwaminifu.
Mimi ni mufuata wako, nitakuwa kama wewe,
Walitesa Bwana wangu, na watanitesa vile.

3. Taabu zote za dunia zinanikokota kwako.
Huko unanipa neema, kwako nitapata raha ;
Kweli siogopi kwani ninajua unachunga,
Ni furaha sikuzote kukutegemea, Bwana.

4. Nyuma ya maisha yangu nitafika kwako mbingu,
Unaniongoza pale, ninafuata na imani.
Ee furaha kuonana nawe, Bwana na Mupenzi,
Kwa milele nitaimba Haleluya kwako, Yesu.

Cfr/ SSS596 RS558 IH352

## G-3/4 KUJITOA KWA MUNGU 221

1. Yesu, unapita ndugu na rafiki za dunia ;
Kwa maisha yangu yote nikufuate tu karibu.

*Nikufuate wewe, Yesu, nikufuate wewe, Yesu,*
*Kwa maisha yangu yote nikufuate tu karibu.*

2. Sitamani mali tena wala sifa na heshima.
Kitu hiki ninataka, nikufuate tu karibu.

3. Hata unaniongoza kwa mateso na huzuni,
Nitafika siku moja kupumzika kwako, Yesu.

Cfr/ SSS574 IH340 CH377 CV43

## Eb-9/4 KUJITOA KWA MUNGU 222

1. Fanya mapenzi yako, Ee Bwana,
   Mwenye akili nyingi kabisa ;
   Kama udongo unifinyange,
   Ninapongoja kimya kwa wewe.

2. Fanya mapenzi yako, Ee Bwana,
   Unitafute kwa roho yangu ;
   Unitakase, ninakuomba,
   Niweze kuwa kwawe faida.

3. Fanya mapenzi yako, Ee Bwana,
   Mimi zaifu na ninachoka ;
   Wewe ni Mwenye nguvu ya kweli,
   Ee uniguse, uniponyeshe.

4. Fanya mapenzi yako, Ee Bwana,
   Unitawale, ninakuomba ;
   Na unijaze na Roho yako
   Watu waone Yesu tu kwangu.

Cfr/ IH438 CH298

## G-6/8 KUJITOA KWA MUNGU 223

1. Kitu kisi-ingie kutenga
   Mimi na Yesu, Bwana Mupendwa ;

Nimeokoka, sasa sipendi
Kutenda zambi Yesu ni wangu.

*Kitu kisi-ingie kutenga*
*Mimi na Yesu, Bwana Mupendwa ;*
*Sitaki neno kuhuzunisha*
*Yesu Mwokozi na Bwana yangu.*

2. Kitu kisi-ingie kutenga
Mimi na Yesu, Bwana Mupendwa ;
Vyote Mungu asivyovipenda,
Ninaviacha kwa Yesu Bwana.

3. Kitu kisi-ingie kutenga mimi na Yesu, nisijisifu ;
Hata rafiki wasitutenge, ninakusudi kumupendeza.

4. Kitu kisi-ingie kutenga mimi na Yesu, hata mateso ;
Nitamupenda na kumufuata,
Nitashindishwa kwa nguvu yake.

Cfr/ IH275

## F-4/4 KUJITOA KWA MUNGU 224

1. Yote kwa Mwokozi wangu, Kwaye nguvu yangu yote,
Mafikili na matendo, vile siku zangu zote.

*Yote kwa Mwokozi wangu, yote kwaye tu daima ;*
*Yote kwa Mwokozi wangu, utukufu na heshima.*

2. Hii mikono na migu-u ni kwa kazi yake Yesu ;
Macho yatazame ju-u, na midomo imusifu.

3. Tangu nilipotazama Yesu kule kwa Kalvari,
Vitu vyote vya dunia vilikuwa bule kwami.

4. Ee ajabu kubwa Yesu, yeye Bwana wa wabwana.
Ananipokea kwake na mapendo ya kuzidi !

Cfr/ IH316 CH257

**F-4/4** **KUJITOA KWA MUNGU 225**

1. Bwana, upokee maisha yangu
Yawe yako tu kwa sikuzote ;
Na mikono ninakupa itumike kazi ya mapendo
Kwa kukutukuza, Bwana.

2. Hii migu-u yangu upoke-e ikimbie kukutumikia ;
Na sauti ukamate kwa kuimba sifa yako, Yesu,
Wewe ni Mufalme wangu.

3. Na midomo vile itangaze
Neno lako kwa wenye makosa ;
Mali yangu yote iwe mali yako, Yesu Bwana wangu,
Kwa kufanya kazi yako.

4. Kwa migu-u yako, Bwana Yesu,
Ninatoa mwili wangu wote ;

Ee ninakupenda, Bwana, sikuzote ninataka sana
Wewe pekee utukuzwe.

Cfr/ IH375 CH362

## C-6/8 KUJITOA KWA MUNGU 226

1. Nilikubali kutoa uzima wangu kwawe,
Na damu ilimwangika upate kuokolewa ;
*:: Kwa wewe niliutoa mwili, kwami utatoa nini ?::*

2. Na niliacha mungini wa Baba wangu ju-u,
Kufika huko dunia na giza lake na taabu ;
*:: Kwa wewe niliziacha mbingu,*
*Kwami uta-acha nini ?::*

3. Ee nilibeba uchungu kushinda mafikili,
Usi-ingie kwa moto kuteswa pale milele ;
*:: Kwa wewe nilizibeba zote, kwami utabeba nini ?::*

4. Kutoka kule mbinguni niliyaleta kwako
Mapendo, vile wokovu, na usamehe wa zambi ;
*:: Kwa wewe niliyaleta yote, kwami utaleta nini ?::*

Cfr/ IH341 CH290

## Ab-4/4 KUJITOA KWA MUNGU 227

1. Mimi wako, Bwana, nimesikia sauti ya mapendo ;
Nina hamu sana kuvutwa tena karibu nawe, Bwana.

*Univute, univute kwa musalaba wako, Bwana ;*
*Univute, Bwana, univute kwako nibakie pale tu.*

2. Ee, unitakase kwa kazi yako
Kwa neema, Bwana Yesu ;
Roho yangu ikutazame hata ninakupenda pekee.

3. Ni kutamu sana kushinda saa ya maombi mbele yako,
Ninapoinama kusemezana nawe, Mwokozi wangu.

4. Sijajua bado mapendo yako kwa mimi duniani,
Shangwe itazidi saa ya kufika
Mbinguni kwako, Bwana.

Cfr/ SSS607 RS561 IH347 CH287

## F-3/4 KUJITOA KWA MUNGU 228

1. Unataka salama na imani zaidi,
Umeomba saa nyingi kushinda ?
Hutapata pumziko ao baraka ya Bwana
Hata unajitoa kwa Mungu.

*Umetoa maisha mazima kwa Mungu,*
*Na Roho anakutawala ?*
*Utapata baraka na salama moyoni,*

*Ukimupa mutima na mwili.*

2. Unapenda kufanya ma-agizo ya Bwana,
Na kupata salama na nuru ?
Sharti umupendeze, kumufuata kabisa,
Ujitoe mwenyewe kwa Mungu.

3. Tutaweza kujua pendo toka mbinguni
Na furaha kuja-a moyoni,
Upatano mutamu kwa migu-u ya Yesu
Kama tukijitoa kwa Mungu.

Cfr/ IH351

**Ab-3/4** **KUJITOA KWA MUNGU 229**

1. Ninakushukuru, Bwana, kwani uliniokoa ;
Vile ulinisafisha niwe chombo chako safi.

*Chombo chako, Bwana Yesu,*
*Niko mikononi mwako ;*
*Unijaze, utumie, kila siku, kila saa.*

2. Mimi chombo ‘tupu, Bwana, unijaze na baraka ;
Hivi maji ya uzima yatatoka ndani yangu.

3. Sina nguvu ila yako, ndiyo Roho yako, Mungu ;
Unijaze na uwezo niwe mushuhuda wako.

4. Mimi chombo cha udongo, utukuzwe ndani yangu ;
Ulininunua Bwana, niwe kweli mali yako.

Cfr/ RS781 IH387 CH286

## D-4/4 KUJITOA KWA MUNGU 230

1. Yesu, ninakutolea vitu vyangu vyote leo,
Nikupende, nikufuate sikuzote duniani.

*Ninakupa vyote, ninakupa vyote,*
*Vyote kwako, Bwana Yesu, ninakupa vyote.*

2. Kwa migu-u yako, Yesu, nikunyenyeke-e sasa ;
Ninakutolea vyote, roho, mwili, na kutaka.

3. Ninakupa mali yangu, sitaitamani tena ;
Ulikuwa masikini ili niwe mutajiri.

4. Kwa baraka ninakuja, unijaze Roho yako ;
Uni'ngoze, nipa nguvu, niwe mushindaji kweli.

Cfr/ SSS601 RS581 IH348 CV172

## G-4/4 KUJITOA KWA MUNGU 231

1. Nimeahidi, Yesu, nitakutumikia ;
Usiniache kamwe, Rafiki yangu mwema ;

Sitaogopa taabu pamoja nawe, Yesu,
Na sitahangaika, nikiongwa nawe.

2. Ee Bwana, unichunge katika majaribu
Yanayonizunguka kwa kunitamanisha ;
Adui ni karibu, ni hata ndani yangu ;
Ee Bwana, karibia na chunga nafsi yangu.

3. Umeahidi, Yesu, kwa watumishi wako
Kukaa pamoja nawe katika utukufu ;
Nimeahidi, Yesu, nitakutumikia
Unipatishe nguvu nifuate nyuma yako.

Cfr/ IH368

**Db-4/4 KUJITOA KWA MUNGU 232**

1. Yesu, nivutwe karibu nawe,
Ninakupenda, Mwokozi muzuri ;
Uliyekufa musalabani,
Unizungushe na pendo na neema,
Unizungushe na pendo na neema.

2. Yesu, nivutwe, mimi ni bule,
Sina zawadi kwa kukutolea ;
Mimi muchafu katika moyo,
Unipokee, unioshe kwa damu.

3. Yesu, nivutwe, nikupe yote

Niliyo nayo, Ee Bwana Mupendwa ;
Ninakuomba, uyaondoe
Yote yanayonitenga na wewe,
Yote yanayonitenga na wewe.

4. Yesu, nivutwe karibu nawe,
Hata kwa mwisho wa vita na taabu ;
Tena mbinguni nitabakia,
Karibu nawe, Ee Yesu Mwokozi.

Cfr/ RS584

## F-4/4 KUJITOA KWA MUNGU 233

1. Nasikia Bwana Yesu, anaita nimufuate ;
Anaponitangulia, nitafuata Yesu njia yote.

*Nitafuata nyayo zake, nitafuata nyayo zake,*
*Nitafuata nyayo zake, nitafuata Yesu njia yote.*

2. Nitafuata Bwana Yesu hata kwa mateso, kufa,
Nitafufuliwa naye, nitafuata Yesu njia yote.

3. Atanipa neema yake kwa kudumu hata mwisho,
Hata nitakapomwona
Yesu Bwana wangu kule mbingu.

Cfr/ RS297 IH200 CV180

**Db-4/4** **MAOMBI 234**

1. Pahali pa salama tamu ni mbele yake Bwana ;
Makosa ni pahali pale kwa kututesa tena.

*Ee Yesu Mukombozi uliyetumwa kwetu,*
*Uchunge watu wako wote karibu nawe.*

2. Pahali pa furaha nzuri ni mbele yake Bwana ;
Tunapoweza kukutana naye Mwokozi wetu.

3. Pahali pa uhuru vile ni mbele yake Bwana ;
Pahali pa furaha tele na ustarehe kweli.

Cfr/ IH336

**F-4/4** **MAOMBI 235**

1. Yesu ni Rafiki yetu anayenipenda kweli,
Tunaweza kumwambia mahitaji yetu yote.
Siku nyingi tunabeba taabu na huzuni kubwa.
Kwa sababu tuna-acha kumwambia kila neno.

2. Tunapata majaribu na masikitiko sana ;
Tusishinde na huzuni, twende kumwambia Bwana
Kweli hatuna rafiki kama Yesu Musaidia
Anayefahamu kwamba sisi ni zaifu sana.

3. Tunachoka na uzito wa makosa sikuzote ?
Bwana Yesu ni Mwokozi, atatupokea wote.
Watu wanatuchukia ? Twende kumwambia Bwana ;
Yeye atatufariji, atachunga na mapendo.
Cfr/ SSS319 CV234 IH384 CH383

**Eb-4/4**

## MAOMBI 236

1. Mukate wa uzima, Bwana, uvunje,
Kama zamani kando ya bahari ;
Gawa maneno yako kwa roho yangu ;
Ee nina hamu kubwa kwawe, Yesu.

2. Bariki Neno lako kwa rho yangu,
Kama mukate kule Galilaya,
Nipate kuwa huru toka makosa,
Salama yako itanitawala.

3. Mukate wa uzima ni wewe, Bwana ;
Kwa Neno lako nimeokolewa.
Unifundishe, Bwana, ninakusihi,
Kulifahamu na kutii daima.

4. Ee unijaze, Bwana, na Roho yako,
Naye atanifungulia macho ;
Atafunua kwami kitabu chako,
Na ndani yake nikuone, Kristo.

Cfr/ RS2 IH99 CH6

**Ab-2/2** **MAOMBI 237**

1. Zamani, Pentekote, Mungu, ulituma nguvu ;
Na hivi leo tunaomba kwa baraka yako.

*Ee Mungu, tuma nguvu, uwezo wa zamani,*
*Baraka ya Roho utume leo, Mungu ;*
*Tuma nguvu yako ya Pentekote, Mungu,*
*Waovu waokoke, na upate heshima.*

2. Kwa kazi za uwezo wako tengeneza mioyo ;
Uje na kutawala leo kila mutu wako.

3. Ondosha zambi, washa roho, tuwe na uwezo ;
Kwa kila moyo wa kungoja, Mungu, tia nguvu.

4. Na sasa, Mungu, sisi sote tuko mbele yako ;
Baraka yako tunangoja, usitupitie.

Cfr/ IH149

**Ab-3/4** **MAOMBI 238**

1. Nakuhitaji, Yesu, Mwokozi wangu mwema,
Sauti yoko nzuri inilete-e raha.

Nakuhitaji, Yesu, muchana na usiku ;

Unibariki sasa, ninakukaribia.

2. Nakuhitaji, Yesu, unionyeshe njia,
Na unitimizie ahadi za ne-ema.

3. Nakuhitaji, Yesu, uwe karibu nami,
Nipate kulishinda jaribu la Shetani.

4. Nakuhitaji, Yesu, katika mambo yote,
Kwa kuwa bila wewe, maisha hayafai.

5. Nakuhitaji, Yesu, njiani huko chini,
Nipate kuwa kwako milele na milele.

Cfr/ SSS577 CV249 IH100 CH294

**Ab-4/4** **MAOMBI 239**

1. Yesu, Mwenye pendo kubwa, usinipitie ;
Ndani ya maombi yangu, unibarikie.

*Yesu, Yesu, unisikilie,*
*Ukiwabariki wote, usinipitie.*

2. Miaka mengi nilifuata njia ya uovu ;
Nilikuwa mutumishi wa mudanganyifu.

3. Ninakiri zambi zangu mbele yako, Bwana ;
Roho yangu imevunjwa, uponyeshe sasa.

4. Wewe, Yesu, ni kisima cha furaha yetu ;
Nani Muchungaji mwema ila Bwana Yesu ?

Cfr/ SSS488 RS280 IH254 CH238

## Eb-9/8 MAOMBI 240

1. Ninakuomba, Yesu Mupenzi,
Nina miziko mingi mizito ;
Katika taabu utasaidia, unanipenda na kunichunga.

*Ninakuomba, Yesu Mupenzi,*
*Nina mizigo mingi rohoni ;*
*Ninakuomba, Yesu Mupenzi,*
*Wewe mumoja utasaidia.*

2. Ninakuomba, Yesu Mupenzi,
Wewe Rafiki mwenye mapendo ;
Nikikuomba, utasikia, wewe utaondosha matata.

3. Ninapojaribiwa na nguvu,
Mutu mwingine hatasaidia ;
Ninakuomba, Yesu Mupenzi, kweli utashiriki mateso.

4. Siku nyingine vitu vibaya vinanitamanisha hakika ;
Ninakuomba unisaidie, Yesu, unishindishe kabisa.

Cfr/ IH422

**Ab-3/4** **MAOMBI 241**

1. Ee Yesu, nataka usafi kwa roho,
Nataka uishi daima moyoni ;
Ondosha sanamu, uchafu wo wote,
Na unisafishe nipate usafi.

*Unisafishe sasa kutubu,*
*Ee, unisafishe nipate usafi.*

2. Ee Yesu, tazama na unisaidie,
Nataka kuishi kwa kukupendeza.
Sitaki kufanya mapenzi ya mwili,
Ee unisafishe nipate usafi.

3. Ee Yesu, sikia na jibu maombi,
Ingia moyoni, unibadilishe ;
Nataka salama, nataka furaha,
Ee unisafishe nipate usafi.

Cfr/ SSS569 RS156 IH382

**G-6/4** **MAOMBI 242**

1. Mungu, umetuma kwetu Roho yako Musaidizi ;
Kwa kuishi ndani yetu, vile kutujaza roho.

*Unijaze Roho yako, Mungu, unijaze sasa ;*

*Ninaomba kwako, Mungu, unijaze Roho yako.*

2. Sifahamu namna gani utakavyofanya hivi ;
Bali ninakuhitaji unijaze Roho sasa.

3. Mimi ni zaifu sana, ninaanguka mbele yako :
Sasa unijaze nguvu naye Roho yako, Mungu.

4. Unioshe, 'nifariji, vile unibarikie ;
Ninaamini Neno lako ; Bwana, unijaze Roho.

Cfr/ IH134

## Eb-6/8 MAOMBI 243

1. Sema na roho yangu, Bwana, na pendo kubwa ;
Uniambie wazi : « Sitakuacha pekee. »
Moyo ufunguliwe kwa kusikia neno,
Na unijaze roho na pendo, sifa kwako.

*Sema na roho yangu, Bwana, na pendo kubwa ;*
*Uniambie wazi : « Sitakuacha pekee. »*
*Sasa tayari mimi kukusikia, Bwana :*
*« Utashindishwa nami, na utakuwa huru. »*

2. Sema na wana wako kuwaonyesha njia,
Na unijaze tele na shangwe na furaha,
Ili watoe roho kutumikia Mungu
Hata kurudi kwako kwa kuwatwaa mbinguni.

3. Kama univyoonyesha nia yako zamani,
Uniyafahamishe mapenzi yako kwami,
Uniongoze jinsi kukutukuza, Bwana,
Hata maneno yako nitayatii daima.

Cfr/ RS567 IH373 CH360

## D-6/8 MAOMBI 244

1. Saa ya maombi iko tamu, inatuita kwa Baba Mungu ;
Kwa kiti chake cha ne-ema tunaonyesha hitaji letu ;
Wakati wa huzuni nyingi faraja nzuri tunapata,
Na tunashinda majaribu wakati tunapo-omba Mungu.

2. Saa ya maombi iko tamu,
Furaha nyingi kwa roho zetu ;
Kuleta kwake Yesu Kristo miziko inayotusumbusha.
Tutupe kwake masumbuko, aliahidi kuyabeba ;
Na raha ataleta kwetu wakati tunapo-omba Mungu.

3. Saa ya maombi iko tamu,
Kupata nguvu kwa roho zetu ;
Mwokozi wetu mwaminifu yuko tayari kutubariki.
Inamufurahisha kweli wakati tunapomwamini ;
Anasikia na kujibu wakati tunapo-omba Mungu.
Cfr/ SSS318 RS560 IH30 CH363

## Eb-4/4 MAOMBI 245

1. Ukae nami, giza linafika,
   Usiniache, Mungu, ninaomba,
   Sina mwingine kwa kunisaidia,
   Ee Mufariji, ubakie nami.

2. Nakuhitaji wewe sikuzote,
   Ne-ema yako inanishindisha ;
   Wewe Mwongozi, wewe Musaidia,
   Katika giza ubakie nami.

3. Uzima unapita mbiombio,
   Dunia yote inaharibika ;
   Vitu vyo vyote vinapogeuka
   Hubadiliki, ubakie nami.

4. Adui zote sitawaogopa
   Kama mukono wako ni karibu ;
   Uchungu wa mauti uko wapi ?
   Uliushinda, ubakie nami.

5. Saa ya mauti nitakukumbuka,
   Kwa damu yako nimeokolewa :
   Unipoke-e kwako na salama,
   Katika kufa ubakie nami.

Cfr/ SSS297 CV214 IH363 CH255

## C-6/4 MAOMBI 246

1. Kutoka taabu ya dunia, kutoka vile huzuni ya hapa,
Salama tunaipokea karibu na kiti cha rehema.

2. Na pale Yesu anangoja
Kumwanga kwetu baraka yake ;
Nafasi tamu ya kupita, karibu na kiti cha rehema.

3. Katika inchi pa'li pote rafiki zetu wanainama
Kuombeana kwa imani karibu na kiti cha rehema.

4. Shetani anatujaribu, kwa saa ya taabu, huzuni kubwa,
Tutakimbia wapi ila karibu na kiti cha rehema ?

Cfr/ IH404 CH270

**Bb-6/8** **MAOMBI 247**

1. Mvua ya mbingu inyeshe kama ulivyoahidi ;
Ju-u ya inchi po pote iwe kwa kutubariki.

*Mvua ya mbingu, mvua ya mbingu utume ;*
*Utunyeshe-e baraka, tunakuomba, Ee Mungu.*

2. Mvua ya mbingu inyeshe kwa kulegeza udongo ;
Ju-u ya bande, vilima, mwua ya mbingu ifike.

3. Mvua ya mbingu inyeshe, katika dunia yote ;
Watu wa Mungu wawake, mbegu za roho ziote.

4. Mvua ya mbingu inyeshe, tunapokukaribia ;
Ututumie baraka, tunakuomba, Ee Mungu.

Cfr/ SSS306 CV143 IH380 CH27

## Eb-4/4 MAOMBI 248

1. Mungu wetu mwaminifu ametuahidi sisi
Kusikia na kujibu kama tukiomba kwake.

*Mungu atatusikia kama tukiomba kwake ;*
*Twende sasa na imani, kweli atatusikia.*

2. Mungu atatupa sisi vitu vyote kututosha ;
Kitu gani ni kizuri tutakipokea kwake.

3. Tusi’gope kumwambia mahitaji yetu yote,
Ao makubwa ao madogo, anapenda kusikia.

4. Kwa furaha ao huzuni kila pa’li na saa zote,
Tukimwomba tunajua kwamba atatusikia.

Cfr/ Tabernacle 4-15

## Eb-2/4 MAOMBI 249

1. Omba, omba kwa Mungu pekee,
Usiache kuomba kwake ;

Kweli Mungu aliahidi kukujibu kwa kila kitu.

2. Omba, omba saa ya hitaji,
Mungu atasikia kweli ;
Hata neno ni dogo sana, umwambie, analijua.

3. Omba, omba saa ya jaribu,
Utashinda kwa Jina lake ;
Bwana Yesu anafahamu, atashika mukono wako.

4. Omba, omba na kumwamini,
Tunapashwa kuomba kwake ;
Na imani ngojea Mungu, usiache, atakujibu.

Cfr/ Tabernacle 3-69

## Eb-12/8 MAOMBI 250

1. Unipe usafi zaidi rohoni,
Nione huzuni zaidi kwa zambi ;
Imani zaidi kwa Yesu Mwokozi,
Furaha kwa kazi, vile kwa maombi.

2. Niwe na asante zaidi kwa Mungu,
Na matumaini katika kitabu,
Machozi zaidi kwa taabu ya Bwana,
Na unyenyekevu, upole, na neema.

3. Unipe uwezo kushinda jaribu,

Na vile uhuru na utakatifu,
Na hamu kuona ufalme wa mbingu,
Ili nifanane na Yesu zaidi.

Cfr/ SSS582 RS590 IH338 CV177

## Ab-6/8 MAOMBI 251

1. Bwana, fungua macho yangu
   Kwa kufahamu Neno lako ;
   Unionyeshe mambo matamu
   Ndani ya Neno lako, Bwana.

*Ninainama sasa kwako, unionyeshe kweli yako,*
*Vile mapenzi yako, Bwana, ninakusihi.*

2. Bwana, fungua masikio kwa Neno lako nisikie,
   Kwani sauti yako ni tamu, inanichunga kwa jaribu.

3. Bwana, fungua kinywa changu
   Niwe tayari kutangaza
   Kwa wapotevu kila pahali, wewe uliwakufilia.

Cfr/ RS537 IH371 CH346

## Ab-4/4 MAOMBI 252

1. Yesu Mwokozi, Mwana wake Mungu,

Mara nyingine tunakuabudu,
Siku ya leo ulitusaidia,
Tena kwa kesho ututangulie.

2. Nyuma kidogo jua ‘taingia,
Katika giza utuangalie ;
Na uzilinde roho za wakridto,
Wewe ni zamu, Yesu Kristo Bwana.

3. Sisi tungali hapa kwa dunia,
Wengine wengi wanatuchukia ;
Utupe sisi utulivu wako,
Vile salama, Bwana Yesu Kristo.

Cfr/ SSS291 RS950 CW199

**Bb-4/4** **MAOMBI 253**

1. Unachoka, una roho nzito ?
Sema na Yesu, sema na Yesu ;
Na furaha imekwisha yote ?
Sema na Yesu pekee.

*Sema na Yesu, sema na Yesu,*
*Yeye Rafiki wa kweli ;*
*Si mwingine sawasawa naye.*
*Sema na Yesu pekee.*

2. Unalia kwa huzuni nyingi ?

Sema na Yesu, sema na Yesu ;
Roho yako inaficha zambi ?
Sema na Yesu pekee.

3. Ndugu zako wanakuchukia ?
Sema na Yesu, sema na Yesu,
Walimukata-a Yesu vile,
Sema na Yesu pekee.

4. Unajaribiwa sikuzote ?
Sema na Yesu, sema na Yesu,
Anajua sisi ni zaifu.
Sema na Yesu pekee.

5. Unakosa mali ya dunia ?
Sema na Yesu, sema na Yesu,
Anachunga kila ndege vile.
Sema na Yesu pekee.

Cfr/ RS592 IH453 CV108

**Ab-4/4** **MAOMBI 254**

1. Sasa mangaribi, jua limechuka,
Giza la usiku limetushukia.

2. Yesu, ninataka kupumzika kwako ;
Na baraka yako nitafunga macho.

3. Katika usiku tuma malaika
Wanilinde mimi kando ya kitanda.

4. Kisha asubui, hapa mangaribi,
Leta nguvu, haki, kwa kukupendeza.

Cfr/ IH101

**Bb-2/4** **MAOMBI 255**

1. Bwana, kwa usiku huu utubarikie wote ;
Tunakiri zambi zetu, usamehe, tunaomba.

2. Giza linatuzunguka, na hatari ni karibu,
Tuma malaika zako kusimama kando yetu.

3. Giza halitakuficha, wewe ni karibu nasi ;
Kweli hutalala kamwe, wewe ni Mulinzi wetu.

4. Hata kufa kutafika katikati ya usiku,
Nitakuwa asubui mbele yako kule mbingu.

Cfr/ SSS286 IH494 CV159

**Ab-4/4** **KURUDI KWA KRISTO 256**

1. Siku baragumu yake Mungu itakapolia,
Pambazuko la milele litanga-a ;

Siku ile sisi wa-amini tutaona Yesu,
Ataita kila Jina kwa kitabu.

*Ataita kila Jina, ataita kila Jina,*
*Ataita kila Jina, ataita kila Jina kwa kitabu.*

2. Siku ile watu waliomwamini Bwana Yesu
Watafufuliwa kwanza kwa mawingu ;
Kisha wa-aamini ha-i watanyanyuliwa vile,
Ataita kila Jina kwa kitabu.

3. Tujitoe kwa kutumikia Bwana wetu Yesu
Tufundishe watu njia ya wokovu,
Na wakati kazi yetu itakapokwisha huko,
Ataita kila Jina kwa kitabu.

Cfr/ SSS980 RS528 IH511 CH202

## Ab-6/4 KURUDI KWA KRISTO 257

1. Siku nyingine taabu 'takwisha,
Vile huzuni na majaribu ;
Siku nyingine tutapumzika,
Saa ya kurudi kwa Bwana Yesu.

*Siku nyingine Yesu Mwokozi*
*Atatokea kutukamata ;*
*Tutasikia sauti yake akituita sisi na wewe.*

2. Unasumbuka ? utafurahi ! utasahau kila huzuni.

Utafanana naye Mwokozi, na utamwona uso kwa uso.

3. Tutakutana naye kwa hewa, kisha furaha itatimia ;
Tutaonana na nduvu zetu, tutatukuza Kristo milele.

Cfr/ IH136 CH412

## Bb-3/4 KURUDI KWA KRISTO 258

1. Watu wa Kristo, angalieni,
Mwone alama za kuonyesha
Kwamba Mwokozi atatokea,
Ni yeye tunayemungoja na hamu.

*Atarudi hakika, atarudi hakika,*
*Ni Yesu mwenyewe waliyemukana ;*
*Atarudi hakika, atarudi hakika,*
*Mwenye utukufu atarudi hakika.*

2. Huko dunia, giza na zambi
Zinazunguka watu wa Mungu ;
Mioyo mizito itageuzwa kupata
Furaha kwa siku ya Bwana.

3. Kuja, Mupenzi, tunakungoja,
Hamu ya kukuona ni kubwa ;
Tutakutana ndani ya hewa,
Taraja hii tamu : milele na wewe.

Cfr/ IH133 CH403

## Bb-4/4 KURUDI KWA KRISTO 259

1. Yesu atakapokuja tena kwa kutupeleka kwake,
Atatukuta tayari kweli, ta-a zetu zikinga-a ?

*Ndugu, wewe ni tayari sasa*
*Kukutana naye Bwana ?*
*Saa zote wewe ni mwaminifu ?*
*Leo unatazamia Yesu ?*

2. Atatuita na Jina letu kusimama mbele yake ;
Ukimutoa habari zako, atakuambia : « Vema » ?

3. Hakose sisi ni waaminifu, tukitumikia Bwana ?
Na roho safi tunangojea kuja kwake na furaha ?

4. Heri ni wale wanaogoja kushiriki utukufu ;
Yesu atakapo-onekana, watakwenda naye ju-u.

Cfr/ SSS791 RS517 IH140

## F-4/4 KURUDI KWA KRISTO 260

1. Bonde la mauti halitakuwa siku Yesu atakaporudia,
Bonde la mauti halitakuwa, atatupokea kwake.

*Atatupokea kwake kwa kuishi naye milele ;*
*Tuta-acha dunia ya huzuni kupata furaha kwake.*

2. Sikitiko halitakuwa kamwe siku Yesu atakaporudia,
Sikitiko halitakuwa kamwe, atatupokea kwake.

3. Na kilio hakitakuwa tena siku Yesu atakaporudia,
Na kilio hakitakuwa tena, atatupokea kwake.

4. Nyimbo za furaha tutamwimbia
Siku Yesu atakaporudia,
Nyimbo za furaha tutamwimbia, atatupokea kwake.

Cfr/ SSS1026 CH424

**F-4/4 KURUDI KWA KRISTO 261**

1. Ninangoja asubui, ndiyo siku ya baraka,
Siku taabu na huzuni zitakapokwisha pia ;
Na pamoja na Mwokozi, mbali na dunia hii,
Nitashinda kumwabudu kwa milele na milele.

2. Ninangoja utukufu, unanga-a toka mbali,
Wa Mwokozi wangu Yesu, ndiye « Nyota ya 'subui » ;
Katika mapambazuko nitaona nuru yake,
Na usiku utakwisha, taabu, zambi, na kuchoka.

3. Ninangoja Bwana yangu, aliyenikufilia ;
Tamu ni ahadi yake, « Nitarudi kukuita » ;
Kuja kwake ni karibu, ndiyo, ni karibu sana,

Hamu kwake inazidi, hamu ya kufika kwake.

Cfr/ SSS221 IH213 HW204

**Eb-3/4** **KURUDI KWA KRISTO 262**

1. Bwana, ninakungojea kwa kukutazama,
   Bwana, ninakungojea kurudi kwa mimi.
   Umekwenda mbinguni kunitengenezea
   Nyumba nzuri mbinguni karibu na Bwana.

2. Hapa ninaona woga, kuchoka kabisa,
   Kweli siku ni karibu utakapokuja.
   Kwako tu ni furaha, si machozi na taabu,
   Utukufu mukubwa utakaporudi.

3. Hata sasa ninataka nikupe furaha,
   Siku chake zinabaki kukutumikia.
   Ninangoja kuona macho yake, Ee Bwana.
   Shangwe kubwa kuzidi utakaporudi.

Cfr/ CH395

**Db-6/4** **KURUDI KWA KRISTO 263**

1. Hakose leo tu, tutaona Yesu Rafiki yetu,
   Mwenye kuleta furaha, na mwisho wa taabu zote.

*Tufurahi, Yesu atarudia ;*
*Tuishi kwa leo bila woga,*
*Kweli Mwokozi tutamwona ;*
*Tufurahi, Yesu atarudia.*

2. Hakose leo tu, tutakwenda kwetu mbinguni juu ;
Tutafurahi kabisa, akitufikisha leo.

3. Tufazaike nini ? Tutashinda kwani Mwokozi wetu
Yuko pamoja na sisi kwa sasa na sikuzote.

4. Tuwe watoto wake waaminifu, tukimutumikia,
Tukihubiri habari za Yesu Mwokozi wetu.

Cfr/ IH132

**Eb-2/2 KURUDI KWA KRISTO 264**

1. Yesu atatawala hapa katika mataifa yote,
Na kila mutu wa dunia atamutambuwa yeye Bwana.

2. Toka kusini, kaskazini, watainama kwake Bwana ;
Hata wafalme na wajinga watasikia Neno lake.

3. Atatawala na salama, watu watamusifu Bwana,
Na watapenda Jina lake kama malasi tamu sana.

4. Watu wa makabila yote wataimbia pendo lake ;
Vile sauti za watoto zitabariki Jina lake.

Cfr/ SSS1084 RS646 IH470 CH299

## Bb-4/4 KURUDI KWA KRISTO 265

1. Siku Mwana wake Mungu atakaporudi hapa
Tutaona utukufu wake wazi ;
Ataita watu wake mataifa yote,
Makutano ya furaha ya waamini.

*Makutano ya furaha,*
*Watu walioamini watakusanyika wote ;*
*Makutano ya furaha*
*Ya waamini kwa mungini wa Mwokozi.*

2. Na waliokufa mbele wakimusadiki Yesu,
Toka kimya ya kaburi na bahari,
Watapata mwili mupya, watakwenda nasi vile,
Makutano ya furaha ya waamini.

3. Macho yetu yataona muji wetu kwa mbinguni,
Vile muto ukitelemuka kimya ;
Na rafiki tutaona waliotutangulia,
Makutano ya furaha ya waamini.

4. Ee Mufalme anakuja, atarudi mbio sana,
Siku ya ahadi yake tutaona ;
Tutabadilishwa mbio, kama kupepesa macho,
Kwa milele tutaka-a na Mwokozi.

Cfr/ SSS149 IH139

## G/4/4 MBINGU 266

1. Wananiambia habari za mbingu,
Wanasema nyumba nyingi ni kule,
Wanasema ni pahali pazuri sana,
Wananiambia ju-u ya mbingu.

*Inchi ile nzuri sana,*
*Ni mungini wa Mungu Mwenyezi ;*
*Wananiambia ju-u ya nyumba yangu*
*Inayoningoja pale mbinguni.*

2. Wananiambia kwamba rafiki wengi
Wananingojea sana mbinguni ;
Kule muto wa uzima wenye kungaa
Unatoka kiti cha Mungu Baba.

3. Wananiambia Mufalme yuko pale
Nitamutazama uso kwa uso ;
Wala laana haitakuwa tena kweli
Kwa mungini wa zahabu mbinguni.

4. Wananiambia Yesu atapangusa
Kila chozi la watoto wa Mungu ;
Wanasema taabu haitakuwa tena,
Ni furaha tu pahali pa mbingu.

Cfr/ IH508

## G-4/4 MBINGU 267

1. Kuna muji muzuri mbinguni,
   Kwa imani tunautazama,
   Baba Mungu anapotungoja
   Kwa furaha kutukaribisha.

*Tutaona Yesu Bwana,*
*Vile ndugu waliyomwamini,*
*Tutaona wao wote*
*Kule mbingu pahali pa Mungu.*

2. Tataimba kwa muji wa ngambo
   Nyimbo za wenye kubarikiwa ;
   Taabu itaondoshwa kwa roho,
   Ustarehe pasipo kulia.

3. Kwa mapendo ya Baba wa mbingu
   Na baraka anazozitupa,
   Tutapiga asante ya kweli,
   Vile tutamusifu milele.

Cfr/ SSS964 CV293 IH505 CH425

## C-4/4 MBINGU 268

1. Imba pendo la Mwokozi, imba neema na rehema ;
Anatengeneza nyumba pa’li tutakapoishi.

*Tutakwenda mbinguni,*
*Tutaimba na kumusifu Yesu !*
*Tutaona Bwana, tutamwibia Haleluya !*

2. Wasafiri duniani, sisi watu wa mbinguni ;
Kisha tutafika kwake, tuta-acha taabu zote.

3. Ndugu, tuwe waaminifu, kila siku, kila saa ;
Tutakapo-ona Yesu, taji zetu tutapata.

4. Twende mbele, tutumike, tutamutazama ju-u ;
Mbingu zitafunguliwa, kwa milele tumusifu !

Cfr/ CH378 RS400 IH296 CV298

## G-3/4 MBINGU 269

1. Ninatazama mbingu mbali, ninaona kwa imani,
Muji ule ni muzuri, safi kama bilauri.

*Ee, muji ule wa mbinguni, muji ule ni muzuri,*
*Kule kuna nyumba nyingi, zinangoja kwa waamini ;*
*Nina hamu ya kufika, kwa milele kupumzika.*

2. Misingi ya ukuta wake mawe ya bei ya damani ;

Njia yake ni zahabu safi kama kioo wazi.

3. Hauhitaji jua wala mwezi kuangaza pale,
Kwa ma-ana nuru iko utukufu wake Mungu.

4. Na kila kitu cha uchafu hakitaingia kamwe,
Wale walioandikwa kwa kitabu watakuwa.

5. Na watumishi wake Mungu wataona uso wake,
Na watatawala naye kwa milele na milele.

Cfr/ SSS944 RS389 IH310

**Bb-4/4** **MBINGU 270**

1. Ee furaha kuonana na Mwokozi wangu Kristo,
Kutazama uso wake aliyenikufilia !

*Ninaona uso wake kule mbingu kwa milele ;*
*Nitaona Mukombozi, utukufu wake wote !*

2. Sasa macho yanaona nusu tu katika giza ;
Kule nitaona wazi utukufu wa Mwokozi.

3. Shangwe gani kwake Yesu ! taabu yote itakwisha,
Yote itatengenea, nuru itashinda giza.

4. Nitaona uso wake, nitajua Bwana wangu
Aliyenipenda sana, Mukombozi Yesu Kristo.

Cfr/ RS421 IH482 CH392 CV252

**Ab-4/4 MBINGU 271**

1. Siku zangu zitakapotimia hapa chini,
Nitaona asubui ya uzima,
Nitaona mbinguni Mukombozi wangu Yesu,
Na « Karibu » yake nitasikia.

*Nitamutambua Yesu,*
*Na karibu naye nitabakia,*
*Nitamutambua Yesu*
*Kwa alama za majeraha yake.*

2. Itakuwa furaha kutazama uso wake
Na uzuri wa kutoka macho yake ;
Moyo utafurika kwa uheri na furaha
Kwa pahali aliponifanyizia.

3. Na walio mbinguni wananingojea kwao,
Nakumbuka siku tulipoachana ;
Wataimba kabisa kunikaribisha kule,
Hata hivi nitamwona Yesu kwanza.

Cfr/ SSS967 RS364 IH491 CH8432

**Eb-4/4 MBINGU 272**

1. Kuna muji kule mbingu, umejengwa naye Mungu,
Pale muto wa uzima ni karibu na kiti cha Mungu.

*Tutakusanyika ngambo*
*Kuona Bwana wetu Yesu Kristo ;*
*Tutakusanyika na waamini*
*Kusifu Mwokozi milele.*

2. Kule ngambo inchi nzuri, bila zambi na huzuni,
Nyimbo mpya tutaimba,
Nyimbo kusifu Yesu Mwokozi.

3. Wenye luga mbalimbali wataabudu Mukombozi,
Makabila ya dunia watasifu Mwokozi pamoja.

4. Sasa sisi ni karibu kutazama muji ule ;
Mungu atatupa raha na kutufurahisha milele.

Cfr/ SSS1000 RS664 IH427

## G-4/4 MBINGU 273

1. Tutafufuka kusimama mbele yake Bwana Yesu ;
Habari zetu tutatoa kwake kwa matendo yetu ;

*Nitaonekana mbele yake, Jina langu litaitwa naye ;*
*Sita'gopa, ninaamini damu ya Mwokozi Yesu.*

2. Nitapokea taji ya uzima mikononi mwake ;
Nitaitupa mbele yake Yesu anayestahili.

3. Tutakutana kwa milele pale, taabu itakwisha ;
Mizigo tuta-acha kwa miguu ya Yesu Mukombozi.

Cfr/ RS434

## D-2/4 MBINGU 274

1. Kuna muji wa furaha mbali, mbali sana ;
Wenye kuamini Bwana watakwenda pale.
Tutaimba kwa milele sifa kwa Yesu Mufalme
Anayestahili yote, sifa, sifa kwake.

2. Kuja ku-ungana nasi, unangoja nini ?
Usibishe Yesu hivi, kuja kumwamini.
Tutakuwa na uhuru toka zambi, toka taabu,
Tutaishi naye Yesu, tutabarikiwa.

3. Kule Baba anachunga watu kwa mapendo,
Hivi tukimbie sana, tuna mashindano.
Atawapa wote taji, wenye kumufuata kweli,
Na tutatawala naye kwake kwa milele.

Cfr/ RS680 CV107

## Ab-4/4 MBINGU 275

1. Tuwaze mungini wa mbingu,
Ndio ngambo ya muto wa nuru,
Watu watakatifu ni kule,
Wanavikwa mavazi meupe,
*:: Kule ngambo, kule ngambo,*
*Tuwaze mungini wa mbingu ::*

2. Tuwaze rafiki kwa mbingu,
Walitutangulia zamani,
Wanaishi karibu na Mungu,
Pale wanamwabudu daima,
*:: Kule ngambo, kule ngambo,*
*Tuwaze rafiki kwa mbingu::*

3. Tuwaze Mwokozi wa mbingu,
Alikufa na alifufuka ;
Sasa anatungoja tufike,
Tutamufurahia na shangwe,
*:: Kule ngambo, kule ngambo,*
*Tuwaze Mwokozi wa mbingu::*

4. Saa tutakapofika kule
Ni karibu, na tutaonana
Na rafiki na ndugu za ngambo,
Pamoja na Yesu Mwokozi.
*:: Kule ngambo, kule ngambo,*
*Tuwaze furaha ya mbingu ::*

Cfr/ SSS942 CV273

## G-4/4 KUZALIWA KWA YESU 276

1. Jeshi kuu la malaika wali-imba kule mbingu,
   Utukufu  kwake Mungu, na salama kwa dunia.
   Kila mutu amusifu na kumutukuza sana ;
   :: Tuheshimu Yesu Kristo yeye ndiye Mukombozi ::

2. Ee kujeni tumwabudu, ni Mufalme wa wafalme ;
   Mungu, Baba ya mapendo, alituma Mwana wake.
   Alikuwa kama Mungu, alikuja kama mutu ;
   :: alitoka kule mbingu  kuokoa watu wote ::

3. Mushangao wa ajabu, Mungu amefika huko ;
   Ametupa nuru yake na uzima na wokovu.
   Aliacha utukufu na alijinyenyekeza,
   :: Kristo, Mwana wake Mungu,
   Yeye Bwana wa mbinguni ::

4. Leo malaika ju-u wanafurahia Yesu
   Sisi tumwabudu vile, yeye tu anastahili.
   Tuiname kwake Yesu, yeye pekee ni Mwokozi ;
   :: Sifa iwe kwake Mungu, yeye Bwana wa milele ::

Cfr/ SSS30 RS42 IH47 CH520

## C-4/4 KUZALIWA KWA YESU 277

1. Malaika za mbinguni walitoka kwake Mungu,
Walikuja kutangaza kuzaliwa kwa Mwokozi.

*Tuabudu, tuabudu Yesu Kristo Mukombozi.*

2. Wachungaji walichunga kundi lao kwa usiku ;
Waliona nuru kubwa ikinga-a toka mbingu.

3. Wa-akili toka mbali walifuata nyota yake;
Walikuja na zawadi kuabudu Yesu Kristo.

4. Kwa mutima wako kweli Kristo ni Mufalme wile ?
Kila siku na mapendo unatumikia Yesu ?

Cfr/ IH43

## G-4/4 KUZALIWA KWA YESU 278

1. Ee muji wa betelemu, unalala kimya,
Na nyota nyingi kule mbingu kimya zinapita ;
Kwa ndaki zako nuru ya mbingu inanga-a ;
Linatimizwa kwako leo tumaini lote.

2. Maria aliza-a Bwana Yesu kwa usiku,
Na malaika walikuja na habari tamu.
Ee, nuru kubwa gani ya nyota ilinga-a
Mbinguni kuonyesha pa'li alipozaliwa !

3. Zawadi kubwa sana Mungu alituletea

Kwa saa alipotutumia Mwana wake hapa ;
Atapokea wote wanaomusadiki,
Anafurahi kuingia kuondoa zambi.

4. Mutoto wa Betelehemu, tunaomba sana,
Ondoa zambi na kuosha roho zetu sasa ;
Ukae ndani yetu, kubaki sikuzote,
Rafiki, Mufariji, na Mufalme kwa milele.

Cfr/ SSS26 IH42

## G-2/2 KUZALIWA KWA YESU 279

1. Tunafurahi leo, tunasifu Mungu sana,
Kwa maana alitukumbuka na kutoa Bwana
Aliyekuja kuokoa watu wenye zambi.

*Sikieni habari za faraja, vile furaha ;*
*Ni Habari Njema ya Mwokozi Yesu.*

2. Usiku wachungaji walilinda kundi lao,
Tazama, malaika alionekana kwao ;
Waliogopa sana wakiona nuru kubwa.

3. « Musiogope », malaika aliwa-ambia,
« Habari za furaha ninawaletea ninyi ;
Amezaliwa kwenu leo Kristo ndiye Bwana. »

4. Na wachungaji waliacha kundi, wakisema,

« Ee, twende zetu kwa habari kwa Betelehemu,
Tuone neno hili lililofanyika leo. »

5. Walipofika wakakuta mama na Mutoto
Aliyelala kwa sanduku iliyo ya nyumba ;
Wakatukuza Mungu, wakamushukuru sana.

Cfr/ IH41

## F-3/4 KUZALIWA KWA YESU 280

1. Nyumbani mwa ngombe kwa Betelehemu,
Mutoto wa Mungu alipozaliwa ;
Kwa nyasi Maria alimulalisha,
Na jeshi la mbingu walimutukuza.

2. Na hakuogopa kulia kwa ngombe,
Mutoto wa Mungu alilala kimya.
Ee ninakupenda kabisa, Mwokozi ;
Bakia karibu na mimi saa zote.

Cfr/

## D-2/4 KUZALIWA KWA YESU 281

1. Furaha kubwa kwa dunia, Mufalme amekuja !
Na tumufungulie mioyo aingie,
Yeye Mufalme wetu, yeye Mufalme wetu

Mufalme na vile Bwana wetu.

2. Furaha kubwa kwa dunia, Mwokozi ni Mufalme !
Viumbe vyake vyote, imbeni sifa kwake ;
Musifu na furaha, musifu na furaha,
Musifu na wimbo wa furaha.

3. Masikitiko yatakwisha, na laana ya dunia !
Kusudi lake Bwana kutubariki sana,
Na kuondosha zambi, Na kuondosha zambi,
Kusudi ni kuondosha zambi.

4. Anatawala na rehema, na haki na mapendo !
Tunashanga-a sana kwa pendo lake Bwana,
Na utukufu wake, na utukufu wake,
Mapendo na utukufu wake.

Cfr/ SSS111 IH45 CH522

## G-3/4 KUZALIWA KWA YESU 282

1. Kuna wimbo muzuri, kuna nyota mbinguni,
Kwa sababu Maria anaza-a mutoto ;
Nyota hii inanga-a katika usiku
Kwani amezaliwa Mwokozi Mufalme.

2. Kuna shangwe kabisa kwa usiku wenyewe,
Maana Yesu mutoto ni Mwokozi wa watu ;
Ndiyo, nuru ya nyota ‘nanga-a vizuri ;

Kwani amezaliwa Mwokozi Mufalme.

3. Nuru ya nyota ile, tangu siku ya kale,
Inanga-a katika roho za wa-amini ;
Vile wanafurahi kwa wimbo muzuri,
Kwani amezaliwa Mwokozi Mufalme.

4. Tunaifurahia nuru ya nyota ile,
Tunaimba pamoja na majeshi ya mbingu ;
Kwa habari za Yesu tunashangilia,
Kwani amezaliwa Mwokozi Mufalme.

Cfr/ IH53

**Ab-4/4** **KUZALIWA KWA YESU 283**

1. Kujeni kusifu na furaha nyingi,
Kujeni kusifu Yesu ndiye Mwokozi ;
Alizaliwa kuwa Mukombozi.

*Kujeni kumwabudu, kujeni kumwabudu,*
*Kujeni kumwabudu Yesu Mwokozi.*

2. Bikira Maria aliza-a Yesu,
Ni Mwana wa Mungu, vile Mwana wa Mutu ;
Aliondoa utukufu wake.

3. Pamoja na jeshi la mbinguni ju-u
Tusifu na kuabudu Yesu daima ;

Mwana wa Mungu anapata mwili.

Cfr/ SSS31 RS40 IH48 CH521

## C-6/8 KUZALIWA KWA YESU 284

1. Kwa usiku wa zamani, yote kimya, takatifu,
Mama na Mutoto Yesu walilala kwa kizizi,
Na salama ya mbingu, na salama ya mbingu.

2. Kwa usiku wa zamani, wachungaji waliona
Nuru kubwa kule mbingu, malaika wakisifu,
Haleluya kwa Mungu, Haleluya kwa Mungu !

3. Kwa usiku wa zamani, wa-akili toka mbali
Walifuata nyota kubwa kutafuta Bwana Yesu.
Wakileta zawadi, wakileta zawadi.

4. Kwa usiku wa zamani, Mungu, tunakushukuru ;
Kwa mapendo ya ajabu, ulituma kwetu Yesu
Kuokoa dunia, kuokoa dunia.

Cfr/ IH44 CH523

## D-4/4 KUZALIWA KWA YESU 285

1. Uliacha mbinguni na utukufu
Kufika dunia kwa mimi,

Saa ulipozaliwa kwa Betelemu
Nafasi hukuipata.

*Ingia mayoni mwangu,*
*Bwana nina nafasi kwawe.*

2. Malaika za mbingu walikusifu,
Mufalme mukubwa wa mbingu,
Ulijifanya kuwa bila utukufu,
Na ulijinyenyekeza.

3. Mbweha wana matundu, na ndege vile
Kwa miti vioto vyao ;
Kwawe Mwana wa Mungu, sanduku ya nyama
Ni kama kitanda chako.

4. Ulikuja na neno lenye uzima
Kwa kutufungua sisi ;
Watu walikufunga na kukupeleka
Kwa kufa musalabani.

5. Kisha siku nyingine utarudia,
Mufalme wa utukufu ;
Utani-ita kwako, ukiniambia :
« Mbinguni nafasi iko. »

Cfr/ IH46 CH245

**G-4/4 KUZALIWA KWA YESU 286**

1. Kule muji wa Daudi pa’li kulisha nyama,
Mama alimulalisha Mwana wake na mapendo ;
Mama yule ni Maria, Mwana wake Yesu Kristo.

2. Yesu aliacha mbingu, akakuja duniani,
Nyumba yake, zizi bule ; na kitanda chake, nyasi ;
Alikuwa masikini na munyenyekevu sana.

3. Siku za watoto wake, vile siku za ujana,
Mwana wa kusikiliza, aliti-i mama yake ;
Na watoto wa-amini wanapashwa kuwa hivi.

4. Alikwenda pa’li pote, akifanya kazi njema,
Naye akawaponyesha watu wengi wa ugongwa ;
Akakufa kwa Kalvari kwa ajili yetu yote.

5. Tutamwona waziwazi, kwani ametukomboa ;
Mwana yule ni Mwokozi, vile Bwana wa wabwana ;
Naye anatuongoza hata atakaporudi.

6. Hututamukuta tena pa’li pa kulisha nyuma ;
Tutamwona kule mbingu, Bwana mwenye utukufu ;
Kama nyota watu wake watamuzunguka wote.

Cfr/ SSS32

**C-4/4** **UFUFUKO 287**

1. Yesu amefufuliwa, Haleluya !
Tumusifu sisi sote, Haleluya !
Mufurahi, ‘mutukuze, Haleluya !
Malaika, mumwimbie, Haleluya !

2. Yesu ametuokoa, Haleluya !
Kazi yake imekwisha, Haleluya !
Mushindaji wa Shetani, Haleluya !
Tunamutolea sifa, Haleluya !

3. Jiwe halikumufunga, Haleluya !
Alitoka kwa kaburi, Haleluya !
Hakushindwa na mauti, Haleluya !
Alivunja nguvu yake, Haleluya !

4. Yesu ni Mufalme mwema, Haleluya !
Yeye hai kutuombea, Haleluya !
Tutamwona kule ju-u, Haleluya !
Tutakuwa kama Yesu, Haleluya !

Cfr/ SSS158 IH122

**C-4/4** **UFUFUKO 288**

1. Yesu alipolala kati’ kaburi,
Giza lilifunga Yesu Mwokozi.

*Alifufuka hakika, akavunja nguvu ya mauti ;*
*Mushindaji ju-u ya mamlaka yote*
*Ni Mufalme wa milele na milele ;*

*Alikuwa amekufa, na tazama, amefufuka !*

2. Walinzi wa kaburi walikimbia ;
   Muhuri na vifungo vilivunjika.

3. Kufa hakukushika maiti yake,
   Alilivunja pingu, Yesu Mwokozi.

Cfr/ SSS152 RS352 IH121 CH118

**Bb-6/8** **UFUFUKO 289**

1. Mwokozi anaishi, ni hapa duniani ;
   Ni neno la hakika, ni neno la furaha.
   Ananihurumia, ananifurahisha,
   Na anaka-a karibu sikuzote.

*Mwokozi ni hai, ni hai kwa milele,*
*Anatembea nami kwa safari yangu yote ;*
*Mwokozi ni hai, tayari kuokoa,*
*Na ninajua namna gani ? <ni hai moyoni mwangu !*

2. Ananipenda kweli na kunichunga sana,
   Na hata ninachoka, nadumu kumufuata ;
   Katika mambo yote Mwokozi ndiye Bwana,
   Kufika siku atakaponitwa-a.

3. Nasi Wakristo wote, tusifu sikuzote,
   Tuimbe Haleluya kwa Kristo na Mufalme ;

Anapokea wote wanaofika kwake,
Hakuna anayependa kama yeye.

Cfr/ IH124 CH88

## Bb-4/4 UFUFUKO 290

1. Kristo aliacha utukufu kufika dunia yenye zambi,
Alivikwa taji ya mi-iba, na alinilipia deni yote.

*Yeye ni hai, yeye ni hai,*
*Amezishinda zambi na kaburi ;*
*Yeye ni hai, yeye ni hai,*
*Atarudia kwami.*

2. Mushindaji alitoka kufa, na alirudia mbingu kwake ;
Atakuja tena kunitwala, ili niende na kuishi naye.

3. Wewe unayesumbuka sana, Mwokozi anakuita sasa,
Uamini Yesu kupokea kwake
Uzima, shangwe, na salama.

Cfr/ IH123 CH49

## Db-4/4 UFUFUKO 291

1. Najua Yesu anaishi, yeye ni hai mbinguni kweli ;
Sababu alishinda kufa, vile uwezo wa kaburi.

*Najua Yesu anaishi, yeye ni hai mbinguni kweli ;*
*Najua Yesu ananipa uzima na uwezo wake.*

2. Najua atakuja tena, nina ahadi yake hivi ;
Na siku nitakapomwona furaha itakuwa nyingi.

3. Najua anatengeneza pahali nitakapoishi ;
Na atakuja kuni-ita na kunikaribisha kwake.

Cfr/ CH510

**Eb-4/4** **UFUFUKO 292**

1. Kwako heshima, Kristo Mushindaji,
Kwako utukufu, sifa kwa milele.
Toka kwako mbingu yule malaika
Alifingirisha jiwe la kaburi.

*Kwako heshima, Kristo Mushindaji*
*Kwako utukufu, sifa kwa milele.*

2. Tazama Yesu akishinda kufa,
Yeye ni Mwokozi, yeye Bwana yetu.
Wenye kuamini, mutangaze wazi
Neno lake Kristo ndiye Mushindaji.

3. Sitaogopa, Yesu anaishi
Ninayemupenda, Bwana ya salama.

Ninashinda naye kwa uwezo wake ;
Yeye ni uzima, utukufu wangu.

Cfr/ CV44

## Bb-4/4 KWA WOTOTO 293

1. Rafiki wa watoto ni Kristo Bwana Yesu,
Hawezi kugeuka, ni sawa kila siku ;
Rafiki za dunia wanageuka sana,
Rafiki ndiye Yesu ni sawa tu daima.

2. Pumziko kwa watoto ni kwake Baba Mungu,
Wenye kupenda Yesu wataingia mbingu ;
Mateso, maumivu, na zambi zitakwisha,
Furaha itazidi karibu naye Baba.

3. Na nyumba kwa watoto ni kwa mungini wake,
Anatawala kule na shangwe na salama ;
Na hapa duniani si kama kwake kule,
Pahali pa furaha kwa wenye kumwamini.

4. Na taji kwa watoto kuva-a kule mbingu
Ni taji ya kunga-a, na vile utukufu,
Mwokozi atawapa watoto waminifu,
Wenye kupenda Bwana na wenye kumutii.

Cfr/ RS657 CH463

**Eb-2/4** **KWA WOTOTO 294**

1. Yesu anapenda kweli, Neno lake linasema ;
   Yeye ndiye mwenye nguvu, sisi sote ni zaifu.

   *Ananipenda, Ananipenda ;*
   *Ananipenda, Biblia inasema.*

2. Anapenda, alikufa kwa kuniokoa kweli ;
   Ataosha moyo wangu ni-ingie muji wake.

3. Na anatupenda sawa saa ya afya na ugonjwa ;
   Anachunga kila siku watu wake kwa dunia.

4. Anapenda, atakuwa Mungu wangu wangu sikuzote ;
   Nikipenda Yesu kweli, atanipeleka kwake.

Cfr/ SSS1155 RS670 IH454 CH458

**G-6/8** **KWA WOTOTO 295**

1. Ninafurahi sababu Mwokozi
   Anatangaza mapendo kwa wote ;
   Ni mushangao mukubwa zaidi,
   Ananipenda mwenye zambi nyingi.

   *Ninafurahi ananipenda,*
   *Yesu Mwokozi ananipenda ;*

*Ninafurahi ananipenda,*
*Ananipenda mimi.*

2. Kama nikimusahau Mwokozi
Na nikikwenda njia nyingine,
Saa nitakapokumbuka mapendo,
Nitarudia karibu na Mungu.

3. Wimbo mumoja tu nitamwimbia
Nitakapomutazama Mupendwa,
Nitamwimbia Mwokozi milele :
« Ulinipenda – ajabu la kweli ! »

Cfr/ SSS38 RS671 CV304 CH449

**G-4/4** **KWA WOTOTO 296**

1. Yesu anataka tungae kwetu
Kama ta-a ya kuwa usiku ;
Giza linazidi duniani huko ;
Wewe nga-a kwako na mimi kwangu.

2. Yesu anataka tungae safi,
Tusiache kitu kupunguza nuru ;
Anarutazama toka kule mbingu,
Wewe nga-a kwako na mimi kwangu.

3. Yesu anataka tungae kwake
Watu wengi wasikie Neno lake ;

Na watoke giza kuingia nuru,
Wewe nga-a kwako na mimi kwangu.

Cfr/ SSS1138 RS660

## Eb-3/4 KWA WOTOTO 297

1. Bwana Yesu atakuja kutoka mbinguni,
Atawachukua wote wanaomwamini.

*Kama nyota za mbingu watu wote wa Mungu*
*Watanga-a kwa Yesu Mwokozi milele.*

2. Atawakusanya wote wanaomupenda,
Watakuwa mali yake milele mbinguni.

3. Na watoto watakuwa pamoja na Yesu,
Watanga-a kama nyota nyumbani mwa Baba.

Cfr/ SSS1140 RS659 IH455 CH459

## Bb-2/4 KWA WOTOTO 298

1. Weka makusudi mema bila kuogopa,
Usimame kwa imani kama Danieli !

*Uwe muhodari kama Danieli !*
*Weka makusudi mema bila kuogopa*

2. Wenye woga hawawezi kuingia mbingu ;
Nyosha tu bendera yake, endelea mbele !

3. Watumishi wa Shetani wanashindwa sana ;
Wakikuta jeshi la askari za imani !

4. Endelea kwa kushinda, Yesu ni Mufalme !
Taji ya uzima utapata pale kwake.

Cfr/ SSS707 IH456 CH460

## G-6/8 KWA WOTOTO 299

1. Yesu Mwokozi nataka ningae kila siku,
Nimupendeze kabisa kwa kazi na michezo.

*Ningae, ningae, Yesu 'nataka ningae ;*
*Ningae, ningae, mimi ni ta-a kwa Yesu.*

2. Yesu Mwokozi nataka nipende Mungu sana,
Na kuonyesha mapendo kwa watu wote hapa.

3. Yesu Mwokozi 'nataka nitumikie Mungu ;
Hata mutoto 'naweza kumupendeza Yesu.

Cfr/ SSS1129 RS654 CV305

**Bb-4/4** **KWA WOTOTO 300**

1. Yesu ana pendo kubwa kwa watoto wa dunia,
Anapenda kuwabarikia sana ;
« Usiwazuize kamwe, » alisema, « waje kwangu, »
Kwani yeye ni Mwokozi wa watoto.

*Yesu ana pendo kubwa kwa watoto wa dunia,*
*Hata wa kabila gani, wote ni wenye damani,*
*Yesu ana pendo kubwa kwa watoto.*

2. Yesu aliwakufia pale juu ya musalaba,
Alimwanga damu yake kuwaosha ;
Mutu anayeamini anaokolewa naye,
Na atawachunga wote kwa mapendo.

3. Watu elfu wanakufa kila siku bila Yesu.
Wengi wa watoto hawajasikia ;
Omba Mungu, vile kwenda, wasikie Neno jema
La wokovu na furaha ya mbinguni.

4. Tutangaze Neno lake hata linafika pote,
Inchi zote za dunia zisikie ;
Kila lugha na kabila wafundishwe wimbo bora
Na mbinguni watasifu Mukombozi.

Cfr/ CH445

**C-4/4** **KWA WOTOTO 301**

1. Zamani Mwokozi aliwakaribisha
Watoto wote na furaha, akawabariki ;
Alikemea wanafunzi, akasema kwa mapendo :
« Acha watoto wadogo kuja kwangu. »

2. « watoto wadogo ninawapenda sana,
Nitawachunga kama Muchungaji wa kondoo ;
Na wakinipa roho zao, nitawaokoa wote,
Acha watoto wadogo kuja kwangu. »

3. Aliwapokea na pendo na furaha,
Mikono yake aliweka Muchungaji wa kondoo ;
Na alitaka wafahamu anapenda kila mutu,
« Acha watoto wadogo kuja kwangu. »

4. Mwokozi aliwaonyesha pendo kubwa,
Lakini hapa sasa wengi hawamutambui,
Na hawajasikia bado kwamba Yesu ni Mwokozi,
« Acha watoto wadogo kuja kwangu. »

Cfr/ RS683

## Ab-4/4 KUAGANA 302

1. Bwana, sasa uruhusu watu wako kwenda kwao ;
Umetufikisha hapa, umetubariki sana ;
Umekusanyika nasi, kwenda nasi kwa mungini.

2. Tunakushukuru sana kwa baraka yako kubwa ;
Ndani ya kitabu chako umetufundisha roho ;
Tukikwenda tukumbuke Neno tuliolipata.

3. Umepanda mbegu yako, sasa uitie maji ;
Hivi tutazaa matunda, utukuzwe ndani yetu ;
Utuchunge hata siku tutakapomwona Yesu.

Cfr/ SSS287 RS945

**Db-4/4** **KUAGANA 303**

1. Mungu awe nanyi sikuzote, awabarikie wote,
Awalinde kwa amani ; Mungu awe nanyi sikuzote.

*Mungu awe nanyi daima,*
*Hata mwisho wa safari yenu ;*
*Mungu awe nanyi daima,*
*Hata tuonane kule mbingu.*

2. Mungu awe nanyi sikuzote, awalishe, awatunze
Chini ya mabawa yake ; Mungu awe nanyi sikuzote.

3. Mungu awe nanyi sikuzote, awe ngabo yenu kubwa
Katikati ya hatari ; Mungu awe nanyi sikuzote.

4. Mungu awe nanyi sikuzote, atukutanishe tena,
Ama kwetu, ama kwake ; Mungu awe nanyi sikuzote.

Cfr/ SSS298 RS942 CV286 CH541

**G-4/4** **NYIMBO NYINGINE 304**

1. Mumufanyie Bwana shangwe,
   Ee ninyi inchi zote pia ;
   Mutumikie kwa furaha,
   Kuimba sifa mbele yake.

2. Mujue Bwana ndiye Mungu,
   Ni yeye aliyetu-umba ;
   Kwa hivi sisi watu wake,
   Kondo-o za malisho yake.

3. Mwingie malangoni mwake
   Na katika viwanja vyake ;
   Mumushukuru na kusifu,
   Na kubariki Jina lake.

4. Kwa kuwa Bwana ndiye mwema ;
   Rehema yake ya milele,
   Uaminifu wake vile
   Ni kwa vizazi na vizazi.

Cfr/ SSS9 RS26 HW282 CH543

**Ab-9/8** **NYIMBO NYINGINE 305**

1. Nitasifu Mwokozi na mapendo yake kwami,

Aliyenikufilia kuondosha laana kwangu.

*Nitasifu Mukombozi ; damu yake alimwanga*
*Kwa kunisamehe zambi na kulipa deni yangu.*

2. Nitawahubiri wote Neno la Mwokozi wangu ;
Kwa mapendo na rehema Yesu alinikomboa.

3. Nitasifu Mukombozi kwa sababu ya uwezo ;
Kweli ameshinda zambi na mauti na Hadeze.

4. Nitaimba na kusifu pendo lake kubwa kwami ;
Nimepita toka kufa, nimepata kuokoka.

Cfr/ SSS896 RS17 IH109 CH16 CV20

**G-3/4** **NYIMBO NYINGINE 306**

1. Asante, Ee Mungu, kwani ulitupenda
Na kutuma Mwokozi kutukufilia.

*Haleluya, utukufu ! Haleluya kwa Mungu !*
*Haleluya, utukufu kwa Mungu Mujuu !*

2. Asante, Ee Mungu, kwa sababu ya Roho
Anayetuongoza kwa njia ya nuru.

3. Asante na sifa kwa kondo-o wa Mungu,
Ndiye aliyekufa kwa ‘jili ya watu.

4. Ee Mungu, ujaze kila moyo na pendo,
Roho zetu ziwake na moto wa mbingu.

Cfr/ RS36 IH366 CH31

## Ab-6/8 NYIMBO NYINGINE 307

1. Napenda kusikia Jina la Mwokozi Yesu ;
Ni tamu sana kila mara, linapita yote.

*Ee, ninamupenda, Ee, ninamupenda.*
*Ee, ninamupenda,* aliyenipenda kwanza.

2. Napenda Jina la Mwokozi aliyenipenda,
Aliyemwanga damu yake kwa kuniokoa.

3. Napenda Jina lake Yesu anayenipenda,
Na kutimiza mahitaji yangu sikuzote.

4. Napenda Jina lake Yesu anayefariji,
Anayebeba taabu yangu na kunisaidia.

Cfr/ IH211

## Ab-3/4 NYIMBO NYINGINE 308

1. Sifurahi kwa mali ya dunia, Ee Bwana ;

Ninataka kujua kweli mimi ni wako ;
Na katika kitabu cha ufalme wa mbingu
Jina langu ni kule ? Ninataka kujua.

*Jina langu ni kule kwa kitabu cha Mungu ?*
*Jina langu ni kule ? Ninataka kujua.*

2. Zambi zangu ni nyingi, zinazidi kabisa ;
Damu yako, Mwokozi, inatosha kwa mimi.
Ni ahadi ya Mungu : « Zambi zenu nyekundu
Zitakuwa nyeupe hata kama theluji. »

3. Ninajua mbinguni nyumba zetu ni nyingi,
Mungu anazochunga kwa wenye kuamini ?
Ninaamini Mwokozi, zambi zimesafishwa ;
Jina langu ni kule, ninajua kabisa !

*Jina langu ni kule kwa kitabu cha Mungu ;*
*Jina langu ni kule, ninajua kabisa !*

Cfr/ CH116

## Ab-2/4 NYIMBO NYINGINE 309

1. Hata tangu zamani : (3), tuna Neno lake Yesu.

*Neno lake ni kweli (3), Neno lake Bwana Yesu.*

2. Alitoka mbinguni (3), kwa kutuokoa wote.

3. Yeye mutakatifu (3), ndiye mwana wake Mungu.

4. Alikufa kwa zambi (3), hata zambi zetu zote.

5. Alitoka kaburi (3), naye alishinda kufa.

6. Alikwenda mbinguni (3), kwa kutengeneza pa'li.

7. Atarudi upesi (3), kwa kutupeleka kwake.

8. Mungu atapokea (3), wenye kumwamini Yesu.

Cfr/ RS441

## G-3/2 NYIMBO NYINGINE 310

1. Ninakuomba, Mungu Baba, unisikilize,
   Kwa maana sina Musaidizi ila wewe pekee.

   *Nina-amini kweli Yesu alikuja kwami,*
   *Na damu yake inanifungua toka zambi.*

2. Mapigo mengi Yesu alivumilia kwami ;
   Kwa ajili yangu alibeba hata musalaba.

3. Na sasa kazi yangu moja ni kumupokea ;
   Mwokozi alifanya yote kwa kuniokoa.

4. Ee Yesu, ninakuamini, ninakupokea ;
Na ninapata kwako tu uzima wa milele.

Cfr/ SSS493

## Ab-4/4 NYIMBO NYINGINE 311

1. : Utazame Bwana Yesu, aliyechukua zambi :
: Aliteswa kabisa, akavumilia yote :

2. : Sasa kuja kwake Yesu, atakuokoa wewe :
: Alikufa kwa zambi, alimwanga damu yake :

3. : Kiri zambi zako kwake, na kufuata njia yake :
: Utapata uzima na furaha kwa milele :

4. : Ujitoe sasa kwake, kumutumikia pekee :
: Roho Mutakatifu atakupatisha nguvu :

Cfr/ Bangala 49

## G-3/4 NYIMBO NYINGINE 312

1. Ninakaribia sasa musalaba wako, Bwana ;
Mwenye zambi na zaifu, bila wewe sina kitu.

*Sasa ninakuja kwako, ninaanguka mbele yako*
*Na unyenyekevu sana ; Ee, uniokoe, Bwana.*

2. Zambi zimenitawala, nimefungwa nazo sana ;

Ninakusikia, Bwana, ukisema : « Kuja kwangu. »

3. Ninakutolea vyote – mali, ndugu, mwili, roho ;
Ninatoa vyote kwako, ninataka kuwa wako.

4. Ninaamini damu yako kuniosha niwe safi ;
Kweli unanipokea ; Haleluya kwako, Yesu !

Cfr/ SSS477 RS289 IH361

**Eb-3/4** **NYIMBO NYINGINE 313**

1. Ninakusikia, Bwana, unani-ita sasa
Kufika kwako nisafishwe kwa damu ya Mwokozi.

*Ninakuja Bwana, ninakuja sasa ;*
*Unioshe nisafishwe kwa damu ya Mwokozi.*

2. Hata mimi ni muchafu, unipe nguvu yako,
Nipate kuwa safi kweli kwa damu ya Mwokozi.

3. Bwana Yesu anaita, nipate kwake vile
Imani, pendo, na salama, furaha na taraja.

Cfr/ SSS475 RS269 CH219

**Bb-4/4** **NYIMBO NYINGINE 314**

1. Usimame na piga baragumu,
Unyanyue bendera ya Yesu ;
Ujivike silaha za imani,
Kwenda kwa uwezo wake Mungu.

*Kwenda mbele chini ya bendera,*
*Kila mutu awe muhodari ;*
*Kwenda mbele, imba Haleluya !*
*Yesu Kristo ndiye Mushindaji.*

2. Tusimame imara, tupigane
Kwa upanga wa Neno la Mungu ;
Na zaidi ya yote tunatwaa
Ngabo ya imani kwa kushinda.

3. Mungu, sasa tunakuomba wewe,
Usaidie tushinde kabisa ;
Kisha tutapumzika kwako, Baba ;
Utaleta kila mutu taji.

Cfr/ SSS703 RS388 IH178

## Ab-6/8 NYIMBO NYINGINE 315

1. Nimepata salama kutoka mbinguni,
Sasa ninapumzika kwa Yesu ;
Na katika mateso na taabu ya hapa
Ninaona salama na kimya.

*Nimepata salama, ni salama kutoka mbinguni ;*
*Ni salama ya Mungu kulinda mioyo ;*
*Ndiyo inayopita kusema.*

2. Sina mali nyingine kupita salama,
Mungu aliyoleta kwa mimi ;
Na salama hii mutu hawezi kutoa,
Itakuwa milele moyoni.

3. Sasa ninapumzika katika salama,
Kwa mikono ya Yesu Mwokozi ;
Ninalala usiku pahali po pote,
Bila woga wa kitu cho chote.

4. Na wakati nitakapofika mbinguni,
Nitaona Mwokozi Mupenzi ;
Nitapiga asante kwaye kwa salama
Iliyonituliza saa zote.

Cfr/ SSS658 RS788 IH287 CH58

**G-4/4** **NYIMBO NYINGINE 316**

1. Ukae sikuzote kwake Yesu,
Atakusaidia sana kabisa ;
Utegeme-e pendo lake vile,
Naye atakuchunga.

*Ukae saa zote kwake Yesu,*

*Kumbuka mapendo yake Mungu ;*
*Ukimwamini atakushindisha ;*
*Na utegeme-e Yesu.*

2. Ukae sikuzote kwake Yesu,
Atakuongoza katika nuru ;
Utii sauti yake kwa furaha,
Atakubarikia.

3. Ukae sikuzote kwake Yesu,
Uache mateso na taabu kwake ;
Anafikili mahitaji yako,
Na atakusaidia.

Cfr/ N/A

**Eb-4/4** **NYIMBO NYINGINE 317**

1. Ninakuomba, Yesu, ndiwe kondoo wa Mungu,
Wewe Mwokozi,
Sasa unisikie, vile unisafishe,
Unitakase niwe wako pekee.

2. Kwa neema yako kubwa unipe mimi nguvu
Kwa kazi yako ;
Ulinikufilia, hivi mapendo kwake
Yawake ndani yangu kama moto.

3. Dunia ina giza, mateso, na huzuni,

Uniongoze ;
Ee, ufukuze giza, mateso, na huzuni,
Usiniache kukufuata mbali.

4. Siku ya kufa kwangu, ninapokwenda ngambo,
Sitaogopa ;
Mikono ya mapendo itanibeba kwako,
Niwe pamoja nawe kwa milele.

Cfr/ SSS235 RS580 IH409

## G-6/8 NYIMBO NYINGINE 318

1. Nasikia, Bwana Yesu, unabarikia watu ;
Ee, unikumbuke vile, unibarikie mimi ;
Hata mimi, hata mimi, unibarikie mimi.

2. Bwana, usinipitie, hata nina zambi nyingi ;
Ee, usiniache kamwe, uonyeshe neema kwami ;
Hata mimi, hata mimi, uonyeshe neema kwami.

3. Bwana Yesu, Mukombozi, nina hamu kubwa sana
Kukutumikia pekee, sasa uni-ite mimi.
Hata mimi, hata mimi, sasa uni-ite mimi.

4. Pendo lako takatifu, damu yako ya damani,
Neema yako bila mwisho, yote unanipa mimi ;
Hata mimi, hata mimi, yote unanipa mimi.

Cfr/ SSS485 IH143

## F-4/4 NYIMBO NYINGINE 319

1. Ee ninakupenda, Mwokozi Mupenzi ;
   Kwawe nina-acha furaha ya zambi ;
   Kwa maana wewe ni wangu, nami mutu wako ;
   Ee, ninakupenda kupita vitu vyote.

2. Ee, ninakupenda na sikukujua ;
   Ulininunua kwa bei ya damani ;
   Kwami ulivikwa miiba kama taji yako ;
   Ee, ninakupenda kupita vitu vyote.

3. Ee, ninakupenda kwa saa ya maisha,
   Na nitakupenda kwa saa ya mauti ;
   Na saa nitakapokwenda kwako nitasema :
   « Ee, ninakupenda kupita vitu vyote. »

4. Katika furaha na shangwe za mbingu,
   Ninakutukuza kwa nyimbo za sifa ;
   Maneno makubwa nitakayoimba kwako ;
   Ee, ninakupenda kupita vitu vyote.

Cfr/ SSS659 IH364

## F-3/4 NYIMBO NYINGINE 320

1. Maisha na mapendo yangu ninayatoa kwako, Bwana ;

Na nitakuwa wako peke, Mwokozi, Mungu wangu.

*Maisha yangu yawe yako,*
*Uliyekufa kwami, Bwana ;*
*Na kweli kwako nitapata furaha yangu yote.*

2. Nina-amini unanipa uzima wako wa milele ;
Kwa hivi nitaishi kwawe, Mwokozi, Mungu wangu.

3. Uliyekufa kwa Kalvari kuniokoa toka zambi,
Nataka kujitoa kwako, Mwokozi, Mungu wangu.

Cfr/ RS284

**Ab-9/8** **NYIMBO NYINGINE 321**

1. Ninakutolea, Bwana, roho na maisha yangu ;
Hii mikono yangu iwe kukutumikia pekee.

*: Ninatoa yote, Yesu, niwe wako kwa milele :*

2. Kwa migu-u yangu vile nitakwenda kuhubiri ;
Kwa sauti nitaimba sifa kwako tu daima.

3. Kinywa changu kitangaze Neno lako waziwazi ;
Mali yangu iwe yako, sitanyima kitu kwako.

4. Unijaze moyo wangu na mapendo kwawe, Bwana ;
Upoke-e mwili wote, niwe wako sikuzote.

Cfr/ Bangala 82

## Bb-3/2 NYIMBO NYINGINE 322

1. Bwana Yesu anaita watu wake duniani ;
Kwa sauti ya mapendo anaita : « Unifuate. »

2. Mali bule ya dunia si faida kwa milele ;
Bwana Yesu anaita, akisema : « Unipende. »

3. Katikati ya furaha, katikati ya huzuni,
Anadumu ku-uliza : « Utazidi kunipenda ? »

4. Bwana Yesu anaita ; tunapenda kusikia
Na kumupa roho zetu kumutumikia pekee.

Cfr/ IH383 CH310

## Bb-4/4 NYIMBO NYINGINE 323

1. Ee, Yesu atakuja tena katika mawingu,
Na sauti kubwa Bwana atashuka toka mbingu ;
Macho yetu yataona utukufu wake Mungu ;
Ee, Yesu atakuja !

*Tutaona utukufu siku ya kuona Yesu ;*
*Tutaimba Haleluya kwa Yesu ndiye Bwana !*

2. Ee, Yesu atakuja tena kwa kutupokea ;
Tutakwenda kwa mungini wake kule kwa mbinguni ;
Atakuja na baraka, kweli tunamungojea ;
Ee, Yesu atakuja !

3. Kwa maana Yesu alikufa  kwa kutuokoa,
Tunapashwa kwenda sasa kuhubiri watu wote,
Hata wa-amini Yesu kuwa Bwana na Mwokozi ;
Ee, Yesu atakuja !

4. Ee, ndugu, wewe ni tayari kwa kuona Bwana ?
Zambi zako zimesamehewa, unaamini damu ?
Jina lako linaandikwa kwa kitabu cha ufalme ?
Ee, Yesu atakuja !

Cfr/ Bangala 91

## G-3/2 NYIMBO NYINGINE 324

1. Mateso mengi duniani, hatuna nyumba nzuri hapa ;
Lakini kule kwake Baba tutafurahi kwa milele.

*Ee, Haleluya kwake Mungu,*
*Sababu ninakwenda mbingu ;*
*Huzuni na machozi yangu*
*Hayatakuwa tena ngambo.*

2. Nilizaliwa bila kitu, muchafu, bule, na zaifu ;

Mutupu nilifika huku, mutupu nitarudi kule.

3. Ninasafiri duniani kufika muji wa mbinguni ;
Mwokozi alikwenda kule kutengeneza nyumba zetu.

4. Naona masumbuko mengi saa zote hapa duniani ;
Lakini kule ni furaha, nitapumzika kwake Baba.

Cfr/ Bangala 102

## D-4/4 NYIMBO NYINGINE 325

1. Wachunga walilinda kundi la-o kwa usiku ;
Tazama, malaika aliwatokea mbio,
Kutoka kwake Mungu.

2. Na utukufu wake Bwana ukawaangazia ;
Wakaogopa sana wakiona nuru ile,
Wakashutuka kweli.

3. Na malaika yake Bwana akawa-ambia :
« Musiogope, kwani ninawaletea ninyi
Habari toka Mungu.

4. « Habari Njema ya furaha itakayokuwa
Kwa watu wote wa dunia, ninaleta kwenu
Habari Njema hii.

5. « Kwa maana mutajua leo tu amezaliwa

Katika muji wa Daudi kwa ajili yenu
Mwokozi Kristo Bwana.

6. « Na hii alama kwenu mutamwona kwa kizizi,
Amelalishwa kwa sanduku ya kulisha nyama ;
Mutamukuta pale. »

7. Kwa gaf'la makutano ya majeshi ya mbinguni
Walizunguka huyu malaika yake Bwana,
Na walisifu Mungu.

8. « Ee utukufu kwake Mungu, kule kwa mbinguni ;
Salama duniani kwa wanaomupendeza ;
Ee, sifa kwake Mungu. »

Cfr/ IH51

**G-4/4 NYIMBO NYINGINE 326**

1. Wachunga walilinda kundi la-o kwa usiku ;
Tazama, malaika aliwatokea mbio.

2. Na utukufu wake Bwana ukawaangazia ;
Wakaogopa sana wakiona nuru ile.

3. Na malaika yake Bwana akawa-ambia,
« Musiogope, kwani ninakuja na habari. »

4. « Habari Njema ya furaha itakayokuwa

Kwa watu wote wa dunia ninaleta kwenu.

5. « Amezaliwa leo tu kwa muji wa Daudi
Mwokozi ndiye Kristo Bwana, kwa ajili Yesu.

6. « Na hii alama kwenu mutamwona kwa kizizi,
Amelalishwa kwa sanduku ya kulisha nyama. »

7. Kwa gaf'la makutano ya majeshi ya mbinguni
Walizunguka malaika wakisifu Mungu.

9. « Ee utukufu kwake Mungu, kule kwa mbinguni ;
Salama duniani kwa wanaomupendeza ;

Cfr/ SSS33 RS501 Bangala 109

**Ab-6/4** **NYIMBO NYINGINE 327**

1. Siku mateso yatakapokwisha,
Kule mbinguni nitakapofika,
Kuwa na Yesu Mwokozi karibu,
Hii ni furaha kupita kipimo.

*Hii ni furaha, na utukufu,*
*Na utukufu, na utukufu ;*
*Kuwa na Yesu Mwokozi karibu,*
*Hii ni furaha kupita kipimo*

2. Kwa maana nimeamini Mwokozi,

Nitamusifu daima mbinguni ;
Kumutazama kwa macho karibu,
Hii ni furaha kupita kipimo.

3. Ndugu wananingojea mbinguni,
Tutafurahi pamoja milele ;
Yesu akinipokea karibu,
Hii ni furaha kupita kipimo.

Cfr/ SSS949 RS356 IH501 CH427

COPYRIGHT AOUT/2015 Par Fr Dieudonné MW